VERBATIM REPORT OF

# MATUGA CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, AT KWALE COUNTY HALL

ON

MAY 3, 2002.

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MATUGA CONSTITUENCY HELD AT KWALE COUNTY HALL ON 3RD MAY, 2002.**

**Present**

1. Com. Dr. Mohammed Swazuri – Chairperson
2. Com. Nancy Baraza – Commissioner
3. Com. Bishop B.K Njoroge – Commissioner

**Secretariat Staff in attendance**

1. Peter Apamo - Programme Officer
2. Edgar Kagoni – Assistant Programme Officer
3. Jacqueline Nyumoo – Verbatim Recorder
4. Mwero wa Mkalla – District Coordinator

The meeting was called to order by Com. Swazuri in the chair and it started at 9.45 a.m.

**Com. Swazuri:** Wananchi watukufu Salaam Aleikum.

**Audience:** Aleikum Salaam.

**Com. Swazuri:** Haya, tumekuja hapa kama tulivyoahidi mara nyingi sana na hall ni hii hii. Tuliahidi tutakuja tuwapatie nafasi mseme mnayotaka. Leo tumefika. Huyu mwenzangu hapa ni Commissioner anaitwa Bishop Benard Njoroge Kariuki, na huyu ni Commissioner anaitwa Nancy Baraza. Mimi mnanijua naitwa Swazuri. Kwa hivyo tutaanza na maombi. Nani leo atatupatia dua? Sheikh Kassim.

**Sheikh Kassim:** Salaam Aleikum Warakba Tulai Wabarakatu. (prayed in Arabic). Eeh Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, tunakuomba asubuhi ya leo Ya-Allah utuweke katika amani yako. Ya-Allah ee Mwenyezi Mungu tunakuomba tutakayokuzungumza hapa Ya-Allah, yatiliwe maanani Ya-Allah na kuwekewa njia. Ya-Allah Mwenyezi Mungu tujaalie tuwe na uwezo wa kutengeneza Katiba ina manufaa. Katiba ambayo kwamba itakayotufaa sisi na vizazi vyetu. Katiba ambayo kwamba itaongoza nchi hii. Katiba ambayo itatuongoza sisi na watoto wetu. Ya-Allah ee Mwenyezi Mungu tupe amani, tupe masikilizano. Viongozi na makamishina walioko hapa Ya-Allah Mwenyezi Mungu wape uzingativu wa maoni yetu, wape uzingativu wa mafikira zetu. Ya-Allah ee Mwenyezi Mungu fungua mabongo yetu tupe fikra nzima, fikra ambazo zitajenga. Ya-Allah na wale wageni ambao kwamba wamekuja uwapishe makao kwa salama.

**Com. Swazuri:** Shukrani, sasa utaratibu wetu ni kama ifuatavyo. Kuna njia tatu za kutoa maoni. Ya kwanza, ni kuleta memorandum (mswada) na usiusome. Nikisema hivyo, utaenda pale, utaandikisha jina lako na mswada, utaandikisha jina lako na mswada utaandikishwa pale, sisi kazi yetu tutakwenda kusoma.

Pili, umeleta mswada na unataka kuupitia. Tunataka upitie mapendekezo tu, usiseme shida zilizoko pale ndani. Dakika tano halafu sisi tutakwenda kusoma ule mswada. Kwa hivyo usome yale ambayo ni ya umuhimu unayopendekeza. Tatu, kuna kutoa maoni sasa kwa kusema tu. Huna mswada, huna nini, kusema tu. Hata hiyo pia tutakupa dakika tano ili watu wote wapate nafasi ya kusema. Tuliwaambia tukija hapa tutakaa mpaka nyinyi wenyewe mseme basi na tumekuwa tukifanya hivyo kutoka tuanze. Juzi Samburu, Kinango, Shimba Hills tunakaa mpaka hall inakuwa haina mtu ndio tunaondoka. Kwa hivyo ikifika ni wakati wa Ijumaa, wanaokwenda kuswali, wataenda kuswali sisi tuko hapa.

Sisi hatuendi lunch, mpaka tuwasikilize nyote. Sawa hapo? Haya, karibuni. Dakika tano tano ili kila mmoja apate nafasi. Watakaokuja tutawakaribisha namna hii. Omari Maganga. Utakaa hapo.

**Mr. Omari:**. Mimi kwanza natoa shukrani kwa nafasi hii kuipata ambayo kwa kusema ukweli kwa upande wetu imekuwa ni kitu kizuri au kipya sana maanake hatukuwa tukitarajia. Kwa hivyo sitachukua muda mrefu. Kwa kifupi mimi mapendekezo yangu kuhusu katiba, utaratibu wa katiba, mchango wangu ninaotoa kwamba tunataka katika, serikali ya kenya iwe na Majimbo. Majimbo ndio mapendekezo yangu, na iwapo Mwenyezi Mungu atajali Majimbo yaingie itakuwa ni maana kwamba

watu wenyewe walio na jimbo mapato na shughuli zinazofanywa zifanywe kuhusu jimbo lenyewe jinsi vile ambavyo litaweza kujisaidia na matatizo yaliyoko katika jimbo.

Sitachukua muda mrefu sana hata hizo dakika tano kwangu naziona nyingi lakini kwa pale nilipofikia hiyo yatosha, nitaiwacha nafasi hii kwa wenzangu wafuatao lakini lengo na madhumuni ni Majimbo uhuru wa kenya upate Majimbo. Hili ni neno ambalo lina uzito kwetu, kenya iko huru na haina Majimbo. Kwa hivyo tunataka jimbo tafadhali, huenda likatupunguzia taabu.

**Com. Swazuri:** Ngoja kidogo.

**Com. Baraza:** Asante sana mzee Madanga. Hiyo Majimbo unafikiria ipangwe namna gani? Unaonelea hili jimbo lako liwe style gani?

**Bishop Njoroge:** Ningetaka kuongeza. Katika hilo jimbo lako, ungetaka utawala uwe namna gani? Na pia katika hili jimbo ungetaka lifanye kazi kwa njia gani pamoja na Central Governmentiliyoko Nairobi?

**Mr. Omari:** Wakati Majimbo yakija, mimi vile ninavyofikiria kwa kichwa changu ni kwamba jimbo lenyewe litakaa kutakuwa na wazee ambao watazungumza vile taratibu za jimbo zitakavyokuwa likiwakilisha watu lakini kulingana na hilo swali sasa iwapo Majimbo yatapatikana, katika jimbo lile ambalo ni langu, tuna taabu ambayo pia itapungua kwa sababu katika pato la jimbo tunataka 75% ibaki kwenye jimbo, 25% iende katika serikali kuu.

Hivi hutufanya sisi kidogo tuwe na nafuu kwa sababu kwanza kati yetu baadhi yetu wengine tu wangojwa lakini hatuendi hospitali, si kwamba tunaweza ugonjwa lakini gharama iliyo hospitali ni ya ajabu, sisi hatuna chochote pia. Jambo la kusikitisha ni kwamba pesa za kumpeleka mgonjwa hospitali ni taabu. Leo nimepelekwa hospitali nimekufa kule, hupati maiti mpaka kwanza ulipe na pesa ni za taabu. Itakavyokuwa 75% itabaki hapa, huenda ikatusaidia pengine tukifa hospitalini tukachukuliwa na sehemu hizo. Basi nina mengi yafuatayo kama maskuli. Nafikiri nimeweka sawa hapo kwenu. Sipendi kuchukua muda mrefu kwa sababu sote tuko hapa tukizungumza haya. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Omari Macharo.

**Mr. Mwacharo:** Asante sana mwenyekiti, jina langu ni Omari Juma Mwacharo. Mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuzungumza mambo machache tu. Sina mengi ila ninamuunga mkono msemaji aliyezungumza awali kwa sababu mambo mengi hapa Pwani yanaharibika na kuharibika kwake si makosa ya serikali bali ni makosa ya viongozi wetu. Na ikiwa tutapata Majimbo nafikiri kila mmoja atajiangalia mwenyewe mipango yake vile inaendelea. Nafikiri kwa hayo machache nasema asante sana.

**Com. Swazuri:** Said Mwakafani. Nenda pale mzee uandike.

**Mr. Said:** Bwana chairman, mimi kwa jina ni naitwa Said Ramadhani Mwakafani. Maoni yangu ni kama yafuatavyo. Kwanza naiomba Katiba katika serikali apawe chief Kadhi mamlaka ambayo yatamwezesha kufanya kazi zake kama wale majaji wengine katika ngazi yake. kinyume cha sasa ambacho kwamba Kadhi yule anachaguliwa kwanza na kazi zake ni mbili ama ni tatu. Ya kuoza, ya kutalaki na kuridhisha ambapo maswala mengine yote ya Kiislamu hayaangalii na tumo katika mwongozo wa Kiislamu katika Korani tunaambiwa ya kwamba waislamu wamwamini Mwenyezi Mungu na MTumena wenyewe amri juu yao. Na mwenye amri juu yetu ni chief Kadhi basi naomba awe na mamlaka kamili. Pili, serikali naiomba iwape waislamu katika hali ya kuabudu kisawasawa tofauti ya kwamba, iwapo wengine wanabaguliwa na wengine hawabaguliwi kwa mfano kupawa kibali cha kuendesha mambo fulani.

**Com. Swazuri:** Fafanua hapo.

**Mr. Said:** Hapo nafafanua kusema kwamba iwapo pengine ni kongamano la waislamu wanataka kufanya mambo fulani, kuna mshikili mshikili, yaani wanazuiliwazuiliwa kiasi cha kwamba wanafikiriwa kana kwamba wao watazungumza kinyume cha serikali kwa hivyo wao wenyewe wanachukuliwa kama raia wale halisi na watu wengine wa madhehebu tofauti tofauti.

Tatu, ni kwamba waislamu wanaomba ama ninaomba Katiba iondoe ile sheria inayofanya mwanamke awe sawa na mwanamume kwa sababu inapinga Korani tukufu sura ya nne, aya ya thelathini na nne ambapo mume amepawa jukumu kuliko mwanamke. Tatu, tunaomba Katiba hii ibadilishwe iwe ya kimajimbo kama ifuatavyo; Wale walioko katika jimbo, waandikishe wawe katika sehemu ile wakijulikana ni wangapi bila mtu yeyote kufukuzwa lakini wawe na mamlaka maalum ambapo wao wenyewe watayakalia halafu wawe wanachagua wajumbe ambao watakwenda katika serikali kuu yaani central government. katika mapato yanayopatikana pale wale walioandikishwa pale kama raia wa jimbo lile wawe ndio wanaweza kufaidika, 75% ili wafanye mambo yao. Hivyo hivyo kuwe na uhuru kwamba pakipatikana pengine watu fulani wanatakikana wafanye kazi katika jimbo hili kutoka jimbo jingine kuwe na uhuru wa kufanya hivyo kama vile serikali inavyowachukua watu kutoka sehemu za nchi zingine kuja kutoa ujuzi hapa kwetu. Kwa hivyo rasilimali zote zinakuwa ziko chini na sheria zote zinakuwa ziko chini ya wale walioandikishwa. Na iwapo pengine wengine katika Majimbo mengine hawataki, sisi Wapwanituwe kama vile Tanzania na Zanzibari. Sisi Wapwanitupate letu na wale watanzania walivyo nao wawe na sehemu zao. Hayo ni maoni ambayo ningependa Tumehii iweze kuchukua.

Katika mamlaka ya ardhi, kuna yule raia ambaye ni mzaliwa na yule raia ambaye amechukua kibali. Yule mzaliwa aangaliwe zaidi kuliko yule ambaye amechukua kibali kwa sababu kizazi chake chote kimetoka pale na apawe priority ya kwanza katika hali ardhi. Napenda pia kuzungumzia kwamba, Rais ambaye atachaguliwa asiwe na mamlaka ya moja kwa moja ya kwa mfano wa kulivunja Bunge, pili kuwachagua makamishina wa Tumembalimbali na kuwachagua majaji bali kazi hizo tatu nilizozitaja ziwe chini ya mamlaka ya Bunge na kamati ya Bunge kwa sababu ikiwa atachaguliwa na Rais, Commission ile haitakwenda zaidi ama

kinyume cha yule aliyemchagua. Unapomchagua mtu wewe umefanya akusikilize kwa sababu Bunge litakuwa na mamlaka zaidi, hayo yatakuwa na mamlaka ya kila pahali na uhaki uweze kutekelezwa. Asanteni sana.

**Bishop Njoroge:** Umesema kwamba hali ya mashamba kwamba yule ambaye ni mzaliwa apate na haki kwanza kabla ya wale wamepewa kibali cha kuwa mwananchi. Ningetaka kuuliza hivi tutafanya nini tupate haya mashamba kwa sababu tayari kama hapa Pwanimashamba imechukuliwa na wana title deed zao. Sasa hiyo ungetaka tufanye nini?

**Mr. Said:** Asante sana. kuna sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni squatter, yaani sehemu ambayo serikali imeifanya ni squatter. Kwa hivyo wakati inagawanya sehemu kama ile waangaliwe wale vizazi wa kuzaliwa halafu ndipo wale ambao wamo kwa kibali kwa kibali. Pili, kuna sehemu fulani ambapo tumeona kwamba vibali vile ambapo si squatter lakini vimepatikana kwa njia ambayo si halali hata inawezekana kwamba mtu alikufa lakini akafufuliwa kimaneno na akauza shamba. Mambo kama hayo pia yaangaliwe na ipatikanapo sababu nzuri kwamba imehusika ama imechukuliwa na yule kimakosa, serikali iweze kuirudisha chini ya mamlaka ya wazee ipate yule ambaye ni haki miliki kwa kuzaliwa. Asante.

**Bishop Njoroge:** Nauliza, kuna wengi ambao wana mashamba makubwa mpaka ma-acre maelfu hapa pwani. Kuna wengi wana ma-acre maelfu. Ungetaka ikae hivyo hivyo au ungetaka kufikiria nini ili Katiba ifanye nini. Ungetaka kufikiria habari ya ceiling ambayo mtu anahitaji kuwa, ningetaka tu kusikia kwa sababu hapa ninaona kama kuna matatizo ya mashamba na wakati huu ndio wa kusema kwa sababu msiposema sasa hakuna wakati mwingine mtasema.

**Mr. Said:** Asante sana. kwa wale ambao wana mashamba makubwa makubwa kuwe na utaratibu kama ufuatavyo. Kuwe na kiwango fulani ambacho serikali itaweka ili ikiwa kwa mfano mtu ana hekari kama mia moja basi apawe kiwango fulani kama thelathini na waangaliwe wale ambao ni landless yaani hawana chochote waweze ijapo robo ili ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini katika nchi yetu. Asante sana.

**Com. Swazuri:** Ali …….

**Sheikh Ali Hamisi:** Salaam Aleikum Warakba tulai wabarakatu. Maofisa ambayo mnachukua maoni au maneno ambayo ni ya watu wa Kwale kuhusu katiba. Marekebisho ya katiba. Kwanza mimi nina masikitiko kwamba Katiba ya zamani,

**Com. Baraza:** Jina lako.

**Sheikh Ali:** Samahani jina langu ni Sheikh Ali Hamisi Gakucha kama alivyosoma Bwana Swazuri. Masikitiko ni kwamba Katiba ya zamani sikuisoma, sasa naambiwa nitoe maoni ya marekebisho ya katiba. Pili, serikali iliyopo, serikali inayotuongoza sasa twataka iwe serikali ya Majimbo. Pili, serikali iliyopo na hiyo ya Majimbo ambayo tutaitaka ni kwamba sisi wananchi tulipopata uhuru tuliambiwa tunapigania ardhi, elimu, afya na mambo mengineo. Sitaki kueleza kila mtu hayo maneno ayajua

lakini ardhi ndio serikali, maofisa wa serikali walifanya kuwa hizi ardhi maanake sisi ni masquatter. Sisi watu tuliokuja hapa ni masquatter.

Kwa hivyo hatukumiliki ardhi na tuko katika nchi yetu na twasemekana tuko huru, sasa serikali hii hii yataka turekebishe katiba. Je, serikali hii itarekebisha zile ardhi zetu zilizopotea au tutakuja rekebishiwa ni ile serikali ambayo twasema twataka Majimbo. Basi tunaiambia serikali iliyopo ambayo imewaleta nyinyi maafisa twataka yale mashamba yetu yaliyonyakuliwa na maofisa wa serikali mpaka mtu mmoja akaweza kuwa na acre elfu tatu. Mashamba yetu, turejeshewe, tuyamiliki halafu sasa tuone hiyo serikali ya Majimbo itakayokuja, tuwe tuko katika ardhi yetu.

Upande wa elimu, tuliridhi elimu ya kiingereza kutokana na serikali ya mkoloni lakini serikali hii hii yetu tuliyoiunda sisi ambayo inatuongoza sasa ilibagua katika Islamic education haikuwatia maanani. Kwa hivyo ni masikitiko kwamba mwislamu amesoma Korani peke yake lakini ukampeleka Saudi Arabia hawezi kuzungumza kiarabu. Kwa hivyo twataka Islamic education standard education. Serikali ianzishe std. 1,2,3,4 ili mtoto asome kizungu pale asome kiarabu, asome na Korani ili mtoto akitoka chuoni maanake ilikuwa ni chuo lakini twataka skuli. Twataka skuli kama vile std. 8, mtoto akifika std. 8 ajua kuzungumza kizungu apelekwa Alliance Nairobi skuli lakini katika Korani hakuna mtoto atokaye chuoni huku Kwale hawezi kufika hata hapo Likoni. Kwa hivyo twataka elimu standard education ya Kiislamu.

Nyingine, mwananchi wa kenya kuna maofisa ambao ni police officers. Police officers ukikutana naye akwambia wewe kaa chini. Hii wewe 'kaa chini' na mimi nimetawala, ni mfalme ni kenya huru. Mtoto mdogo ni askari, ni afisa wa polisi amwambia mzee kama yule 'kaa chini na usizungumze'. Hii sheria twataka iondoke ya kukalishana chini na kusukumana virungu kwa sababu sisi ni watu huru. Twaiomba serikali iondoshe hii mambo ya kukalishana chini. Ofisa wa polisi amwone mzee, shikamoo bwana mimi najitambulisha ni ofisa wa polisi, nilikuwa na maswali nataka kukuuliza, kiheshima kuwa mtu huru. Kwa hivyo hii sheria ya kukalishana chini iondoshwe.

Ya kumalizia ni kwamba rasilimali zetu za watu wa Pwanizilivurugwa na serikali iliyopo. Sisi hatuna rasilimali unavyoona sisi sote hatuna rasilimali. Hatuna chochote, kwa hivyo hii serikali ikiwa nasema turekebishe Katiba ni kwamba zile mali zetu zilizovurugwa tukizitaja hapa zitakuwa ni hizi kubwa, wataturegeshea maana waliziharibu serikali. Je, serikali itarekebisha? Kwa hivyo ikiwa wataka tutoe maoni, twataka rasilimali zetu zilizoharibiwa zirekebishwe na serikali hii hii.

Rasilimali ni kama bandari yetu. Bandari yetu ki-history ya mwingereza ilikuwa kuna ushuru unagawanywa mara tatu. Kulikuwa kuna ushuru unagawanywa na mwingereza. Zilikuwa ni pesa kidogo lakini zilikuwa zikigawanywa, zikitoka port pale, mara tatu. Mara ya kwanza ikiwa serikali yenyewe, mara ya pili pesa hizi zilikuwa zinavuka zinakwenda Changamwe, pesa hizi zilikuwa zinakuja digo na nyingine zinabaki pale Mombasa. kwa hivyo ilikuwa hizo senti zinaangalia maslahi ya elimu. Kwa hivyo tunataka bandari yetu ile pesa ambazo zilikuwa zikigawanywa na mkoloni, hii serikali yetu itugawanyie pesa zetu maanake pesa zote siku hizi zaenda katika treasurer. Pesa za port zote mamilion katika treasurer. Ndio sisi tunakuwa hali ya chini. Kwa hayo

machache asante sana.

**Com. Swazuri:** Nenda uandikishe jina lako pale. Tumpate bwana Ali.

**Mr. Ali:** Salaam Aleikum. Mimi sitaki kuzungumza sana. maoni yangu kwanza, mimi nina maoni mara mbili hapa. Nina maoni yangu ya kibinafsi, na maoni ya wanakijiji wangu. Maoni yangu ya kibinafsi nataka Katiba hii itakayoanza, ama tutakayoitengeneza maoni yangu ili jina la kenya libadilishwe. Kimaoni yangu ni kwamba, hili jina Kenya halikukusudia wananchi wa kenya mzima. Bali maoni yangu nawaahidi neno kenya, ni neno ambalo kwamba limetengenezwa na taifa fulani ama na jamii fulani. Ndivyo nilivyoelewa mimi. Na nimejaribu kuuliza maana ya kenya nini mpaka sasa sijapata. Maana ya kenya ninavyoelewa mimi hii K ni Kirinyaga, E ni Embu, Nya ni Nyandarua. Muungano wa mataifa haya ndio ilitengeneza kenya.

Kwa hivyo maoni yangu mimi nataka iwe jina la kenya iwe serikali ya demokrasia ya muungano wa bara wa pwani. Maoni yangu nataka iwe serikali ya demokrasia ya muungano wa bara la Pwanina wala sio kenya. Hayo ni maoni yangu. Serikali ama mfumo wa serikali- nataka serikali ya Majimbo. Serikali ambayo kwamba itamiliki, kila jimbo limiliki mahali yake kama ilivyozungumzwa, asilimia themanini iwe wafanya kazi iwe wa jimbo lile.

Iwe na Rais ambaye atachaguliwa serikali hiyo ya muungano. Iwe na Rais ambaye atachaguliwa na raia. Ambaye kwamba atakuwa si wa serikali kuu na kila jimbo liwe na Rais wake yaani governor. Pili, mali asili. Kiwango cha mapato kutoka mahali ya asili kigawanywe kama ifuatavyo. Asilimia hamsini ipatiwe wilaya iliyo na mali hiyo. Asilimia thelathini ipatiwe mkoa ulio na mali hiyo na asilimia ishirini ipatiwe serikali kuu. Mwananchi aliyepakana na mali asili mfano mbunga za wanyama, msitu, bahari na kadhalika, anufaike na mali hiyo, kwa mfano kupatiwa shule, hospitali, maji safi na misaada ya masomo.

Mali asili iliyoko shambani mwa mtu. Mtu huyo apatiwe asilimia hamsini ya faida ya mali hiyo. Utalii na mbunga za wanyama- shule ya utalii ijengwe Pwanikwa sababu Pwanindio kuna utalii kwa wingi. Asilimia themanini ya wafanya kazi wanaofanya kazi katika mahoteli, iwe ni watu wa pwani. Mapato yanayopatikana kutokana na mali ya utalii asilimia hamsini ipatiwe wilaya, thelathini ipatiwe mkoa na ishirini ipatiwe serikali kuu.

Ardhi- watu walionunua mashamba zote hizi ziondolewe na waruhusiwe pesa zao na mashamba hayo yagawanywe kwa masquatter ambao kwamba hawana ardhi. Sehemu zifuatazo Vanga, Shimoni, Wasini, Garsen na Mombasa ni ardhi ya watu wa asili na hao ni wadigo. Mazrui ni wageni wa wadigo, asili ya ardhi ya Kwale, ni ya wadigo na waduruma. Kama wataka nirudie nitarudia hapo. Iwe ni ardhi ya wadigo kama vile wanadai katika ile chama cha wamiji kwamba hizo sehemu ni zao. Wana miji kumi na moja, kuanzia shimoni mpaka Lamu, wanadai katika chama chao hii ni sehemu haiko katika Katiba ya zamani. Kwa hivyo twataka hii miji yote ambayo kwamba nimezungumza ifikishwe kwa wenyeji wa asili ambao ni wadigo na waduruma na wala sio hao mazrui, waarabu walikuja tu.

Bunge- mBunge atengewe muda wa kukutana na kamati maalum kutoa kila ward ama location kutadhmini maendeleo ya sehemu hiyo ya uakilishi Bungeni. MBunge akikiuka kanuni hiyo kukutana na wale viongozi ambao kwamba wamechaguliwa location atolewe Bungeni maanake sasa Bunge anaweza kukaa bila hata kukutana na watu wake na hakuna njia ya kumwondoa kwa hivyo kuwekwe vifungu kama hivyo ukutane na watu muda kadha akipatikana kwenye vikao hivyo atolewe.

MBunge maalum asiwe mtu aliyeshindwa kisiasa alipigania akaangushwa halafu anachaguliwa na Rais anakuwa waziri. Huku ni kufedhehesha  wale wananchi ambao walimwangusha. Kwa hivyo asichaguliwe kabisa. Kuwe na kamati maalum ya kutadhmini mishahara ya waBunge na marupurupu yao. Umilikaji wa ardhi- wananchi wawe na uwezo wa kumiliki crown land kwa uhusiano wa baraza la wilaya ya wilaya. Mtu asiwe na shamba kubwa lenye hekari ya zaidi ya mia moja, kuwe na minimum. Kenya hii kusiwe na mtu ana hekari hamsini ama hekari elfu hamsini na kuna mwingine hana kabisa. Kwa hivyo kiwango cha juu kabisa kiwe hekari mia moja kwa kenya nzima kwa yale mashamba makubwa makubwa.

Kila mwananchi awe na si chini ya hekari ishirini katika yale mashamba madogo madogo. Unaona mtu anakosa shamba kwa sababu shamba lote limechukuliwa na watu wawili katika district nzima. Kwa hivyo kuwe na kiwango maalum. Kadhi mkuu- achaguliwe na Tumemaalum. Tumehii iwe ni ya watu kutoka kila wilaya humu nchini. Tumeiwe na uwezo wa kupendekeza mtu awe na kiwango ya kupendekeza mtu ambaye kwamba atakuwa Kadhi mkuu na mwenye kupendekeza awe ni kiwango cha elimu, dini awe na sheria ya Kiislamu. Na katika mambo ya kizungu awe na sheria ya kizungu vile vile ya kiingereza na zaidi. Awe muumini na tabia nzuri, sio Kadhi achaguliwe na yeye ndio anakwenda kuzungumza na barabara kama tulivyo wakati huu. Kadhi anakwenda huko anacheza na mabati yaliyowekwa kujengewa nyumba. Umri asiwe chini ya miaka thelathini na tano. Kadhi mkuu akichaguliwa awe na kuanzia miaka thelathini na tano kuendelea mbele. Asiingiliwe kikazi, awe na uhuru wa kuamua maswala ya dini bila ya kuingiliwa na serikali. Tumehiyo ya Kadhi iitwe Kadhi service Commission na iwe na mamlaka ya ofisi ya Kadhi.

Basi ungeniacha nikazungumza kitu kimoja kisha. Nataka kuzungumza kwa upande wa wanawake kwa sababu inaonekana hili jambo la wanawake limetutia matatizo sana. viwango vya uongozi vya wanawake au viwango vya wanawake vya uongozi. Maoni yetu tulikaa tukapitisha ya kwamba mwanamke wa Kiislamu awe na uwezo wa kuongoza mpaka daraja ya makamu wa Rais. juu kuwe na Rais yeye awe hapa chini. Itakuwa ni dhambi kumsomesha mtoto mpaka afike university halafu umwambie aje awe mwanamke wa jikoni. Itakuwa ni laana. Kwa hivyo tumependekeza sisi kwamba wanawake wa Kiislamu waweze kuongoza mpaka daraja ya makamu wa Rais ama kama kuna Rais awe waziri mkuu. Asanteni. Kuna maswali ama niondoke.

**Bishop Njoroge:** Nataka kukuuliza, hawa watu wana mashamba makubwa na umesema vile ni acre mia moja ikiwa mtu anaweka elfu mbili ungetaka ile ikiondolewa apewe compensation na serikali au anyang'anywe yote bila kupewa chochote.

**Mr. Ali:** Swali lako ni nzuri. Sio kwamba anyang'anywe kwa sababu kumnyang'anya itakuwa ni kumdhulumu. Kufanywe kiwango fulani ambacho kwamba atapewa kama ridhaa ya ile sehemu ambayo kwamba imechukuliwa na serikali. Asante.

**Com. Swazuri:** Andika jina lako pale. Halima Chivumbe.

**Mrs. Chivumbe:** Jina langu naitwa Halima Chivumbe, mimi ni kiongozi wa akina mama wilayani Kwale. Maoni yangu ningependa serikali hii ambayo tuko nayo katika Katiba hii ibadilike na iwe serikali ya Majimbo. Tukisema Majimbo hatujasema watu wa bara waende kwao lakini bado tunasema kwamba hapa si kwao. Kwa hivyo tunasema 75% ya chochote katika jimbo hili la Pwanilipatiwe wenyewe wa Pwanina labda 25% tupatie wageni wetu kwa sababu si vizuri hata kule manyumbani mwetu huwezi (spoke in kidigo)

Halafu katika hiyo hali ya serikali ya Majimbo, tukasema kwamba katika mali zetu hizi ambazo ni za asili kama vile kilindini na sehemu zinginezo watu wenyewe wa jimbo la Pwani au katika serikali ya Majimbo tupatiwe mamlaka zaidi ya kumiliki vitu vyote katika jimbo hili. Tunakuja sasa upande wa utalii. Utalii ni sector muhimu katika hii sehemu yetu lakini utaona mwenye hapa hanufaiki na chochote kwa hivyo mimi bado nasema kwamba katika hali ya utalii pia mwenye hapa apate 75% kwa sababu yeye ndio mwenye hapa mahali, kuanzia mahotelini, na hata sehemu nyinginezo.

Tukija kwa utalii tena utakuta kuna hizi rasilimali zingine kama ndovu. Kweli ndovu ni wazuri wana utalii lakini sisi wanatuudhi sana hapa kwetu kwa sababu ndovu anapokula mahindi yako hakuna hata mtu ambaye anakuuliza wala anakuhurumia na anapokuua wewe au akiua mwanao labda wewe utatoa shillingi elfu thelathini. Elfu thelathini ni kitu gani? Sisi tunasema kwamba hatuwataki ndovu na kama tunawataka, basi wakiwa wengi wafanywe kama nchi zingine kule Zimbabwe wanachukuliwa wanauzwa sehemu zinginezo na nyama zao kuna wengine wanakula nyama za ndovu huko wauziwe hizo nyama za ndovu na sisi tupate pesa zirejee hapa kwetu Pwanitupate kunufaika.

Lingine ni kwamba katika serikali yetu iliyoko haikujali sana viwanda katika sehemu ya pwani. Utakuta viwanda vingi vimekufa hatuna chochote na sasa mwananchi wa kawaida kitu ambacho anakiangalia ni mnazi peke yake. mnazi huu una maneno mengi, mnazi una maarifa yake, mnazi unatilia mboga lakini hakuna mtu ambaye anautambua. Tunasema hata sisi mnazi utambulike kama vile ulivyo kule Malaysia, Mauritius ambako wanafanya vitu vingi kutokana na mnazi.

Lingine pia mnazi huu kule ambako wengine tunatoka unatumika kuuzwa na hata watu wakinywa wanalipa skuli ya mtoto. Sasa tunasema hii tembo ya mnazi ifanywe kama tembo zingine, ihalalishwe na iwe well done na iuzwe vizuri badala sasa watu kufichwafichwa na kushikwa akikutwa anakunywa mnazi. Sasa sisi tunashangaa, mtu amegema tembo lake yuanywa pale kando maanake ndio mila yake anashikwa. Mwingine anaenda bar anakunywa busaa mpaka wanakuwa vipofu na hawashikwi. Tunaomba mnazi uhalalishwe ukiuzwa kwa sababu utatufaa hata kupeleka watoto wetu mashuleni.

Ninakuja sasa kwa haki za akina mama. Haki za akina mama ninashukuru sana kwamba kina mama tumeambiwa tutoe maoni yetu na sisi tutatoa. Tunataka haki za akina mama ziangaliwe katika sehemu zote. Kuhusu mambo ya uridhi tuangaliwe katika

mambo yote ya kugawanya mali tuangaliwe kwa sababu sisi tuko pamoja na mwanamume yule ambaye amechuma akiwa hana chochote mpaka sasa ana kila kitu. Kwa hivyo tunasema kwamba kwa bahati mbaya mume wangu akifa na watoto wangu ni wakubwa nitakaa na watoto wangu lakini still ile mali ni yangu na wala si ya watoto wangu. Na kama labda nitakuwa bado ni mtoto na bwanangu amekufa nimeenda kuolewa mahali ingine, nigawanyiwe uridhi sawa ule ambao mume wangu tulikuwa naye. Kama labda nitakuwa na mtoto pale nimeacha watoto then, nipate ¼% ya ule uridhi ambao bwanangu aliniachia.

Tukasema pia kwamba katika hali hizo za kuridhi kuna vitu vingine kina mama hata hatuangaliwi kabisa, kama mambo ya mashamba, mambo ya title deeds. Tunasema ya kwamba kina mama wa Kwale au kina mama wa kenya nzima kwamba katika mashamba title deed isiandikwe tu jina la bwana peke yake iandikwe jina la Bakari Said na Halima Chivumbe title deed yao. Halafu tunakuja katika vitu vingine hizi ambazo tunaziita domestic violence ambazo zimekuwa zikiendelea katika nyumba zetu. Tunasema kwamba mwanamke si mtu wa kutumiwa vibaya, wala mwanamke si mtu wa kuonewa bali mwanamke ni mtu kama wewe ulivyo ndani ya nyumba. Kwa hivyo kama baba atapiga mama kila siku sheria ipangwe kwamba baba yule kama kila siku amepigwa miaka mitano na kuendelea mbele. Tunakuja mahali ambapo saa ingine kina mama sisi tunafanywa vibaya hata na waume zetu. Bwanako anaenda ana-rape mtoto wako nyumbani mwako. Ni mwanawe hata yeye ni mwanao lakini anaenda anamgeukia. Mzee kama yule sisi kina mama tulikaa tukasema afungwe maisha, kwa sababu huyo anakuwa si baba tena bali ni jibaba, na kama ni jibaba basi lifungwe kabisa kabisa. Na ikiwezekana pia huyo hana maana akatwe halafu aachwe hivyo hivyo.

Tumesema sasa katika hali ya mamlaka katika Bunge. Sisi wanawake tupatiwe kama viti arobaini au themanini kule Bungeni ambapo hivyo vitakuwa ni vya akina mama tu na sisi wenyewe tutavipigania, halafu tukija katika hizi councils zetu tuwekewe viti ishirini hivyo viti ambavyo vitakuwa ni vyetu sisi akina mama.

Mwisho namaliza kidogo bwana kamishina ni kwamba, ni kweli waBunge tuliwachagua kwa nia safi lakini mishahara yao ni mikubwa mno. Na tunasema hii mishahara yao ipunguzwe kwa sababu sasa tunaambiwa wanapata laki sita na kuendelea, wakati mwananchi wa kawaida anapata shillingi elfu nne. Haki hiyo iko wapi. Asante.

**Com. Swazuri:** Councillor Mandano.

**Cllr. Mandano:** Kwa jina naitwa Mandano kutoka Waa. Baada ya kusikia Tumeinakuja kuchukua maoni, nilikutanisha watu wangu wa Waa na tukaandika na tukachukua maoni na mapendekezo kutoka Waa location kwa hivyo nitakayoitoa hapa ni mapendekezo na maoni ya watu wa Waa location kwa sababu tulikuwa na mikutano tofauti tofauti na tukawa na ile referendum ambayo tulipitisha na kudhibitisha kuwa ni maoni ya watu wa Waa wote.

Kwanza, watu wa Waa tulizungumzia wananchi (citizenship). Kwa sasa nchi hii inaruhusu uraia mara mbili, dual citizenship. Mtu anaweza kuwa mkenya na vile vile kuwa mwingereza. Na tuliangalia kwa mfano kama baba ni mzungu na mama ni mwafrika

kuna uwezekano kuwa mwananchi yule akawa ni mwananchi wa nchi mbili. Tulisema, mambo hayo yaondolewe, ili mtu akizaliwa aamue kama anataka kuwa mkenya awe mkenya au anataka kuwa nchi ingine.

Halafu tukazungumzia mambo ya usalama ambayo ni defence national security, tukasema Rais asiwe peke yake katika uamuzi wa mambo kama hayo. Lazima kuwe na speaker wa senate ambaye atakuwa anasaidia Rais katika mambo hayo, kutakuw na vile vile waziri ambaye anahusiana na usalama na vile vile mkuu wa majeshi pamoja na mkuu wa sheria. Tukazungumzia habari ya vyama vya siasa. Sasa vyama vya siasa vimekuwa vingi sana zaidi ya vyama arobaini. Tulizungumza tukasema kwamba na tukakubaliana kwamba vyama viendelee kusajiliwa lakini visipate ruzuku yoyote kutoka kwa serikali na vyama hivi vitaisha vyenyewe automatically.

Vitapunguzwa halafu vile vinaonekana ni vya haki, vitaendelea na shughuli zao. Halafu tukazungumza mfumo wa serikali tunayoitaka na tukakubaliana tunataka mfumo wa serikali ya Majimbo ambayo itakuwa inaangalia watu wake. Katika mfumo wa serikali ya Majimbo tulizungumzia tunataka maBunge mawili, ile lower house na upper house. Katika lower house ile original house ambayo itakuwa maamuzi yatafanywa hapa na kama kuna umuhimu, ya upper house itakuwa inashughulika na mambo ya nchi nzima yote lakini regions zipewe powers zake. Halafu tulisema Rais asiwe ni mBunge wa sehemu yoyote. Awe ni president tu wa nchi, kwa sababu system ya sasa iliyoko Rais anakuwa ni mBunge inaonekana inalalia kwake zaidi. Hizi system zipo hata Tanzania, Rais sio mBunge wa sehemu yoyote, kwa hivyo hata sisi tulipendekeza kuwa katika serikali ijayo Rais asiwe mBunge wa sehemu yoyote. Apiganie kiti cha uRais peke yake, halafu atangaze mapema kuwa mimi nasimamia uRais lakini makamu wangu atakuwa mtu fulani, tujue mapema.

Halafu, watu wa Waa tulisema katika zile powers ambazo tutakuwa nazo katika regions kuna power fulani tutazipeleka katika central government, kwa mfano usalama, na foreign affairs mambo ya nje kwa sababu usalama tuliona tukichukua katika Majimbo, Majimbo mengine yanaweza kuchukua advantage wakazusha vita ambavyo vitaleta balaa.

Halafu watu wa Waa, tulisema Majimbo ambayo tumetaka sisi ni yale yaliyopo sasa. Coast province, central province, Nyanza province, Nairobi, whatever na hayo Majimbo yote yaende vile vile yalivyo. Halafu tukasema ma-mayor wote na ma-chairman katika mabaraza wachaguliwe kwa mfano chairman wa Kwale county council achaguliwe na watu wa Kwale wote, sio madiwani kama vile tunavyofanya hapa lakini wananchi wote wa Kwale wahusike katika kuchagua madiwani kama vile tunavyofanya hapa lakini wananchi wote wa Kwale wahusike katika kuchagua ma-mayor au ma-chairmen wao.

Halafu tukasema, kwa sasa nafikiri umri wa kupiga kura ni miaka ishirini na moja lakini tukasema upunguzwe mtu kuanzia miaka kumi na nane awe na uwezo wa kupiga kura. Watu wa Waa tulipitisha kuwa mtu yeyote anayepigania kiti cha uBunge awe na elimu ya shahada ya chuo kikuu kinachotambulika. Kwa hivyo waBunge wote tunataka wawe na elimu ya juu ya chuo kikuu kinachotambulika, halafu ma-mayor au madiwani wawe na elimu ya form four na kuendelea.

Halafu mBunge au diwani atakayeonekana kuwa hafanyi kazi vizuri atapewa baada ya kuchaguliwa maanake tulipendekeza kipindi kile kile cha miaka mitano, baada ya miaka miwili mBunge yule wapigaji kura wale ambao walimchagua wakifikia theluthi mbili 2/3 councillor yule au mBunge yule akatolewa na kura ya wale watu waliopiga kura kama hafanyi kazi sawasawa. Yaani 2/3 ya wale watu waliomchagua wakisema hawana imani naye basi hiyo inakuwa nullified halafu wanachagua mtu mwingine.

Tunasema baada ya kuchaguliwa diwani au mBunge, theluthi mbili ya wale ambao waliomchagua, 2/3 of the voters, wapewe uwezo wa kuweza kumwondoa kama hafanyi kazi sawasawa kwa mfano anaweza kuchaguliwa mtu na akawa mgonjwa hafanyi kazi. Anaweza kuchaguliwa na akawa labda haonani na watu wake kama vile wenzangu walivyotangulia kusema. Tunaomba kuwe na kifungu ambacho kinaweza kuruhusu wapigaji kura kumwondoa mtu yule. Hayo ndio mojawapo ya hilo.

Halafu tukazugumzia upande wa judiciary, ambapo tunaomba waislamu tunaomba wapewe uwezo wa kuchagua chief Kadhi sio kama vile system inavyoendelea sasa. System ya sasa ni Rais anachagua mtu lakini tunaomba huyu Kadhi waislamu wenyewe wapewe mamlaka ya kuweza kupata mtu na tumependekeza hapa umri wa chief Kadhi uwe kama miaka arobaini na isizidi miaka sitini na tano.

Halafu, tumependekeza pia hapa huyu chief kwanza awe msomi, awe na shahada katika mambo ya sheria na vile vile awe na elimu pia katika mambo ya kidini kwa sababu ziko pia shahada vile vile za dini ya Kiislamu. Kwa hivyo hizo zitamsaidia sana. pia ikiwezekana awe ni wakili katika mahakama makuu. Halafu awe yeye ana popularity, awe anaweza ku-mobilize waislamu, yaani awe ana ule uwezo wa kuwa anasikilizwa na waislamu wote.

Halafu hizi koti zetu za sasa, inaonekana na maamuzi ya mwisho kabisa ikifika high court uamuzi hata sio waislamu. Kwa hivyo sisi waislamu tunapendekeza kwamba huyu chief Kadhi kwa sababu ya hizo shahada nilizozitaja hapa juu awe anaweza kukaa katika mahakama makuu kwa sababu kesi ndogo ndogo za Kiislamu zinaanza katika vijiji, baadaye zinakuja Kwale, zinakwenda Mombasa kwa Kadhi, baada ya hapo zikienda kwenye koti mahakama kuu nafikiri wale majaji na magistrate wa huko wanafanya reference tena huko nyuma ambapo hao hawawezi kutoa uamuzi wanauliza tena huku nyuma ilikuwaje kwa sababu tunataka kama ni mwislamu uhukumiwe Kiislamu vile vile. Tusihukumiwe kulingana na sheria za nchi. Tuhukumiwe kwa sheria za nchi lakini kikiwa ni kifungu cha Kiislamu kiko pale kinasema huyu ni mwislamu kwa hiyo hukumu yake inamfaa aina hii.Haya, asante sana kwa nafasi uliyonipa bwana kamishina.

**Com. Swazuri:**

Asante bwana mwenyekiti wa Tumeyetu. Mimi nitakuwa very brief na kuanza kwangu mapendekezo yangu ningeanza habari ya

ardhi kwani hakuna mtu yeyote ambaye yuaishi kwa amani kama hana ardhi. Kila mtu ni lazima awe na ardhi. Hakuna kitu ambacho ni very sensitive katika ulimwengu huu zaidi ya ardhi. Kwa hivyo ni lazima, twaomba Katiba yetu iwe itawekea imani ya juu sana mambo ya ardhi kwani nikitoa mfano, ni juzi tu kulipokuwa na fujo huko Kosovo na haikuwa ni sababu nyingine zaidi ya mambo ya ardhi.

Kwa hivyo kwanza ningesema ya kwamba katika mdigo ama mduruma, watu wa kwale district waamini sana mambo kitu kama kinachoitwa kaya. Kaya zetu zimenyakuliwa na wenye ardhi na twataka zirudishwe katika jina lile lile la kaya bila kuachwa hata sehemu moja. Public utility land. Kwa land grabbing iliyokuwako zimechukuliwa ardhi za mahospitali, ardhi za mashule, ardhi open spaces, public areas kwa manufaa ya watu binafsi.

Katiba yetu twataka isisitize ardhi hizi zirudie hali ile ile, zajulikaniwa na tuko tayari kuzitambua. Nikitaja hapo, plot allocation committee ndio ambayo imeharibu kabisa mambo haya ni kwa sababu plot allocation committee is composed of people ambao hawakutoka katika district hiyo. Ningetaka members wa plot allocation committee wawe indigenous people wa district hiyo, and departmental heads wawe only advisors lakini members wawe ni indigenous people ndio ambao wanajua ardhi ni nini katika district hiyo. Habari ya serikali ningesema ya kwamba serikali yangu wenzangu washasema juu ya regional government, hakuna choice nyingine zaidi, twataka Majimbo. Jimbo letu twalijua ni la pwani, twajua limeanza wapi na limeishia wapi and we are firm.

Kwa hivyo ibaki jimbo letu liwe la pwani. Nikigusia kwamba serikali, local authorities, ningetaka kusema kidogo juu ya local authorities kabla ya the year 1970 zilikuwa very good organizations ambazo zatoa services kwa watu wote lakini from 1970 baada ya powers hizo kuchukuliwa na kupelekwa Central Governmentzimekufa, hazijulikaniwi ziko ama haziko. Na problems ni ndogo sana. kwanza ningesema kwamba kabla ya wakati huo clerks walikuwa wakiwa selected from the indigenous, qualified people lakini hizi sasa imekuja public service Commission na public service Commission imekuwa set aside watu wawe handpicked. Ni ndugu yangu mchukue akaue baraza fulani. This is what I was saying. Maana mtu hawezi kuwa amekuwa clerk amefail alikotoka lakini achukuliwe akawe clerk katika ofisi nyingine. That is the thing na twataka serikali iingilie jambo hili kwa kikamilifu.

Sasa hizi ambazo ningetaka zirudishwe ni kama public health zilikuwa zajulikana vizuri wakati zilipokuwa katika local authorities wakati huo, primary education, water services, veterinary services, agricultural services na mengine machache. Kwa hivyo ningetaka kwamba serikali yetu ama Katiba yetu mambo haya yarudishwe pale pale yalipokuwa mwanzo. Nikija kwa habari ya tourism, ningesema kwamba habari ya tourism isije ikawa ya benefit Central Governmentinstead of the region, instead of the district. Ningependekeza kwamba 80% of the region of tourism ibaki katika district ile ile and 60% ibaki kwa district. Only 20% iende kwa central government.

Bwana mwenyekiti na members ningependekeza kwamba habari ya nominated councilors na nominated MPs. System irudi ile

ya kwanza, Katiba yetu ilikuwa imesema kwanza mtu anayecontest na akifeli hawezi kuchaguliwa kuwa mBunge lakini hivi sasa mwenzangu ametangulia kusema ni wale wale waliofeli ndio ambao wachaguliwa tena wapewa hata uaziri. This is shame infact we have gone outside the current constitution. kwa hivyo twataka mambo haya yarudi na yawekwe kwa imara zaidi. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana, nenda pale na uandike jina lako. Kassim Abdallah

**Mr. Kassim Abdallah Zani:** Salaam Aleikum. Asante bwana Commissioner, kwa jina ni Kassim Abdallah Zani, Maoni yangu kwanza nagusa katika sehemu ya chief Kadhi. Kulingana na Katiba ya kenya chief Kadhi huwa anachaguliwa na Rais. Hatutaki. Mtu yeyote aliyefanya kuchaguliwa na mtawala huwa hawezi kuwa na mamlaka ya kuendesha dini na kufuata amri zake vile ilivyo. Kwa hivyo chief Kadhi tutachagua wenyewe. Kiwango cha elimu kwa chief Kadhi. Tutachagua chief Kadhi ambaye yuko na shahada ya wanasheria wa dini ya Kiislamu halafu awe na shahada ya wanasheria ile inayoendesha nchi ambayo tunaita circular law, ili aweze kumiliki kesi zote.

Mamlaka- chief Kadhi pamoja na maKadhi wengine wawe wanapewa mamlaka ya kuendesha kesi zote. Kwanza wapewe ofisi kuu, yaani koti kuu high court kama vile ilivyo katika serikali ya kenya kisha wapewe koti ya rufani. Iwapo high court imeshindwa, koti ya rufani ifanye kazi ya Kiislamu. Kisha kuwe na law courts. Wale maKadhi wengine katika district zile koti zao ziwe zinafanya kazi sawa na vile majaji wa kiserikali.

Matumizi ya kitabu cha Korani- Mwenyezi Mungu katika haya yake moja anasema (spoke in Arabic). Hakishiki kitabu hiki cha Kiislamu ila kwa mtu aliyetohara. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba vitabu vitakatifu vya Korani vinawekwa ndani ya makoti. Anayeapishwa ni mwislamu, mwenye kuapisha ni wanjiku, alivyolala hajulikani, tohara yake haieleweki, labda amelala kimakosa vibaya, hata kuoga mwili hajui, anamwapisha mwislamu na kitabu cha Mwenyezi Mungu. Naomba, maombi yangu vitabu vitakatifu vya Korani viondolewe makotini, serikali itafute njia ya kuapishana si kutumia vitabu vyetu vya Korani.

Mwezi mtukufu wa Ramadhani- limetokea tatizo kubwa kuwa waislamu wamefanywa wanafunga kiholela. Wale wanafunga, wale wanafungua, wale wanasali, wale wengine bado kwa sababu ya chief Kadhi hana mamlaka. Mwezi umetoka anaambiwa nyamaza, tangaza baada ya siku tatu kwa sababu maskini anaondoka kumwaga unga wake ananyamaza. Ndio maana unakuta kuna vumbi ambalo halieleweki imeleta mchafuko katika uislamu. Ibada zinaswaliwa mbalimbali. Kwa hivyo mwezi wa ramadhani uachiwe mamlaka yake kwa chief Kadhi. Ukitoka atangaze kama haujatoka asitangaze. Sio kuamrishwa. Fanya hivi au la. haya, hatutaki sisi waislamu.

Siku kuu ni jambo la kushangaza kuwa siku kuu zote za wakristo zinatambuliwa na serikali isipokuwa siku kuu ya waislamu peke yao. Mwezi unatoka tunapewa siku moja, wengine wanaambiwa nendeni mkasali. (spoke in Arabic) hili ni jambo la maudhi kisha jambo la dhuluma. Siku kuu za waislamu zitambuliwe. Kutoka siku kuu ya mwezi wa Ramadhani unapotoka mpaka idd kubwa. Siku kuu ndogo siku tatu, siku kuu kubwa siku tatu ziwe siku sita na zitambuliwe serikali nzima. Zikiwa siku

kuu zetu watu wetu waende nyumbani. Wakristo mpaka waislamu wapumzike.

Mavazi- hizi ni hukumu za Kiislamu ninazotoa mimi. Sisi huku Pwaninamba kubwa ni waislamu. Tunajua mavazi yetu. Kama ni urongo angalieni walivyokaa watu. Lakini kuna wageni wanaokuja tunawaita watalii, wazungu kutoka kwao. Wanakuja katika nchi yetu ambayo ina heshima kubwa, wanavaa visuruali, mashini ziko nje, tunaangalia sisi na watoto wetu na wamama zetu, jambo la kusikitisha. Mzungu akiingia hapa apewe amri ya kuvaa nguo za heshima la tutamfundisha adabu za kuvaa nguo ama asije abakie kwao.

Utawala- kutoka mwaka elfu moja miaka sitini na tatu tulipata uhuru. Tulikuta utawala hapa umewekwa na mwingereza ambao mimi mwenyewe nilikuwa ulaya 1975 sikuona. Hapa kwetu bado ingawaje mama ameingia pole hii ni maombi yangu. Hapa kwetu bado tuna mambo ya PC, mambo ya DC, mambo ya DO, mambo ambayo kwamba mzungu ameyaleta na huko ulaya hakuna nilikuwako sikuona PC, sikuona DO, sikuona DC. Aliyaleta hapa ili mwafrika awe chini, mzungu mume aitwe bwana, mzungu mke aitwe memsahp lakini huu utawala huu hauko. Hata Tanzania hakuna, hata Uganda hakuna, kwa nini kenya peke yake ndio kuna ma-DC na ma-PC na ma-DO. Tunataka hapa kwetu waondolewe, wapewe kazi nyingine kubwa kubwa, tubaki na chifu ahukumu kesi za mallu peke yake.

Rais- hatutaki Rais awe above the law. Haya ni matatizo. Inaweza siku moja akaamka aseme sitaki dini ya waislamu wala wakristo, watu wote wawe devil worshippers. Lazima tufuate maanake Rais amesema. Kwa hivyo Rais wa kuwa above the law hatumtaki. Tunataka Rais ambaye kwamba atachukua maoni ya wananchi. asikize, aambiwe kwamba hili na hili ndilo hili halifai na awe anapata amri. Sio akisema hii ni basi. Huu ni utumwa.

Mazingara- ni jambo moja la kutatiza kuwa siku hizi, wanyama wana dhamani kuliko mwanadamu. Mwenyezi Mungu aliwaleta wanyama kuwa ni utoezi kwetu. Hakuwaleta waje wawe matingi. Leo hii ni serikali inaweka mpaka, wanyama wanatembea huko, ndovu anatoka anaingia mashambani kwetu, wanakula mimea yote, wanaua watu, Serikali inafurahikia. Malipo hakuna. Hebu toka wewe ukaue ndovu mmoja. Serikali itaweka matanga ya siku tatu ndovu ameuawa lakini hawahuzuniki wakati mwanadamu ameuawa. Haya ni mambo ambayo ni kinyume cha Mwenyezi Mungu na labda atakasirika aweke kiama. Kwa hivyo mazingara haya yatupiliwe mbali. Ikiwa kutawekwa sehemu ya wanyama wakae na wakae. Wakipita wakija kwetu ni kitoweo, hakuna kesi.

Uchumi- wenzangu wamezungumza kwa hivyo sina haja ya kurudia mshaelezwa vile uchumi inatakikana kuwa katika sehemu yetu, kwa hivyo hiyo inatosha. Elimu- elimu hii ninazungumzia mimi nikuwa ni kuwa wenzetu wakristo wanapohitimu, wanapewa nafasi ya kuandikwa ni serikali. Wafundishe C.R.E ndani ya mashule lakini waalimu wa Kiislamu hata wanapohitimu hawawezi kuandikwa na serikali wakafundisha I.R.E. kwa nini? Kwa hivyo elimu kuwe na kipengele kiwekwe katika hii Katiba mpya ya kwamba waalimu waislamu waandikwe kwenye mashule, waweze kufundisha elimu ya kizungu na dini ya Kiislamu, kwa sababu huko inapoenda ni hatari. Elimu ya Kiislamu huenda ikapotea. Watoto wanaingia shule akifika anaambiwa funga macho bwana

alisema mtakatifu, alikuja Ijumaa, atatoka jumamosi lakini hawezi kuambiwa MTumemohammed alisema nini. Haambiwi, haya hatuyataki.

Majimbo yamemalizwa, tunataka Rais wetu. Ma-Rais wagawanywe kila upande kuna Rais wake kuna Rais wake halafu watakutana Nairobi watakutana Nairobi, watafanya mashauri nchi yaendelea namna gani. Asanteni.

**Com. Swazuri:** asante sana. tumpate Agnes Mnyapara.

**Mrs. Mnyapara:** Mimi kwa majina naitwa Agnes Mnyapara na ni mkaaji hapa wa Kwale town. Namba moja, tunasema ya kwamba hatutaki dini yoyote I-advocate divorce. Iwe wakristo, iwe waislamu kwa sababu watoto wengi ndio wanaumia tumekaa tukiangalia twaona watoto wengi wanaachwa kwa sababu ya divorce kuwa nyingi na wanarandaranda huko mitaani bila namna yoyote kwa sababu hakuna mama mwingine anaweza kulea mtoto kama mzazi wake. Kwa hivyo ziwe minimal. Ya pili, dini hatutaki iwe associated na politics. Ya tatu, chifu anatakiwa awe mtu ambaye amesoma at least mpaka form four awe na D and above. Kenya, mkenya yeyote anatakiwa awe na mali katika republic ya kenya hata kama ni wapi, provided amelipa pesa zake kununua ile mali na pesa zake. Kama ni ardhi apewe title deed kwa sababu amenunua ile ardhi, hakupewa na hakuchukua kwa njia ambayo isiyo halali.

La tano, tunasema ya kwamba currency hii kubadilisha currency ya kenya mara kwa mara iwachwe, I-remain currency moja tu ambao ndio wanakenya wote wanatumia. Yaani currency ile picha yaani saa zote president huyu akija, unaona currency inabadilishwa ili kulingana na president ambaye amekuja. Ya sita tunataka kuwa tuendelee kuwa na freedom of worship isipokuwa kuna dini zingine kama hizi zina-advocate devil worshipping.

Serikali tunaiuliza dini kama hizo zisiwekwe kwa sababu kuna dini zina-encourage watoto wetu kuvuta bhangi na kula miraa, kitu ambao hazina mwelekeo wowote katika nchi yetu. Tunasema hizi unaona kama mtu kenya, tunataka judiciary itofautishwe iwe peke yake itengwe kwa sababu inaweza kuwa na judge. Mtu amefanya makosa lakini akiwa amefanya makosa lakini akiwa amefanya makosa kwa sababu kuna Central Governmentpale anaambiwa pitisha hii kesi namna hii. Hiyo tunataka judiciary iwe peke yake.

Ya nane, tunataka hii ambayo imezungumzwa yaani tunataka mali ya bibi na bwana iwe ni yao peke yao kwa maana tunaona ya kwamba mtu akifa unaona hii ni loss. Watoto wa shangazi na watu wengine na ndugu za bwana na mama za bwana wanakuja kupokonya yale mali. Tunataka mali iwe ni ya bibi na bwana waamue ni nani watakaompatia. Tunataka ile elimu ya 8-4-4 ile ilikuwako mpaka form six, iwe ndio hiyo irudi hiyo. Turudishe ile elimu ya zamani.

Tunasema mtu yeyote katika Kenyan government au kwa serikali ya kenya, amechukua mali ya raia kwa njia ambayo si ya ki-halali, yaani corruption, ashtakiwe na mali irudishwe ile amechukua kwa njia ambayo sio halali kwa sababu ndio nchi yetu

imekuwa na shida zile tuko nazo kwa sasa kwa sababu mali zetu zina watu wamechukua pesa, wakajitajirisha, sisi tunakaa maskini na watu wamechukua mali.

Na kile kingine tunasema ni tukikuwa mabibi tunakataa. Yaani bwana ameoa bibi hapa, amemfanya ni kama ni mbuzi yake kupika kila wakati, hiyo tunakataa, yaani ashtakiwe, akimpiga mwanamke. Kitu kingine nitazungumzia na ndio ya mwisho ingawa sikumaliza karatasi nitapeana donors kenya tunataka wakija wa-deal na associations bila pesa kupelekwa kwa government kwa sababu zikienda huko kama ni kwa jua kali fulani, ama association fulani haipati zile pesa, zinaenda njia zingine kwa hivyo tunataka kama ni kikundi fulani kipewe hizo pesa kifanyie kazi hicho kikundi.

**Com. Swazuri:** Asante sana mama. Andika jina lako pale na utuachie hiyo memorandum hapo na atafuatiwa na councilor Mwajuma ajiweke tayari.

**Mr. Juma Ali:** Mimi kwa majina ninaitwa Juma Ali Mwachiama, councilor wa kutoka Ziwani ward, Kwale town council. Sisi kama watu wa Pwanitulivyo, mengi yameshasemwa kwamba tunataka Majimbo kwa hivyo swala hilo siwezi kulirudia tena lakini naongezea tu kwamba tunataka Majimbo kivipi. Sisi watu wa Pwanihapa kutoka tupate uhuru naona tumetengwa sana. kuna rasilimali zetu kama minazi, korosho, na hali kadhalika. Hii imerudishwa yaani iko nyuma hata haitajwi lakini kwa sehemu zingine kama kahawa, chai, hata kuna mabodi yamekuwa set-up, hili ni jambo la kuhuzunisha.

Kwa nini hizi miti miwili korosho na mnazi usifanyiwe board nayo ikafanyiwa utafiti na ikawa inatambuliwa na serikali tukapata mazao yetu. Mapato yetu kwa sababu mtu wa Pwani yeye ametegemea sana mnazi, ametegemea sana korosho na huu mnazi ni mti ambao hakuna chochote unaweza kutupa. Mnazi tunajengea nyumba, mnazi tunapata pombe, tunapata kila kitu kamba, kila kitu, mafuta lakini hautambuliki. Tunaomba katika Katiba hii tunaiandika saa hii, hii miti miwili nayo itambuliwe. Iwe inafanyiwa kama vile kahawa na chai.

Pili, tunataka Majimbo kivipi? Tunataka Majimbo ambilikanayo na sisi tuwe sawa na wale wenzetu wa bara. Tukiangalia kielimu, kiafya, mambo yote yako huko bara. National schools ziko huko bara, public universities ziko huko bara, hapa Pwanihakuna chochote. Jingine, tunataka kimajimbo vipi? Tunataka kimajimbo kwa sababu za ardhi zetu. Ardhi zilinyakuliwa mpaka sasa mtu wa Pwani amekuwa ni squatter na hii ni jambo la kuhuzunisha kabisa. Basi katika Katiba hii, mimi ninaomba na nataka iandikwe kwamba wale walionyang'anywa ama ardhi zao zilizonyakuliwa zirudishwe, warudishiwe wenyewe na zile ardhi za serikali ambilikanazo zimechukuliwa, zirudishwe, zigawanywe kwa wananchi ambilikanao hawana mashamba.

Kuhusu mambo ya mapato ya pwani, mengi yamesemwa lakini mimi naongeza. Katika hapa Pwanisisi tuna mapato mengi. Tuna mapato ya utalii, tuna mapato ya port yetu hapa ndio ambilikanao ni kama mlango wa kenya. Mapato haya yote katika hizi kodi na mapato mengineyo, mimi nasema 75% iwe inamilikiwa na jimbo. 25% iwe inaenda kwa central government, kwa sababu tukiangalia barabara zetu zimewachwa nyuma, mambo ya hospitali yameachwa nyuma, kila kitu, hii 75% iwe inagharamia haya

mambo yetu ya development ya barabara, mahospitali yetu, tuwe mwananchi wa kawaida akienda kule hospitali asiambiwe eti kuna cost sharing. No! hiyo cost sharing iwe haiko.

Mambo ya elimu- kuanzia nursery mpaka std. 8 iwe completely bure. Kuwe kuna vitabu vya kuandika, vitabu vya kusoma, na zile ambilikanazo ni kama pencils, pens vyovyote ambilikanacho yule mwanafunzi anahitajika awe ni bure kwa sababu umekuwa ni mzigo wa sisi wazazi. Kuna watoto wengi sana hivi ninavyosema wako nje kwa sababu juu ya kitu kidogo ya vitabu hana, mzazi hawezi kununua. Kwa hayo machache sitasema mengi sana lakini ninarudi hapo kwa upande wetu kuna hizi factories zetu kama kenya sugar factory, ilikufa zamani, lakini jambo la kusikitisha, hapa pwani, vitu kama vile vikifa serikali haiangalii.

Kuna mambo mengi kule kwa wenzetu, sijui ni sony sugar, sijui ni chemilil, zikifa serikali inatia mkono inaendelea. Kwa nini sisi watu wa Pwanituwe ni kama tunabaguliwa, tunataka vitu kama hivi. Hivi nisemavyo, serikali isikie kwamba watu wa Pwaniwanataka mtambo wao wa korosho, wanataka mtambo wao wa sukari, iwe inarekebishwa na sisi tujione kwamba yes! Tuko huru. Kwa hayo machache ninasema ni asante sana.

**Com. Baraza:** Two clarifications. You understand English. Kiswahili I don’t understand, I don’t speak it well. Umesema income ya pwani, 75% ipatiwe kwa jimbo lenu, 25% iende kwa Central Governmentna pia unasema elimu iwe free. Sasa hii itagharamiwa na nani, hiyo elimu.

**Mr. Juma:** Hii elimu tumesema itagharamiwa na hii 75% kwa sababu mapato yote tutagawanyia serikali 25% sasa sisi tumebaki na sanduku letu la pesa.

**Com. Baraza:** Okey, sawa. Swali lingine, umesema industry na vitu vingine vya Pwanivikifa vinakufa tu, hakuna mtu ana…. Serikali haihusiki na huko bara, sukari nini. Mimi huona hao waBunge wa kule wanafanya kazi sana. wao ndio wanatetea nyinyi waBunge wenu huwa mnahusikana namna gani kwa hii mambo ya representation kwa sababu mimi nimeona waBunge wetu huko kwa sukari, wanapigana. Nimeona huko watu wa chai na majani ni waBunge, sio tu wa serikali. Niambie, mmekuwa na waBunge na wamewafanyia nini?

**Mr. Juma:** Bi kamishina hebu kidogo, si kwamba waBunge wetu hawasemi. WaBunge wetu wanasema mpaka machozi yanatoka ya damu lakini nasikitika hawasikilizwi. Wanasema tu kama hivi hata haya ninayosema sijui yatapelekwa ama namna gani lakini naamini yatapelekwa na waBunge wetu ndio vile vile, wanalia lakini hakuna chochote ambilikanacho kinashughulikiwa pwani. Liko swali lingine ama niongeze zaidi.

**Com. Swazuri:** Baada ya councilor mwajuma tuna Rashid Mwatsuma.

**Mr. Rashid:** Asante bwana kamishina, jina langu kamilifu naitwa Rashid Abdallah Mwatsuma kutoka location ya Gombeni.

Kwanza langu mimi nitazungumzia kuhusu mambo ya ardhi. Ardhi katika huu mkoa wa pwani. Kutoka zamani ilipoanza kutawaliwa na mreno, akaja mwarabu, akaja mwingereza kisha tukanyakua uhuru. Ardhi hizi zilikuwa zikimilikiwa kwa njia ya vile walivyojichukulia wale watawala wa kiarabu na mpaka sasa ukiangalia kutoka Vanga mpaka Lamu ardhi hizo wenyeji ambao halisi ni wazaliwa wa hapa, wadigo na waduruma, ardhi hizo hawanazo hata kidogo bali wao ni watumishi katika ardhi hizo.

Pendekezo langu mimi ninalolitoa ni kwamba kulingana na Katiba mpya ambayo itatolewa,vile walivyozipata ardhi zile kulingana na serikali ile ya ya waarabu wakati ule, sheria irejeshe upya kwamba ardhi hizo zirudishwe serikalini na ziweze kugawiwa wenyeji kikamilifu na kupata title deed zao ili kuwe na kwamba kila mmoja ana haki kuliko yule aliyetoka kutoka uarabuni ama uingereza ama mahali pengine aje awe na haki kuliko mzaliwa wa hapa awe hana haki.

Jambo langu la pili, ni ardhi hizi za serikali ambazo ni state land. Wakati tuliponyakua uhuru kulikuwa na mtindo kana kwamba kunachukuliwa ardhi fulani za serikali zigawiwe wananchi wale ambao wanaitwa squatters lakini hawa kufikiriwa wale squatters halisi ambao walikuwa wakiishi ndani ya yale mashamba Commissioner of lands ndiye alikuwa akichukua uwezo wa kuona kwamba ardhi hizo ikiwa kuna jamaa zake ama kina nani wameomba hizo ardhi basi wawe wanapatiwa / letters wanaenda kule tayari shamba ni lake lakini yule mwananchi wa kawaida ambaye ni mzaliwa wa pale amelima pale, ana mimea ya kudumu pale, wakati ule ule yeye hastahili pale ataambiwa hapa ni pangu ondoka. Kwa hivyo jambo hilo lifutiliwe mbali, ardhi zile kwanza zipawe wale ni squatters pale ili wajisikie kwamba wana haki kama mkenya mwingine.

Jambo jingine, ni mambo ya utawala. Kwangu mimi nasema ni haki kabisa wakati huu tuwe na serikali ya Majimbo lakini Rais aweko na kuwe na prime minister wagawiwe madaraka ili kuwe na kwamba kila mmoja akatekeleza kazi zake vile ambavyo atakuwa amepangiwa kulingana na sheria ya nchi yetu kwa sababu hivi sasa ukiangalia kweli kila kitu kiko kwa Rais since he is above the law lakini ukichunguza tena hapo hapo, kibinadamu kuna wengi ambao wamepewa nafasi na vyeo kupitia kwa serikali kuu na Rais amesema okey, wewe shika hii, shika madaraka haya, wale wale wanatupanisha madaraka yao akijisikia pengine Rais ni mjomba wake ama ni kakake, sasa utaona mali nyingi zinaporwa na mtu akipelekwa mahakamani hakuna kesi itakayomshinda mtu yule kuona kwamba amepatikana na hatia aweze kupelekwa gerezani na mali ile irejeshwe kwa serikali ili kuona kwanza umma utaweza kufaidika. Kwa hivyo Rais aweko lakini asiwe above the law.

Ukirudi upande wa polisi, polisi ukweli hivi sasa kuna haja ya mabadiliko makubwa kuhusu sheria zinazofuatiliwa na polisi. Sisi wenyewe Commissioners ambao mmekuja hapa mmejionea wenyewe barabarani. Polisi sasa ni kuwa kila saa kumi na mbili awe barabara ahakikishe ikifika saa nne saa tano ameshatengeneza karibu elfu saba wanaondoka na pesa zile haziendi serikalini. Na gari lishtakiwe liliyo na makosa, lipelekwe mahakamani, pesa zile ziweze kupatikana kwa kuhudumu serikali lakini utakuta sasa ni mtindo wa kubagua shillingi mia mia watu wakiokota na serikali bado inataabika pesa hakuna. Mimi napendekeza kuwe na mahakama ya mobile.

Kupangwe, hakimu aje barabarani, na polisi. Pale pale gari isimamishwe kama ina makosa ishtakiwe, afainiwe pale pale maneno yamemalizika lakini hivi sasa ukiangalia mahakama ya traffic haipati magari mengi zaidi makosa ya madereva hayapatikani kwa sababu mambo yamalizwa hapo hapo. Kwa hivyo napendekeza hivyo kuwe na mahakama ya mobile.

**Com. Swazuri:** Hiyo hoja imejaribiwa mobile, lakini askari anakwambia kosa hili kuenda kotini ni shillingi elfu moja. Nipatie elfu tano tumalize hapa hapa. Sasa tutakuwa tumemaliza vipi?

**Mr. Rashid:** Okey, sawa. Tutapendekeza kwamba baada ya hicho kikao kikiwa sisi wenyewe tunakikubali ya kwamba waislamu na wakristo walioamini kabisa kwa mungu hayuko tayari kupata centi haikufanya kazi. Kutafutwe njia au mimi napendekeza kwamba kutafutwe mapadre na waislamu ili waingizwe katika hiyo serikali wakati haki hizo zinatekelezwa wawe wako pale kushuhudia kitendo kile cha haki kitakachokwa chatendeka.

**Com. Baraza:** Naulizaje, na hii nchi yetu iko na wakristo na waislamu na sisi ndio tutatoa hiyo hongo kwa polisi.

**Mr. Rashid:** Wengi wao wanaotoa hongo kwa polisi madam ambao sio wakristo wa kweli na sio waislamu wa kweli. Kwa sababu kama wangekuwa wacha Mwenyezi Mungu kwa hakika wasingethubutu hata kutoa nusu centi wangemwambia askari shtaki, nipeleke kotini, lakini wengi ni wale ambao hata kuficha, vile anavyoamka hata hashukuru Mwenyezi Mungu anashika steering tu anakwenda. Lakini waislamu wa kweli hawathubutu kufanya hivyo na wakristo pia.

La mwisho, ingawaje maneno bado yako lakini mimi nasema mambo ya elimu, wakenya wengi hivi sasa ukweli ukiwazungukia mtawakuta kwamba ni wale ambao wamekosa elimu. Kwa hivyo pendekezo langu nikuona ya kwamba wizara ya elimu itengenezwe na kuona kwamba mkenya yeyote akizaliwa awe wazazi wako hai, awe hana wazazi lakini iwe ni sheria mkenya yule aweze kupatiwa elimu na serikali, kiwango sawa na yule ambaye mzazi wake yuajimudu ama mzazi wake ni tajiri ama ni maskini ili kila mmoja aweze kufaidi gurudumu lile ambalo ni mpangilio wa serikali.

**Bishop Njoroge:** Councillor, ningetaka unajua tuliambiwa ni serikali ya Majimbo lakini hakuna mtu anayetuambia structure ya serikali vile itakuwa namna gani. Kwa sababu binadamu ni yule yule, na iwe ni jimbo watachukua ile tena. Kwa hivyo ningetaka uandike karatasi ya kuonyesha structure hiyo itakuwa namna gani ili 75% ikija hapa msiwe na serikali tena inaweka kwa mfuko. Sawa?

**Mr. Rashid:** Thankyou.

**Com. Swazuri:** Asante sana councilor. Ali Tchizondo na atafuatiwa na Ali Mwatebe. Dakika tano.

**Mr. Ali Said Tchizondo:** Salaam Aleikum warakba tulai wabarakatu. Kwa jina langu ni Ali Said Tchizondo chairman wa

chama ambacho hakijasajiliwa kenya hii na adu. Bwana Swazuri au bwana kamishina, nimepata utaka wa nafsi yangu uliponiambia ya kwamba au ulipotuambia kwamba walioandika memorandum wasisome, wapeane.

**Com. Swazuri:** Sikusema hivyo tafadhali. Nilisema unaweza kusoma na kama hutaki kusoma ukaitoa pale au ukaipitia.

**Mr. Ali Said:** Okey, hapo ni sawasawa. Nimekubali nilikuwa sijakuelewa maanake lilikuwa dukuduku langu ndio nilisema kwamba kwa nini naambiwa memorandum yangu niliyoiandika nisiisome. Lakini kumbe naambiwa naweza nikaipitia. Asante. Bwana kamishina, mengi yamesemwa na Kwale kuna wasemaji wazuri kama vilivyo lakini wasiwasi wetu au wangu ni kwamba je, katika haya mapendekezo yetu tunayoyanakili yatapitishwa, yataandikwa? Hiyo ndio shida yetu. Kwa sababu twaweza tukasema twataka serikali ya Majimbo mpaka mamake Majimbo lakini isipitishwe. Itakuwa ni vibaya kwamba sisi twataka hivi lakini kisha isitokee. Bwana Swazuri, mimi nasema Katiba hii ambayo leo tunaitayarisha, tulikuwa tuna Katiba ambayo ilitengenezwa Lancaster house 1962 na waliotangulia na wakati wa Katiba ambayo ilitupeleka mpaka leo hii. Ajabu ya kenya hii, kuanzia kiongozi aliyetangulia kutawala nchi hii kenyatta aliifanya mabadiliko ya Katiba bila kushauri Bunge bila kushauri wananchi.

Ina zaidi ya mara thelathini kubadilishwa Katiba hiyo. Leo hii twashukuru Mungu kwamba imepatikana nafasi ya wakenya kuja kutoa maoni yao. Sasa hatujui yatakuwa sasa au itakuwa ni shere. Napendekeza, yale ambayo tutayatoa yawe yatakuwa booked, yapitishwe na yakifanya hivyo ndiyo ina maana kwamba tumeweka huo wakati wetu ya kwamba ulizingatiwa.

Bishop Njoroge: Lakini mzee hakuna ile sheria ambayo inatuambia mradi huu, inasema kwamba mkishapeana maoni yenu itaandikwa na Commission na baadaye italetwa kwenu ili kwamba ikiwa kuna kitu mlisema ambayo haijawekwa, mtaweza kuweka wakati ule, pia mnajua hii itapitishwa na waBunge wote na watu watatu kutoka kila district, na watu wa makanisa na misikiti pia watakuwa katika ile conference, sasa ni wapi tena inaweza kuwa haiwezi kupitishwa.

**Mr. Ali Said:** Hili ni moja. Sisi wale ambao wako village sasa hivi ni zaidi ya watu mia sita ambao wata/ na kutakuwa kuna uwezekano katika hao waBunge na wale delegates ambao watakuwako huko ni rahisi kuwa convinced. Maoni yangu ni kwamba, twaomba Tumehii yale ambayo tumeyasema yawe ni sheria.

**Com. Swazuri:** Haiwezekani hiyo maanake ni lazima tuchukue maoni ya wananchi wote wa kenya, wewe toa pendekezo lako na yule lake.

**Mr. Ali Said:** Haya, haya bwana kamishina tumesema kwamba twataka serikali ya Majimbo na mpaka mimi nami nasema twataka serikali ya Majimbo na serikali ya Majimbo tuitakayo ni hii. Kuna aina nyingi za serikali ya Majimbo lakini tuitakayo serikali ya Majimbo ni ile ambayo itakuwa na bonge mbili. Tuwe na senate, tuwe na upper house. Na katika jimbo kutakuwa na viongozi wafuatao. Tutakuwa na governor, na huyu governor lazima achaguliwe na wananchi. na yule waziri mkuu na Rais

aliyoko kule katika central government, benefit yake au source yake ya kupata njia ya kuongoza hii serikali ni 25% ambayo ataipata kutoka kwenye original.

Serikali ya waziri mkuu huyo huko na Rais aliyoko huko atakuwa anasimamia mambo matatu katika nchi. Anasimamia mambo ya nchi za nje, anasimamia jeshi la nchi, anasimamia na pesa. Hii itakuwa ni njia ambayo itaelekeza vile ambavyo serikali ya Majimbo itaenda. Iliyobakia 75% itakuwa sasa governor na timu yake huko chini wanaangalia miradi ile ambayo imekwama na ambayo imeachwa na serikali hizi mbili, za kenyatta na mwenzake moi kufafanua na kutengeneza maendeleo.

Ukweli ni kwamba governor atakuwa ni mtu mkubwa sana katika pwani, au katika kule jimbo. Ni wao sasa ndio wanaweza kufanya mapendekezo haya na hali hii tunayoitaka leo iwe itadumu kwa sababu bila kusimamia itakuwa ni tatizo kesho vile vile. Hii ina maana kwamba serikali ambayo tunaitarajia ni kwamba itakuwa ni serikali ya watu si ya mtu kama leo hii ambayo tunakwenda nayo. Serikali ya unitary government ambayo ni ya watu wachache. Serikali ya ukoo.

Itakapokuwa governor amelinda rasilimali za nchi na uongozi bora wa nchi kwa kweli nchi hiyo, nchi nzima kwa jumla itakuwa ina sura ya kuonekana kama zile sura nyingine nchi zingine za kilimwengu. Hiyo in one. Pili, au tatu, ardhi- bwana kamishina yamesemwa mengi sana lakini pendekezo langu nasema, ardhi ndio ilikuwa ni kidonda ndugu cha ulimwengu mzima lakini ajabu ardhi ya watu wa Pwani ilichukuliwa kama zawadi ya maofisa wa serikali kuja kupewa zawadi baada ya kazi yao nzuri kuifanya huko serikalini.

Ardhi hizo zilizochukuliwa kiholela kiasi hicho hakuna njia nyingine, hakuna short cut ni kuwa revoked na zirejeshewe wenyewe. Iwe ni ya PC, iwe ilikuwa ni ya Moi, iwe ilikuwa ni ya Kenyatta, iwe revoked maanake alichukua haki ya watu bila kuwashauri wenyewe. Elimu- elimu kenya ndio mwongozo lakini watu wa Pwanikwa jumla wameachwa kwenye giza mpaka leo. Hakuna chombo chochote cha elimu ambacho kimefanya mtu wa Pwanikuonekana mpaka sasa hivi wenzangu waliokuweko hapa wamedhibitisha kwamba watu wanalemezwa kushindwa kusomeshwa watoto wao kwa sababu kila kitu kimekuwa juu. Ajabu kitabu kimoja cha std. 1 au 2 utakinunua kwa shillingi mia sita mpaka saba cha mtoto mmoja na vitabu ni kumi.

Inahitajika kama shillingi elfu sita stationery peke yake ambazo uzi-waste. Kwa hivyo ni wazi kwamba elimu ni lazima iwe bure kuanzia nursery mpaka form six, na ikiwezekana mpaka university kwa sababu resources za nchi ndizo zitasimamia hilo neno. Barabara- ni lazima ziwe safi na zihudumiwe kama zilivyo mbali na kwamba sasa hivi kuna mpango ambao unaendelea wa serikali ya unitary government kwamba kule coast area inapewa shillingi millioni tano kwa development areas lakini hizo pesa hazionekani.

Pesa kuonekana, waBunge tumewachagua, watu wa serikali wote ni conmen. Kwa hivyo barabara lazima zihudumiwe, vilivyo. Maji- bwana Swazuri maji yatoka hapa marere lakini ni ajabu mtu wa Kwale hapa analala siku tatu bila kupata maji. Maji yanapita na barabara mpaka kwa watalii huko baharini. Huyo mwananchi wa kawaida atakwenda / ya maji. Lazima maji

yawafikie wenyewe.

Bahari- bwana Swazuri au bwana kamishina, bahari ndio rasilimali ya watu wa pwani. Ajabu kutokana na hali halisi ya serikali tuliyonayo, imeangalia kwa makini kumpokonya mwananchi wa Pwaniuhai wake huu. Inamfuata na bahari mpaka inamzuilia kitu ambacho hawezi kupata baharini kupata maisha yake kila siku. Kumewekwa Marine Park, kumefanywa nini, ili kumfanya yule mwananchi wa kawaida ambaye kuenda Pwani akapata riziki yake inashindikana, haiwezekani.

Lazima tuachie fuazi, bahari tuitumie kwa wale ambao wanaweza kuitumia ili wapate maisha yao. Dini- watu wa Pwanini waislamu kama inavyosemekana, 95% ni waislamu lakini ajabu wamechanganywa akili walipoambiwa na serikali kwamba watawekewa chief Kadhi, wakaona kwamba Kadhi ni kiongozi wa serikali. La Kadhi ni Kadhi kama jaji mwingine katika nchi. Tunachotaka waislamu tunataka tupewe jukumu, tupewe nafasi ya kumchagua mufti ambaye atakuwa ni kiongozi wa waislamu kwa mambo ya Kiislamu.

Serikali ya Majimbo nishapitia hapo, wafanyi kazi, bwana Commissioner, ukweli wa mambo ni kwamba nchi hii ilikuwa bado haijatawala na sasa inaenda kujitawala. Wafanyi kazi mpaka sasa hivi, isitoshe nikilinganisha ndugu zangu waalimu wanahangaishwa na madaktari. Ni kwa maana vyombo vya wafanyi kazi vilifanya harusi na ikulu. Vilifanya ndoa na state that means COTU, KKTC, zote zilifanya ndoa na serikali. Ina maana kwamba mpaka sasa hivi utaona serikali ili-sign agreement ya waalimu kuwalipa mshahara wao na serikali inakataa hiyo hiyo kuonekana kwamba wafanyi kazi hawawezi kuenda kokote.

Kwa hivyo twataka wafanyi kazi wawe na vyombo vya kufanya kazi independent. Hii inachukulia pamoja na judiciary. Nafikiri kwa hayo machache nisiwe nikaharibu mambo yangu lakini nasema asante sana bwana kamishina na nakuombea mungu haya yote nitayapata baada ya miezi hiyo itakayokuja.

**Com. Swazuri:** Asante sana nenda u-sign jina lako pale.Ali akifuatiwa na  Bibi Omar awe tayari.

**Mr. Ali:** Bwana kamishina mimi kuna mengi ambayo yamezungumzwa kuhusiana na mambo ya Majimbo na kila kitu kwa hivyo mimi sitazungumza mengi zaidi. Kitu ambacho nitazungumzia mtu ambaye yuatawala. Nataka awe chini ya Katiba asiwe juu ya Katiba asiwe juu ya Katiba na wakati wa Katiba ikiwa sheria itawekwa, tunataka itoe kibali ili Rais ikiwa aweze kuondolewa mamlakani kwa kitendo kisichokuwa halali kupitia kwa maoni ya wanachama, wa mikoa na kwa mambo ya usalama, mambo ya maendeleo. Katiba pia ipitishe ikiwa sheria itapitisha nchi ndio iliyo na uhusiano kati ya Bunge na Rais.

Serikali kuu ikiwa itakuwa sheria, ihakikishe kuwa wakenya wote wanafurahia haki za kimsingi kama vile usalama, hata mali na elimu na mengineo. Na ikiwa Katiba itachukua maoni yangu ni kuwa wakenya wawe na haki ya kupata habari zilizoko mikoani, mikononi mwa serikali au shirika lolote la serikali, ili na sisi pia tupate habari zozote. Na Katiba pia ichukue oni langu kuwa wahakikishe kuwa wafanyi kazi wote wana haki ya uakilishi katika vyama vya wafanyaji kazi. Na nitakuwa na maoni yangu

kidogo yangu ya kibinafsi. Wakati wa nyuma tulikuwa kuna kitu hapa kwetu kinaitwa ngambi. Ambao ngambi ni kitu ambacho tunazuia mimea yetu kama minazi zisiangushwe, ziwekewe muda. Kwa hivyo hicho kitu kinachoitwa ngambi nataka kiwe ni sheria na zetu ziangushwe kufuatana na mihula yake ile ambayo watu huangusha zile nazi.

Katiba ilinde haki ya mtu asiye na hatia na mtu atakayepatikana na hatia ahukumiwe kulingana na sheria za nchi. Katiba ilinde haki za wananchi kupata elimu ya msingi na bila ya malipo mpaka kiwango cha darasa la nane. Hilo ni oni langu la mwisho.

**Com. Swazuri:** Haya, asante sana Bibi Omar. Na atafuatiwa na bakari.

**Mr. Bibi Omar:** Salaam Aleikum. Mapendekezo ya gender women in development. Kwa jina mimi naitwa Bibi Omar na hii ni mapendekezo ya gender women in development. Katika mapendekezo ya akina mama wa gender, utangulizi wa Katiba yetu wa kenya unatakikana uwe hivi. Katiba ni ya wananchi wa kenya walio katika taifa huru lililo jumuisha makabila arobaini na mawili yaliyo na haki sawa mamlaka ya juu yawe na wananchi na kenya ni nchi huru yenye mfumo wa vyama vingi na tumependekeza mfumo wa Majimbo.

Sehemu ya pili- wanawake wawe na mamlaka sawa na wanaume. Rais akiwa mume, makamu awe mwanamke. Mayor akiwa mwanamume wa chini wake awe mke na kadhalika. Kwa sababu sisi tunaona wanawake tumezidi na kwa nini tuwe tunanyanyaswa na wanaume saa zote? Tumependekeza pia kuwe na idara ya wanawake ambayo itaanzia kutoka wilayani mpaka kwa national na huyu ambaye atakuwa mkuu wa national aweze kuingia Bunge na kutoa maoni ya wanawake wote.

Pia tumependekeza wanawake wanaoolewa na mabwana zao kufariki, wakiachiwa mali hiyo ya mabwana zao na watoto, ndugu za hawa mabwana waweze kuwaacha, waishi hapa na watoto wao kwa kuwalea vizuri halafu mali hiyo iwe chini ya huyo mama. Tumependekeza pia watoto wanaozaliwa nje ya ndoa washughulikiwe na mababa zao, kielimu, kiafya, mavazi na kadhalika, kuondoa uchokora na wizi mwingi kenya. Wanawake wawekewe wape haki zao ili kuwapunguzia mzigo wa ulevi, umaskini, maradhi ya sasa tuliyonayo.

Wakati wa ugawaji wa ardhi, wanawake walioolewa waweze kugawiwa ardhi hizi pamoja na mabwana zao majina yote mawili yaonekane katika hizo title deeds na mwanamume asiweze kuuza ardhi hiyo bila consultation ya mwanamke. Kesi za dhuluma dhidi ya wanawake zihukumiwe na majaji wanawake kwa sababu majaji wanaume wanaonekana saa nyingine wanapendelea.

Elimu ya msingi iwe ya bure na pia huduma za hospitali ziwe za bure kwa sababu mzigo huu wote unaenda kwa akina mama, ndio walezi na ndio waangalizi wa nyumba kwa hivyo mizigo mingi huwa inaachiwa wao. Serikali isambaze maji yaani hizi huduma ambazo ni za lazima kwa mwanadamu isambaze maji kwa kila sehemu bure halafu huduma hizi za kudumisha huduma za maji ziendelezwe na wananchi wenyewe ili wanawake kupunguziwa mzigo wa kutembea sehemu mbali.

Serikali iwe na makao ya wazee maskini wasiojimudu kwa mfano wasio na watoto au waliosahauliwa na watoto wao ili kuweza kupunguza huu mzigo wa kuwa mtu anaishi na njaa na kudhoofika. Na hii sana inatulalia sisi wanawake kama mnavyojua. Wanaume mara nyingi wao wakiona taabu namna ile hukimbilia kwa, sisi tuna haya. Hatuwezi kukimbilia kwa ndugu ili kukaa kuhifadhiwa. Kwa hivyo kuwe na makao ya aina hiyo ili kuangaliwa watu wa aina hiyo. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Magana.

**Mr. Magana:** Salaam Aleikum. Mimi kwa jina naitwa Salim Magana kutoka Mwaluvanga. Maoni yangu nimeyatayarisha, sitazungumza kwa maelezo.

**Com. Swazuri:** Ushaandika. Haya, asante sana. mwingine ni Zeinab Tchizuga.

**Mrs. Tchizuga:** Bwana kamishina, mabibi na mabwana, salaam aleikum. Kwa jina naitwa Zeinab Tchizuga nawakilisha makundi ya akina mama Kwale district. Haya ndio maoni yetu. Kwanza, tunapendekeza Rais lazima awe ni mtu ambaye ana miaka arobaini na tano na awe ameoa. Na kama ni mke naye awe ameolewa. Pia tunapendekeza serikali itakayokuja iwe ni serikali ya Majimbo. Majimbo hayo, Rais atakuwa hako juu ya sheria. Atagawanya mamlaka yeye na waziri mkuu. Na kama Rais ni mume waziri mkuu atakuwa ni mke.

Tumependekeza kwamba kutakuwa na sehemu mbili za utawala. Serikali kuu na serikali katika Majimbo ambayo itasimamiwa na governor. Tunapendekeza ya kwamba wale walanguzi waliolangua mali za raia hasa tukifikiria barabara zetu vile tunavyoteseka sisi akina mama. Tunazaa njiani kwa ukosefu wa barabara. Mimea inaoza kwa ukosefu wa barabara. Wale wale wanaotuma zile pesa vibaya walazimishwe kuzilipa sio kupewa transfers.

Mavazi- hivi sasa inaonekana kupitia kwa utalii mavazi, watoto wetu wanatembea uchi. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba mavazi yale ambayo wale watu wanatembea uchi yapigwe marufuku. Elimu- tumependekeza elimu iwe ni ya lazima kwa mtoto wa kike na mtoto wa kiume, kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la nane iwe wazazi wameachiwa Majimbo. Yale mambo mengine yote yasimamiwe na county councils ambapo wao watakuwa wanapata yale mapato yanayopatikana katika jimbo kupitia kwenye zile kodi.

Tunapendekeza kuwe na Commission maalum ya akina mama na watoto na Commission hii ichaguliwe na Bunge, sio Rais peke yake. Kwa sababu kumekuwa na mambo ya biasness katika Commission zingine isipokuwa hii ambayo ni ya Katiba at least kila jimbo limewakilishwa. Akina mama wakati tunasema tunataka haki zetu katika nyumba mabwana mutuelewe vizuri, kidini pia tumepewa haki hasa sisi waislamu maana tukiangalia zaidi katika dini tunaambiwa bibi ni wa kupamba nyumba tu na kustarehesha mwenzake lakini imekuwa sasa mabwana majukumu yale yamewashinda ndipo tukapigania haki zetu na tumefikia tunaweza kusoma. Kwa hivyo hatukusema nyinyi muwe chini yetu La! lakini mfahamu kichwa hakiwezi kusimama bila ya

shingo. Nyinyi ni kichwa sisi ni shingo.

Kwa hivyo haki zetu ndani ya nyumba ikiwa wewe ndio Rais wa nyumba, mimi ni makamu wa Rais katika ile nyumba. Tunapendekeza pia, wakati settlement schemes zinagawanya akina mama pia waganywe zile settlement schemes kwa sababu tumeona settlement schemes zote zimeganyiwa kina baba peke yao. Na especially akina mama ambao ni wajane wanafaa kufikiriwa wakati kama huo. Tunapendekeza hizo settlement schemes kwa wenzetu tunaona zimejengewa mahospitali na mashule lakini settlement schemes ambazo ziko katika Pwanihazina mambo kama hayo kwa hivyo settlement scheme zinazotengenezwa bara na huku pia zitengenezwe hivyo hivyo.

Tunapendekeza kuhusu vitambulisho. Ikiwa mtoto ameweza kutambuliwa na mzee wa kijiji na chief hiyo iwe imetosha. Sio ule mlolongo mrefu ambao wale vijana hawana kazi, wazazi nao hawana kazi wazazi pia nao ni maskini zile tikiti za kila siku imekuwa ni big problem na big burden kwa parents.

Mazingira na mali asili- tunapendekeza ya kwamba ikiwa kwa bahati nzuri Mungu amejalia chini ya shamba langu kumepatikana madini, mimi niwe pia nina uwezo wa ku-control yale madini, sio isemekane ondoka kwenye hii shamba, pale kumepatikana madini mwingine ndiye atakuja kusimamia yale madini. Kwa hivyo hiyo rasilimali igawanywe kwa baina ya mwenye shamba na wale wahusika.

Budget- ina mtindo ya kwamba budget inasomewa Nairobi. Unaambiwa sijui mmegawanya peni mbili sijui sumni. Tunapendekeza budget ziwe zikisomwa katika Majimbo ili tujue kila wilaya imepata nini na kiletwe direct katika ile wilaya. Tumependekeza vijana wetu wapewe grants kwa vile wamemaliza mashule na hakuna kazi. Zile grants zitawasaidia kuanzisha biashara zao ndogo ndogo na hivyo hivyo iwe walemavu pia watafikiriwa katika mkondo huo wa grants.

Katika boards zile ambazo zinachaguliwa tumependekeza kuwe na boards za minazi na mikorosho na mimea yote ile ambayo iko katika Pwani ambayo inaleta mapato na katika hizo boards akina mama pia wawemo. Kuhusu utetezi katika waBunge sisi tumependekeza forty percent akina mama wachaguliwe Bungeni. 20% akina mama wachaguliwe kwenye councils. 10% ipatiwe walemavu na hii ni kwa sababu kwa vile waBunge wetu ni wachache kule Bungeni ndio sababu hata wakituombea kitu hakipiti wale wengi ndio wale wenye tamaa kuja kunyakua kwetu lakini wakati hizi nafasi zitatolewa sawa tutaweza kupata zile haki zetu kwa usawa.

Mwisho, wale waBunge maalum, ma-councillors maalum hawa wote hizo wapewe kina mama hizo nafasi, bila upendeleo wowote provided awe anaweza uongozi. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Mwingine ni Mariam J.Sheba. Anafuatiwa na Mwanaisha awe tayari.

**Mrs. Juma:** Bwana kamishina, Bi. Kamishina Salaam Aleikum. Kwa majina naitwa Mariam Juma Sheba. Mengi yamezungumzwa lakini maoni yangu kidogo lakini maoni yangu kidogo ningependa kutilia mkazo mahali fulani. Sana sana ninatilia mkazo upande wa elimu. Sio tu serikali ama Katiba iangalie kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la nane ama university. Sana sana ningependa iangalie kutokea nursery school kwa sababu hiyo ndio foundation. Wangeangaliwa sana, waalimu na watoto kutoka nursery kabla ya kufika huko mbele. Jambo la pili, ningependa serikali ya Majimbo. Na sio eti Majimbo ya kuwa mbara kwao mPwanikwao hata. Majimbo ni kila mwananchi wa kenya anaishi popote pale kenya walakini kwa mfano amekuja pwani. Ni mamlaka ya watu wa Pwani akishapendekeza kuwa mbara kama anataka kujenga mahoteli, 75% ya katika hoteli awe ni vijana ama ni wafanyi kazi kutoka pwani. Na sana sana kuanzia general managers juu awe ni mtu wa kutoka pwani. Ikiwa atakubaliana na hivyo sawa, hatakubaliana si ruhusa ya mtu kutoka mbali aje kujenga Pwanihoteli halafu akatae mamlaka ya watu wa pwani.

Mambo mengine ningependekeza kuwa mambo ya passport itolewe kama vile inavyotolewa mambo ya kitambulisho. Sio kwamba ipitishwe huku na huku na pesa na nini kwa sababu ya passport itolewe kama sawa na kitambulisho kwa mwanakenya yeyote. Nikipitia kwa upande wa akina mama. Ningependa akina mama wachukuliwe sawa ama nusu tukisema sawa itakuwa tumeingia waume kwa zaidi lakini ningependa, wachukuliwe nusu kwa mfano, juu akiwa mume, chini yake ni mwanamke kwa sababu tumeona wanawake, tumeteuliwa sana nyuma. Sina mengi ya kusema ningependa tu kusikiza. Samahani kidogo, yeyote ana swali kutokea hapo?

**Com. Baraza:** I want to understand this federal structure. Umesema kwamba watu wa nje wanaweza kuja waka-invest hapa. Hiyo ni sawa?

**Mrs. Juma:** Mtu wa nje kutoka Kenya.

**Com. Baraza:** Hatutaki kuua hii nchi. Tukiongea maneno yetu tuangalie tuone kwamba hii ni nchi. Tukiongea maneno yetu tuangalie tuone kwamba hii ni nchi yetu ambaye hatutaki kuua. Kwa hivyo ni shida gani mzungu kuja kuweka pesa hapa? Hakuna. Ni nani ndio wasiwasi?

**Mrs. Juma:** Nimesema wakubaliane kama ni mzungu kama ashafika huku wakubaliane na watu wa pwani.

**Com. Baraza:** Na unajua hiyo itakuwa private investments. Haitakuwa investments ya serikali. Sasa utamwingilia namna gani? Si utafukuza watu ambao wanataka kuleta pesa hapa? Na hiyo ni private investment na akikataa tutafanya namna gani.

**Com. Swazuri:** Haya, Mwanaisha Mwaviriko. Mwanaisha haraka haraka kidogo. Atafuatiwa na Salim Mwalaulo.

**Mrs. Mwaviriko:** Bwana kamashina, Bi. Kamishina, kina baba, kina mama salaam aleikum. Kwanza maoni yangu

ningependekeza kuhusu uchumi. Ningependekeza serikali itujengee shule ya utalii huku kwetu pwani. Wafanyi kazi wote wawe asilimia ya tisini na tano ya watu wa pwani, asilimia tano iwe watu wa bara.

Mahoteli yetu tuliofanya ama yaliyojengwa huku Pwani asilimia kubwa ni ya watu wa nje lakini asilimia ndogo ni ya watu wa pwani. Sasa ningependekeza asilimia ya sabini na tano iwe watu wa pwani, asilimia ishirini na tano iwe watu wa bara.

**Com. Baraza:** Owners or workers?

**Mrs. Mwaviriko:** Workers.

**Com. Baraza:** Na hoteli yenyewe 75% iwe ya watu wa bara au?

**Mrs. Mwaviriko:** Hata hiyo hoteli yenyewe yaani. Wawa washirika sasa na watu wa Pwanikuanzia wakubwa. Kuhusu elimu ningependekeza kuwa elimu iwe ya bure kuanzia nursery hadi form four. Mzazi awe na gharama ya kununua form na mahitaji ya mtoto lakini sio elimu. Form four, kuanzia nursery mpaka form four. Mzazi awe na gharama ya school uniform na mahitaji ya mtoto.

Hospitali zetu hizi. Huduma zimekuwa ndogo kwa sababu ya kuwa hatuna uwezo. Wengi wanaumia kwa magonjwa kwa sababu ya kuwa mfuko ndio kidogo, pengine hana uwezo wa kutosha kwa kuwa atajihudumia ugonjwa alio nao. Hapo hapo pia ningependekeza, kuwe na madaktari wanawake special wa kuzalisha kina mama. Sio mwanamke azalishwe na bwana.

Wanawake wawe na mamlaka sawa na wanaume. Panapokuwa na mume ambaye ni kiongozi chini yake awe ni mwanamke. Kuhusu ndoa zetu- kina mama tunateseka sana kuhusu ndoa zetu kwa sababu kina baba hawataki kutuoa. That is why tunakosa ule uridhi wa kutosha kwa sababu ya kuwa bwana hakukuoa. Pengine ulimwambia akuoe lakini akakataa. Akasema nitakuoa lakini mbeleni amepata mrembo zaidi ya wewe. Maoni yangu ningependekeza vipi? Baada ya kuishi na baba ama na kaka mama huyo baada ya miezi mitatu ikiwa hatataka kukuoa baada ya miezi mitatu kuwe kuna koti ama Kadhi ambaye utaenda kumshtaki. Either akuoe baada ya miezi mitatu ama akuache mwaachana.

Na pia ningependa mwanaraia wa kenya atambulike either ni mlemavu ama yuko sawasawa maanake hata mlemavu pia naye ni raia wa kenya. Wawe na vyeo vyao ama skuli zao za bure. Upande wa wazee ningependekeza vipi, wazee basi afanya kazi, hakufanya kazi awe retired, haku-retire lakini kufikia miaka hamsini, awe ana malipo kiasi fulani ambayo serikali itapendekeza. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Salim Mwalaulo. Haraka haraka.

**Mr. Salim:** Bwana kamishina, akina baba, akina mama nyote salaam aleikum. Mimi maoni yangu kwanza nitazungumzia kwa upande wa serikali. Kwa maoni yangu nataka serikali iwe ya Majimbo na watafadhahisha wale ambayo wakati tukitaja Majimbo nasikia woga sio hivyo, sisemi wale wenzetu wa bara. Mimi nasema Majimbo sio kukosana bali tu nikuwa kupawa uwezo ili wa kuweza kujisimamia wenyewe. Pili, nazungumzia kwa upande wa Rais.

Rais asiwe na mamlaka zaidi, apunguzwe mamlaka kwa sababu, kwa mfano huyu wetu tuliyenaye Rais moi shida yake ni kwamba kwa mfano ameteua Tumekama hii akiona pengine inamlemea yeye anasema hiyo Tumeninaivunja. Kwa hivyo nasema Rais asiwe na mamlaka zaidi wakati anapoteua tume. Hata hii Tumeya kurekebisha katiba, kwa maoni yangu nasema ghai awepo na Tumehiyo hiyo iendelee bila kubadilishwa mpaka iweze kumaliza kazi yake. Kuhusu utawala- mapendekezo yangu nasema hivi kuhusu upande wa special wa wilaya, toka niwe mkubwa ama niwe na fahamu sijaona DC wa kidigo hapa Kwale na maDC wako wa kidigo. Kwa hivyo naomba sheria ama hii Katiba iweko ya kila mtu hapa kenya aweze kuenda ile sehemu atakayo ataweza kupawa hiyo kazi. Kwa hivyo, kwa maoni yangu nasema kuwe na hiyo sheria kwamba kila mwananchi aweze kufanya kazi popote.

Michezo- kulingana na maoni yangu. Ninaona matatizo makubwa sana hapa kenya nikiona mfano timu ya taifa ambao wanacheza ni akina Omondi, akina Waweru lakini utaona mdigo ama mtu wa coast hakuna. Kwa hivyo kwa maoni yangu nasema iwe sheria kwa kila mkenya aweze kupatiwa hiyo nafasi. Kuhusu mashamba- sitazungumza zaidi nafikiri jambo hili limezungumza sana lakini natilia mkazo ya kwamba kuna viongozi ama kuna wale ambilikanao walikuwa uongozini zamani na wakanyakua hizo ploti na mpaka sasa wako nazo. Kwa maoni yangu nasema hizo ploti zirudishwe kwa wananchi.

Elimu- kuhusu elimu nataka irudishwe ile ya zamani kama mfano ile ya std. 1 mpaka std. 7 halafu form 1 mpaka form 4, na form 5 mpaka form 6. hii inawezesha mtu awe akimaliza awe na elimu ya kutosha kuliko hawa sasa mtu anapita university na hata kizungu hawezi kuongea. Kuhusu hospitali kwa mawazo yangu hii cost-sharing iondolewe kabisa kwa sababu wengi wao hawana uwezo wa kuwezesha kuenda hospitali. Kwa mfano kuna mtu haendi hospitali na ni mgonjwa anaweza kutibiwa namna gani kama hana cost sharing. Daktari akipewa mtu huyo anapuuza na mtu huyo yuafa bila matarajio.

Bunge- kwa mawazo yangu nasema mBunge asiweze kupewa mshahara wa juu kama hivi sasa ambapo anapata laki sita ambapo anapata laki sita. Ambapo mfano kuna councilors, mtu anapata elfu saba ama elfu tano. MBunge kwa mfano kwa maoni yangu apate kama laki nne na nusu ama tano, councilor apewe kama kumi na tano. Kwa maoni yangu, asante sana.

**Com. Swazuri:** John Mwania na atafuatiwa na bwana Kaimba Mbelu.

**Mr. John Mwania:** Asante sana wanaohusika. Mimi maoni yangu nilikuwa nazungumzia kwa upande wa president. President anaruhusiwa awe na kipindi ambacho kimekubaliwa na wananchi, kama ni kipindi cha two terms na awe ni mzuri kiasi gani. Yaani iwe ni kama ni sheria yeye ashamaliza kipindi, kama ni two terms akimaliza awe amefanyia kenya 800% profit wakenya

wanasherehekea mpaka wanalalia pesa, aondoke. Two terms of 5-5. nilikuwa nazungumzia kwa upande wa elimu kidogo. Ningependekeza serikali, zile universities zote zimepangwa huko juu, hapa pawe na universities. Maanake kama Majimbo tutapata, tutahitaji universities maanake wale ambao wanaendeleza Majimbo they must be learned. Kwa hivyo university hapa mtoto mwingine kulingana na vile watu wanaishi wajua watu wana tabia tofauti. Kuna kasumba ambayo ya kuwa ama itikadi fulani inayomfanya mtu hawezi kuenda mbali na wazazi. Unaona? Sasa kama pengine amechukuliwa university ama ana kiwango cha kuchukuliwa university, ana-prefer aende college fulani badala ya kwenda university. Na hiyo ndio inalete nyuma sehemu hii yetu. Inakaa mpaka hatuna nafasi nyingi katika serikali. Kwa hivyo university ikiwa hapa, hata mtu akiwa na low grade he can also improve university because we have some people who go to university with low grades and at the end wanajiendeleza mpaka wanakuwa ni watu wa kutegemewa. Kwa hivyo ile nafasi kama haikupatiwa watu hapa university kama Mombasa itapatia watu chance sasa ikuwe ili-fail ukienda pale utajiuliza uli-fail vipi na uta-pass.

Kitu kingine ningetaka kuzungumzia ni, imezungumziwa kwa upande wa pesa (currency). Nilisikia nikiwa hapa lakini kitu yangu nilikuwa nimesema hivi, kama president ndio ametoka, ile pesa isi-change. Why? It is very expensive to process another kind of money ikipea picha ya yule mtu na ambapo tunalia sisi hatuna pesa. Kumbe pesa tunaitumia kindanindani zinakwisha. Kwa hivyo ile process imetumia pesa nyingi.

**Com. Swazuri:** Sasa tuweke picha ya nani?

**Mr. Mwania:** Ya yule previous president yule alikuwa, kama vile Europe wanafanya ama America. The first president picha yake inakaa. Because ku-process hiyo pesa irudishwe ilete ni pesa nyingi sana.

**Com. Swazuri:** Kwa hivyo tubaki na ya Kenyatta?

**Mr. Mwania:** Hapana, sitaki ile ya Kenyatta. Nataka yule atakayeanzia ikiwa serikali itakubali. Sitaki warudishwe mpaka kule. Nasema the current president yule yuko, ikubaliwe president atakayekuwa ile pesa iliyoko akitoka picha yake iendelee hivyo.

Ingine ni kind of government. the kind of government ingetakiwa wale ambao wanasema national unity, ikiwa ndio itakuwa pawe na follow-up maanake mtu ameajiriwa ofisini the other day anapewa mabasi manne na mshahara wake uki-assessiwa kwa serikali unajulikana, zile grades zinajulikana. Serikali ifuatilie yule mtu amepataje mpaka amejenga magorofa tano, na amefanya kazi miaka mitano. Na kiwango cha mshahara wake kinajulikana. Hiyo pesa ametoa wapi.

**Com. Swazuri:** They should declare their wealth.

**Mr. Mwania:** Their wealth. Upande wa MPs, mshahara yao should be lowered to less than two hundred thousand. Between

90 and 120 kwa sababu nasema hivi, ndio sababu unaona wakienda kule hawazungumzii mambo ya pesa za watu. Wakienda kule wanadanganywa wanazungumzia watu tunateswa na ndio wanatutesa. Kama mshahara ya MP wetu amechukua ama analipwa 600,000 how much tax can be paid to a person who works in a DCs office as a clerk anapata elfu sita, anaweza kuandika clerks wangapi kenya nzima.

**Com. Baraza:** Si atawapatia kidogo?

**Mr. Mwania:** Apatie nani? Hapatii mtu.
**Com. Baraza:** Na barabara?

**Mr. Mwania:** Na kitu kingine.

**Com. Baraza:** Na harambee?

**Mr. Mwania:** Harambee, mpaka tumwite yeye hajui tulimchagua. Ngoja nizungumzie kwa upande wake vile tunataka MP awe. MP tunataka awe pawekwe sheria katika kenya iwe MP kuja kuona watu wananchi kule waliomchagua iwe ni lazima na imepangwa iwe kwenye ratiba. Si wakati ule anajisikia yeye ana problem ndio anakuja na kuwe na terms zake aki-fail iwe ni kama Bungeni. Mbona Bungeni aki-fail kwenda Bunge tatu haruhusiwi kuingia? Kama haruhusiwi kuona wananchi wale ambao walimchagua wamwelezee mambo yake, sisi tuna-vote of no confidence na tunaandika barua unanimously tunasema sisi hatumtaki.

Upande wa chief- chief or sub-chief ni lazima awe ni mtu ambaye ana vision ya pale mahali na mtu ambaye hana vision mara nyingi kulingana na world vile dunia inaenda, mtu ambaye mara nyingi vision ya mtu ambaye hajasoma iko limited. iko na kiwango chake nafikiri. Ukimwendea zaidi ya hapo anaona kama ni matusi. Chief maanake ndio kiongozi na ndio macho ya serikali. Huko ngazi ya chini, ni mpaka awe ni mtu amesoma na akiwa mpaka form four na ikiwezekana hata ikiwa ni university na kiwango cha mishahara yao iambatane kulingana na education yake vile inakaa.

Achaguliwe, maanake tumeona mambo ya kwenda kwa DC kwenda kuchaguliwa pale anamchagua kwa sababu yeye ndio anaunga mkono MP fulani apite kwa sababu ni wa chama cha KANU ama chama cha NDP. Mtu yeyote wa kenya anaweza kufanya kazi mahali popote. Mimi wakati niliajiriwa niliambiwa uko tayari kufanya kazi mahali popote? Nikakubali. Kwa hivyo mtu yeyote anaishi kenya, ana ruhusa ya kukaa mahali popote lakini ikiwa ana kitu ambacho anataka ku-process kama yeye amekuja kuishi hapa.

Amekuja Kwale kwa mfano kama mimi nimekuja hapa lakini within a short time nina-land over one hundred thousand acres. Sasa mimi either nitumie njia nzuri. Sasa hiyo ni lazima hiyo kitu iende na iwe open kwa administration kutoka kwa DC,

administration yule mtu alipata na wananchi waelezewe yule mtu alipata vipi, maanake zile fununu watu wanazungumza either huyo mtu apitie njia nzuri akapata, lakini wananchi wa kawaida hawawezi kuelewa ile kitu ilipatikana vipi.

Lakini kama kuna procedure za kuelezewa hii kitu ilipatikana hivi na hivi hutasikia watu wakinung'unika. Kitu ingine, education ile ambayo iko, quarter system is very hopeless. Kwa hivyo serikali igeuze quarter system eti kama ni Kwale High ichukue 85% ya watoto wale wanakaa hapa. Hiyo ndiyo chanzo cha nyumba na skuli kuchomwa na strike. Kwa sababu watoto wale wako, / kunatoka watoto kumi form one na the other year walitoka watano.

Those ones are very easy to organize strike in the school. Kuliko watu wamechaganyika. Maanake kama iko hapa Kwale High, it is a provincial school, kama watu wanatoka Meru, wengine wanatoka Kikuyu, wengine Kisumu kuja Kwale High, it is not easy for these kids to organize a strike kwa sababu wote walitoka kwa hali tofauti na kila mmoja alitoka kwao akijua nimetokaje, lakini wale walitoka kijiji kimoja, ni rahisi kuchoma shule na kugoma na kukataa kusoma na ku-fail. Kwa hivyo hii quarter system iondolewe kabisa.

Na nikiondoka hiyo, nilikuwa nataka kusema, katika religious, tumezungumzia mambo ya watalii kuja hapa. Lakini inakaa watu wa religion, wale ambao ni waislamu wanajua uislamu na wale wakristo wanajua wakristo, njia zile watoto wanavalia nguo, akitoka nyumbani kwako unamwona. Mwislamu anaruhusiwa na si mwislamu yeyote, mtu yeyote haruhusiwi kuvaa nguo ambayo inatoka juu ya goti. Lakini mtoto akitoka nyumbani amevaa ndefu sio lakini transparent, akikaa anaonekana suruali ya ndani na wewe mama pale anatoka na wewe ni mwislamu, wewe ni mkristo. Halafu unaanza kusema mambo ya nguo.

Hiyo tungetaka serikali I-set. Kama religious people wataheshimu ile religion ile yao, watoto hawaruhusiwi kuvaa hivyo. Imekuwa wanavaa nguo suruali ndani akitoa ile nguo anatoa anaweka. Haheshimu mungu, haheshimu dini yake na ile watu watazozana wakisema wameambukizwa na watu fulani lakini sisi wazazi ndio tumewaambukiza. Asante sana.

**Com. Swazuri:** Andika jina lako.

**Juma:** Bwana Don umezungumza vizuri lakini nataka uniweke wazi pahali pamoja. Umesema kwamba chief achaguliwe na wananchi. Elimu yake ianzie form four up to university.

**Mr. Don:** Sheria hairuhusu. Ni Commissioners tu peke yake ndio wanaoruhusiwa kuuliza maswali.

**Com. Swazuri:** Bwana Daima Heri.

**Mr. Daima Heri:** Bwana kamishina na wote mliopo, Salaam aleikum warakba tulai wabarakatu. Mimi kwa jina naitwa Daima

Heri, mkenya kutoka mkoa wa Pwanilakini hapa nitatoa maoni yangu kama mkenya, na wala si kama mtu wa pwani. Nitaanzia kwa utangulizi. Nitaanzia kwa utangulizi, nasema Katiba inayoandikwa iwe na utangulizi. Lna katika utangulizi huu, kwanza iwe katika lugha ambayo inaeleweka na wakenya wote, yaani lugha rahisi. Halafu katika utangulizi, isisitize uwezo wa watu kuitetea hata kama ni kufa.

Yaani mtu yeyote ataenda kinyume na katiba. Wananchi wawe wana uwezo wa kuleta ile tunaita civil disobedience. Halafu katika utangulizi Katiba hii iwe na provision ya vifungu maalum, ile tunaita kwa kiingereza special enshrined provisions. Kwa mfano, kile kifungu ambacho kitatueleza jinsi ya system ya government, muundo wa serikali citizenship, vifungu hivi viwe kati ya vile vifungu maalum ambavyo kurekebishwa kwake lazima vipitie kwa referendum, wananchi wote wahusishwe kuvibadilisha vifungu hivi. Na vile vinginevyo kwa sababu huenda Katiba hii tunayoindika ikapitwa na wakati basi pia nayo kama nikubadilishwa, ibadilishwe na national conference(mabaraza ya kitaifa) wala si Bunge.

Nikitoka hapo ninaenda kwa system of government. Nimesema hapa mimi nitaongea kama mkenya wala si kama mtu wa pwani. System of government, Katiba iwe ya Majimbo. Kuwe na provision ya federal system, si kwa sababu natoka Pwanikuna uchumi mwingi, bali hii ndio muundo peke ambao unafanya vizuri kwa jamii ambayo haikushikamana.

I am referring to a cohesive society. When the society is not cohesive like the Kenyan society, basi mfumo wa Majimbo unatambua wakenya wanataka nini. Na katika mfumo huu ufuatiliwe na mfumo wa Bunge ule tunaita parliamentary system kuhakikisha ile tunaita transparency and accountability kwa sababu mfumo huu wa parliamentary ni ule ambao utakuwa na waziri mkuu ambaye atachaguliwa kutoka kwa chama kilichoshinda na waziri mkuu huyu awe mkuu wa hiyo serikali.

Halafu kuwe na president ambaye atachaguliwa moja kwa moja na wananchi na president huyu awe ni mkuu wa dola (head of state). Hapa kutakuwa na ugawaji wa mamlaka kwa mfano, huyu mkuu wa dola awe na uwezo wa kulivunja Bunge kama ambavyo Katiba itaeleza vipi avunje Bunge kwa mfano maoni yangu nasema president huyu awe na uwezo wa kuvunja Bunge wakati kuna wale tunaita MPs elect. Yaani kura za Bunge zifanywe kabla Bunge halijavunjwa.

Pili, tuepushe kuwa kutokuwa na / ya Bunge kwa kipindi fulani katika kenya. Kwa hivyo baada ya kuwa na MPs elect, ndipo huyu bwana awe na uwezo wa kulivunja Bunge wakati anaopenda. Na parliamentary system hii kuwe na provision katika Katiba ya kuruhusu serikali ya mseto. Serikali ya zaidi ya chama kimoja kwa sababu tunataka katika Katiba tuwe na Bunge, chama kinachotawala kiwe na asilimia fulani. Kwa maoni yangu, asilimia hamsini na tano ya viti vya Bunge.

Kwa hivyo kuwe na provision ya opposition ili ikiwa chama kilichoshinda hakikufikisha asilimia hamsini na tano basi kusiwe na shida na gharama ya kufanya uchaguzi mwingine bali iweze kushirikiana na vyama vingine ili wajiunde serikali. Hayo yote ni matumaini yangu au ni matakwa yangu, kuwa yafanywe kwa njia ya kidemokrasia, yaani kila mahali kuchaguliwe kwa kura (direct democracy).

Pili, nitaongea juu ya citizenship (Uraia wa kenya). Kwanza, cheti cha kutambulisha uraia. Ni mapendekezo yangu iwe passport. Kuwe hakuna mambo ya vitambulisho. Mtoto akizaliwa apewe birth certificate na apewe passport. Hiyo itakuwa inaonyesha kuwa yeye ni mkenya na ana umri gani na anaruhusiwa kupiga kura au la na hapa Katiba hii isiwe na ubaguzi katika citizenship kwa sababu kwa mujibu wa Katiba iliyopo, yule mke nitakayemuoa mimi kutoka Uganda, anaruhusiwa kuwa mkenya moja kwa moja. Kwa hivyo tunataka Katiba ijali uraia wote ambao watakuwa na at least mzazi mmoja mkenya wapewe uraia regardless of gender. Parliament- mimi ni mapendekezo yangu baada ya kuwa na mfumo wa Majimbo wakati tuna house of representative and the regional parliament, I am now talking of the house of the representative. Bunge la kenya liwe na waBunge sawa kila jimbo. Ikiwa ni coast, whatever the number of regions. Kama ni central ina waBunge hamsini na coast iwe na waBunge hamsini kwa sababu pale ndipo mahali wakenya wote wanawakilishwa na wakati wa vote, isiwe kuna jimbo jingine lina vote zaidi ya ziada.

Pwani ikiwa nchi za afrika zimekutana mahali na ni kupiga kura ile kura ya Nigeria iliyo na watu milioni tisini, huwa sawa na kenya ambao ina watu milioni thelathini. kwa hivyo regardless of how popular that region is it should have the same number of representatives in parliament as the rest of other regions. Halafu katika Bunge nitaongea kama kijana. Katika Bunge nataka kila wilaya kuwe na mwakilishi mmoja anayewakilisha wale watoto wote hawakupiga kura na mtu huyu, mBunge huyu awe kati ya miaka kumi na nane mpaka thelathini.

Naomba mnisikilize kwa makini. Naomba katika Bunge kuwe viti vya uakilishi vya watoto wale ambao hawakupiga kura na wawakilishi hawa mfumo ninaopendekeza mimi wawe katika kila wilaya na jinsi ya kuchaguliwa (qualification) ya mtu ambaye anawakilisha watu wao awe na umri ya kati ya miaka kumi na nane na thelathini, asiwe mzee.

**Com. Baraza:** Are you proposing a bi-cameral house or a uni-cameral house? Two houses or one house.

**Mr. Daima:** Two houses.

**Com. Baraza:** Now, which one should have equal representation?

**Mr. Daima:** The house of representative, the national parliament.

**Com. Baraza:** The parliament, the lower house.

**Mr. Daima:** Not the lower house the upper house.

**Com. Baraza:** And the lower house.

**Mr. Daima:** Itapata the same testing. I will present a paper to you.

**Com. Baraza:** Fine, I just want to understand. You want to introduce proportionalism.

**Mr. Daima:** Yes, in both houses.

**Com. Baraza:** What about the right of the voter, direct representation we do away with it.

**Mr. Daima:** It should be there, direct representation in respective regions, they should be there. Nitakwenda haraka haraka sasa.

**Com. Swazuri:** One minute, you give us the document, we shall read it.

**Mr. Daima:** Baadaye maanake haiko hapa.

**Com. Swazuri:** Lakini hatuwezi kukupatia uende kuilete.

**Mr. Daima:** Sasa hivyo ndio wakati wapita. Land rights- mimi napendekeza ardhi zote za serikali ambazo zinagawanywa zipewe mtu ambaye hamiliki ardhi mahali popote. Naomba ieleweke hiyo.

**Com. Swazuri:** Hebu rudia tena.

**Mr. Daima:** Ardhi zote za serikali zinazogawanyiwa wananchi, qualification ya kupata ardhi hiyo, uwe humiliki ardhi nyingine mahali popote. Koti ya Kadhi napendekeza kuwa isiwe na kukata rufani kwa high court. Kuwe na system, kuwe na koti ndogo ya Kadhi, koti kubwa ya Kadhi na hukumu ya koti kubwa ya Kadhi ikipitishwa should not be subject to any appeal to in any court in kenya.

Uajiri wa serikali- uajiri wa wafanyi kazi wa serikali, ufanywe katika hali ambayo retirement age isizidi miaka hamsini ili vijana wapate kazi.

**Com. Swazuri:** Nenda upatiane memorandum yako pale. Asante sana.

**Mr. Daima:** Inshallah! Kwa hayo machache asanteni lakini nitapata memorandum yangu ambayo.

**Com. Swazuri:** Ali Mgore na atafuatiwa na Fatuma Mwachichi.

**Mr. Ali:** Salaam aleikum. Kwanza mabwana na bi. Kamishina. Huu muda wa dakika tano ni mfupi sana mtu kuweza kutoa maoni yake lakini tutajaribu na mimi nitazungumza kwa haraka haraka tu kwa sababu yatakuwa ni mengi. Halafu nitazungumza yale ambayo ni muhimu tu halafu memorandum yangu nitawasilisha baadaye. Kwanza ningependa nizungumzie ama niombe nyinyi mnizikize sana kwamba watu wa Pwaniwanataka Majimbo kwa sababu ni haki ya watu wa Pwanikuipata serikali wanayoitaka kwa sababu, tulipopata uhuru watu wa Pwaniwalifanya kushauriwa ikiwa wanataka kuwa katika serikali ya kenya au hawataki kupitia kwa referendum.

Referendum hii ilifanywa pwani, haikufanywa kila mahali. Kwa hivyo Pwani ilitambulika tangu hapo kwamba ni mahali tofauti kidogo na sehemu nyingine yoyote. Tukapatiwa haki ya referendum. Kwa hivyo tukapendelea kwamba tuwe katika serikali ya kenya. Hatukuwa kenya kwa kulazimishwa na mtu. Tulichagua kupitia referendum na ni makubaliano kwamba tuna haki hiyo wakati wowote kwamba tukipendelea kivingine, au tukipendelea serikali ya aina nyingine watu wa Pwanini lazima wapewe haki hiyo.

**Bishop Njoroge:** Unasema, Pwani ilikuwa sehemu nyingine ambaye haikuwa kenya na sasa wenyewe wanaonekana ndio wanataka.

**Mr. Ali:** Nimekuelewa.

**Bishop Njoroge:** Ngoja, sasa wewe na uhuru wa Pwaniunataka iwe / ingine au Pwani iwe kama ni ingine kama ni Nyanza au Central ambao iko kenya lakini ina ruhusa ya kuamua mambo ambayo inahusu wananchi.

**Mr. Ali:** Haya, twende pole pole. Nitakupeleka pole pole nasema hivi, Pwanikihistoria kulikuwa na British protectorate na kulikuwa na British colony. Wakati wangu utakwishwa kwa hivyo nataka kufupisha. Hii ilikuwa ni british protectorate, ilikuwa ni sehemu mbali na british colony kwa hivyo sisi kama protectorate tulikuwa ni sehemu tofauti na tulitoa maoni yetu ya kwamba tunataka tuwe kenya moja na wenzetu. Sasa ikiwa wakenya wa sehemu nyingine wale waliokuwa katika kenya colony, hawataki sisi tuwe Majimbo. Sisi tunasema watu waliokuwa katika British protectorate wanataka Majimbo wawe wakitaka wasitake.

Yaani sehemu ya Pwani inasema hivi, kwamba ikiwa sehemu zile saba yaani mikoa mingine saba wao hawakupendelea Majimbo basi wao watakaa kama sehemu saba lakini humu kwa Wapwani, kutakuwa ni sehemu ya kenya ndio mapenzi yetu lakini itakuwa ni jimbo. Itakuwa ni state under a governor, hapa. Nataka kwenda haraka haraka wakati wangu utakwisha.

Kama ilivyo desturi ya serikali yoyote ya Majimbo najua mapendekezo yetu, ikiwa wale wenzetu wamekataa kutakuwa na Majimbo mawili. Kutakuwa na jimbo la Pwanina jimbo la bara, kisha kutakuwa na Rais wa nchi atakayechaguliwa na watu wote, kisha kutakuwa na waziri mkuu atakayechaguliwa katika Bunge kwa kawaida ni chama kilichoshinda ikiwa hakuna chama kimoja kinachoweza kuunda serikali itaruhusiwa kuwe na serikali ya mseto (coalition government) na waziri mkuu huyu ataliteua baraza la mawaziri atakuwa na haki ya kuteua na viongozi wengine wa serikali yaani judiciary na vile vingine.

Lakini atakapoteua, lazima wale aliowateua yeye wapate approval kutoka kwa Bunge, yaani hatamchukua mtu tu kwa kuwa ni rafiki yake ambandike aseme huyu ni waziri wa elimu. Amchukue huyu ndiye tumekuwa naye miaka mingi kwa hivyo nitambadika atakuwa waziri wa state. Ili kwamba Bunge liwe na haki ya kumwangalia kwamba je, huyu aliyeteuliwa anayo elimu ya kutosha ya kutekeleza wajibu huu. Pili, je, limetumika haki katika kugawa ama kwa mfano au labda kwa mfano yeye huyu ni mkalenjin amechagua baraza la mawaziri na wakalenjin kumi. Tunazungumza wazi wazi mambo ya serikali, tunaunda Katiba bwana.

**Com. Baraza:** You have the freedom to talk.

**Mr. Ali:** Hatukutukana mtu. Sasa,

**Bishop Njoroge:** Ngoja kidogo, katika Act yetu inamruhusu mtoe maoni na tutakupatia wakati wetu wa kusema kabisa kwa sababu hiyo ndio maoni yako lakini / kwa sababu sheria haituruhusu tufanye siasa ya mtu au kabila. Lakini unaweza kusema Pwanitunataka jimbo na tutajitawala. Huna haja ya kusema kabila lingine.

**Mr. Ali:** Kwa hivyo nasema kwamba ili Bunge liweze kulinda haki ya mwananchi liwe na uwezo wa kuweza kuwakagua wale walioteuliwa kwa sababu tumeshaona kwamba mtu anapochaguliwa kutoka kabila fulani anakuwa na upendeleo wa kuzidisha wale aliowateua kutoka kwa kabila lake. Hii ndio unyonge wa afrika. Kisha tunasema kwamba nazungumza habari ya emergency powers kuhusu huyu waziri mkuu langu likiwa kuna hali ya vita.

Waziri mkuu amesema tumevamiwa. Kwa hivyo wamepeleka jeshi kule linapigana. Lazima waziri mkuu apate approval ya Rais kwa muda usiozidi masaa arobaini na nane na lazima apate approval ya parliament kwa muda usiozidi siku nne. Asiwe na uhuru tu wa kufanya anavyotaka. Huyu waziri mkuu atakuwa ana haki ya kuchaguliwa kwa asilimia hamsini na moja kura katika Bunge.

Bunge litakuwa lina uwezo wa kum-impeach president au waziri mkuu prime minister. Nikisema hivi kwamba mfumo ulioko sasa, Rais alioko ana nguvu zaidi za kupita kiasi, hata anapofanya kosa linaloeleweka ama linaonekana wazi wazi, hakuna njia ya kumvuta karibu na kumweka katika sheria. Sasa iwepo uwezekano huo kupitia kwa Bunge liwe linaweza kumgandamiza huyu na ikiwa atapatikana na makosa yale, / yanayoeleweka wazi mambo kama haya yaliyofanyikafanyika hatutasema. Iwe

Bunge lina uwezo wa kumwondolea pale mbali maanake likishasema kwamba halina imani naye kazi yake hiyo imekwisha.

Nasema sasa kwamba serikali, tumesema tunataka governor awe atachaguliwa na ikiwa governor atachaguliwa hapa tunasema yeye governor atachagua watumishi wenzake wote kutoka kwa area hiyo hiyo, kutoka kwa watu hao hao. Yaani ikiwa sisi tumemchagua governor wetu wa pwani, maDC wake watakuwa ni watu wa Pwanina hivyo kuendelea. Tunasema kuwa katika hiyo administration, chief kulingana na maoni ya wengi wa watu atachaguliwa na watu.

Jimbo la Pwanilina wakaazi wengi ambao ni waislamu tunataka chief Kadhi awe atachaguliwa na baraza la ma-imamu, baraza la ma-imamu liwe ni chombo kinachotambuliwa na serikali. Tunasema hivi, kuna sehemu nyingi ambazo zilikuwa marginalized, zilisahauliwa. Sasa tunataka iwe ni provision katika constitution kwamba elimu ya bure lazima kwa kila mtu mpaka darasa ikiwa ni darasa la nane au ni la saba. Yaani primary school education iwe universal, tena lazima na itasimamiwa na Majimbo kwa sababu kwa sababu muda hauniruhusu, memorandum itaeleza jinsi gani ya kugawa zile fedha.

Yule dada aliyekaa hapa akapendekeza kwamba watu wakisha-come-we-stay, watu wakishakaa kwa miezi mitatu iwe kutakuwa na hiari, mimi nasema hivi, watu wakishakaa kwa miezi mitatu iwe kulingana na sheria ameshakuwa ni bibi yake fullstop! Mwisho namaliza nasema hivi, kwamba Rais na waziri mkuu wote watakaa kwa vipindi visizidi vipindi viwili. A maximum of two 5-year term kisha Rais atachaguliwa siku tofauti na waBunge yaani kutakuwa na separate presidential elections na general elections. Kwa sababu gani? Ili kusiwe na ile vaccum of powers ambayo hutumika vibaya.

Kwa mfano kama huu ujira sasa tulivyo. Rais tunakwenda kumchagua na yeye bado ni Rais. Ana uwezo wa kufanya vyovyote saa yote hata wakati mnatia kura kwenye debe. Hatutaki hiyo tunasema kwamba tutafanya general election year halafu tutafanya presidential elections. Na hii presidential election wakati tunapoifanya nguvu zote zile zinazomhusu Rais zitakuwa zimerudi kule kwa speaker wa Bunge ili kwamba asiwe na uwezo wowote wa kuweza kufanya lolote, wa kusema haya madebe haya chukueni, bwana DC fanya hivi la.

Memorandum nitaiwasilisha, jambo la mwisho la kuwa wafanya kazi wote katika jimbo hili la Pwanitunasema asilimia sabini na tano watoke hapa. Wote any institution. Company, education institution, whether it is a government institution whatever. 75% must be people from here. Asante muda wangu haukutosha lakini nakushukuru.

**Com. Baraza:** Thank you Mr. Digore. I just want to understand, constitution making is about understanding people also. I just want to understand. This federalism, in your mind it is to bring services and governance near the people or the people of Pwani are just allergic to people of bara. I get this feeling that it is that hatred for the people is it to bring governance and probably a fairer distribution of national resources to the people or it is just these people of bara you have got nothing to do with them. Let

me understand this. ‘

**Mr. Ali:** Asante sana bi. Kamishina. Kwanza ningependa nikueleze kwamba sisi watu wa Pwani iko desturi ni watu wapole tena tunawapenda wenzetu sana. kwa hivyo tunavyosema tunataka mfumo huu wa serikali ni kwa sababu tumeona huo ndio mfumo peke yake unaoweza kumpatia yule asiyetaka fujo, asiyetaka dhuluma kupata haki yake. yaani tunawapenda wenzetu lakini imeonekana kwamba wao wanapopata mamlaka wanatumia vibaya mamlaka na kunyakua hata kile ambacho ni cha ndugu yao.

Sasa serikali hii tumeipendekeza ndio ambayo inaweza kumpatia ulinzi wa haki zile ambazo ni /. Ambazo zile hata mtu wa Pwani anaweza kuzifurahia maanake hapendi fujo mtu wa pwani. So it is to bring those services and rights closer to the people. Sio kwa chuki, kwa sababu madola mengi katika ulimwengu huu leo ambayo yana watu tofauti tofauti kama hizi sisi. Kwa mfano kuna dola nyingine zina watu kabila mia mbili na hamsini. Mifumo ambayo inatumika kule ni ya Majimbo kwa sababu mwafrika ana unyonge fulani.

Ikitumika unitary government na tumeshaona akitoka mtu kutoka huko mahali fulani kama hapa hapa kwetu, pia sisi twaweza kupata rai siku nyingine. Basi aweza kuteua maDC wote.60% ya maDC wakiwa ni kabila lake na sisi huwa hatupendi fujo, nyinyi ndio husema kwamba kule hufanya maandamano na nini. Sisi huwa hatupendi huwa twaumia lakini hatupendi fujo sisi. Sasa tunasema kuwa mfumo huu ambao tunaopendekeza ndio utakaowezesha sisi kama wakenya kuishi kwa amani, kwa mapenzi, kila mmoja akiwa na haki yake I karibu naye. Asante.

**Com. Swazuri:** Mama Fatuma atafuatiwa na mama Amina.

**Mrs. Fatuma:** Salaam aleikum warakba tulai ta Allah wabarakatu. Bismillahi rahman rahim. Naanza maoni yangu.

**Com. Swazuri:** Jina lako?

**Mrs. Fatuma:** Fatuma Mwanyuchi. Mimi nazungumza kama mama wa Kwale, mwenyekiti, member wa maendeleo ya wanawake Kwale district. Ombi langu, naomba serikali ama Katiba inayokuja na serikali ambayo itakayokuwa ni mpya ya Katiba hii tunayoitolea maoni, isiwe na uchoyo wowote mbali na vile sasa waBunge wanapokea laki tano, laki sita na kuna mambo mengine yanaharibika huku grassroots. Utetezi wangu ni akina mama. Naomba Katiba ijayo na imeshazungumza na akina mama wengine waliokuja hapa, kuongezewe wizara nyingine ya akina mama na watoto. Mfano kama ile iko Zanzibar.

Wizara hii itaanzia grassroots. Kutakuwa na councillor na mBunge, minister na PS. Basi wizara hiyo itakayoundwa hivyo, yule councillor ambaye anashughulikia mambo ya akina mama na watoto na ni mwanamke na ameungana na councillor yule mwingine na ameungana na mBunge yule mwingine, hawa akina mama hawatapata taabu wala hawatanyanyaswa kwa sababu

NGO nyingi zinaingia huko juu na wizara hizo eti zinasimamia maslahi ya akina mama na watoto.

Mfano kama AIDS na mambo ya poverty. Wizara ziko huko na maofficers wengine sijui children's officer, sijui nani lakini hizi pesa zinazotolewa na wafadhili hazifikii mama yule ambaye yuko grassroots anayepata taabu na watoto wake. Anayepata taabu na watoto mayatima ambao wazazi wao wamekumbwa na ukimwi. Hilo ni janga ambalo tumeliangalia sana na hao waBunge tunaowachagua sisi akina mama ambao 90%ni kura zetu sisi akina mama. Wakienda kule wanagandamizwa hata hawazungumzi mambo ya akina mama vilivyo.

Huyu mBunge mmoja wa tarafa hatoshi kwa sababu yeye pengine akipewa uaziri au minister, kukosa pengine hata hakupewa ataangalia mambo yake na maslahi yake ya watu wengine na familia yake. lakini hazungumzii akina mama. Kwa hivyo tunaomba MP, councillor, PS na ministers waanzie wizara yao mbali kama ile ya Zanzibar niliyokwenda iona. Kwa hakika akina mama hawana taabu nyingi. Ma-NGO yakiingia yanaingia kwa waziri. Zinaingia mpaka huko, halafu kabla hiyo wizara haijazungumziwa na hiyo Katiba kuundwa. Kuwe na shule kila location shule special za watoto mayatima na wale needy families. Kwa sababu hiyo misaada inayoambiwa inazungumziwa mambo ya mayatima sisi kina akina mama hatuioni kabisa. Halafu ombi langu lingine ni gender (jisia). Mila ya mduruma na mdigo, wakioana wana mapenzi mazuri sana lakini familia zingine huanza chuchuchu! Chochocho! Mpaka mama anajifikia aende kona halafu anafumaniwa. Akifumaniwa mama huyu anatozwa malu na akitozwa malu, haya zaenda kwa bwana. Lakini ikiwa ni gender ama jisia, tunaomba pia baba naye akifumaniwa atozwe malu. Atozwe malu, maanake huyu mama pia anasononeka na chombo chake. Mbona huyu ameniacha ameenda kutafuta mke mwingine na nimemfumania. Kwa hivyo naye pia yule mume atozwe malu. Sio mke saa zote malu malu a a! msitufanye biashara hapa.

Lingine, ni malipo haya ya Kadhi ya uzeeni. Malipo haya yanachelewa sana. unaweza kustaafu ukakaa mpaka ukafa hivyo hivyo, utapata fidia yako ya malipo ya Kadhi. Kwa hivyo ombi langu naomba Katiba mpya ikiwa pengine bado mwaka mmoja ama miezi sita nipewe kidogo kidogo angalau mwenyewe nikienda nitamaliza ile miradi yangu kabla sijafa, mbona hii malipo ya uzeeni ya wafanyi kazi yachelewa hivi? Katiba mpya ombi langu, tuanze kulipwa kabla ya ule mwaka haujamalizika. Halafu mwisho kabla hujaniambia bado dakika moja, mwisho naomba hivi, hawa machifu ikiwa hawatarudi wa mlolongo ni wa kufanyiwa interview na masub-chief hawa ni wafanyi kazi wa serikali kweli kweli kabisa. Basi ikiwa chief hashughulikii maendeleo ya akina mama huko kwa location, kuwe Katiba mpya iseme hao machief na ma-subchief wapewe ma-transfer kama ma-DO ili tupate ma-chief na masub-chief wengine ambao wana maendeleo waje watuendeleze sisi kwa ma-location. Asanteni.

**Mrs. Amina:** Mabwana Commissioners, mama kamishina mabibi na mabwana Hamjambo. Mimi ninazungumza, nawakilisha shirika la akina mama ninaloitwa national Commission on the status of women Kwale branch. Jina langu naitwa Amina Mwaronga.

Serikali- tumesema twataka serikali ya Majimbo na ikiwa haitafaulu kuwe kenya bara na kenya pwani. Rais akiwa mume, makamu wake awe mwanamke. Twataka kuwe na viti maalum vya uBunge vitakavyogombaniwa na akina mama. Yaani kule serikali ikipanga itenge viti maalum ambavyo akina mama watagombania wenyewe. Akina baba kule na akina mama nao wagombanie ili nasi tuende wengi kule Bunge.

Kuwe na wizara ya huduma za akina mama, watoto ambao wizara hiyo awe waziri wake ni mama vile vile. Madiwani wateule wawe ni akina mama wanaoangalia maslahi ya watoto, kina mama na walemavu. WaBunge ni waajiriwa wa raia. Kwa hivyo, mishahara yao ijadiliwe na raia. Wasiwe na ithini ya kupitisha mishahara wenyewe. Twataka president na makamu wake wasiwe na chama chochote ili kuepuka upendeleo. Ma-chief na manaibu wao wachaguliwe na raia.

Uraia- mtoto yeyote anayezaliwa na mkenya mke nchini ama nje ya nchi yeye awe mkenya. Mkenya yeyote ana haki ya kupata kitambulisho na pasi ya kusafiria bila masharti.

Bunge- waBunge waruhusiwe kwa kuchaguliwa kwa vikao viwili tu. Miaka mitano mitano hata kama anafanya mazuri ama mabaya aende nyumbani, mwingine naye aingie. Twataka uakilishi Bungeni uwe nusu kwa nusu, waume kwa wanawake.

Serikali za wilaya- mayor au mwenyekiti wa baraza achaguliwe na wananchi. sio kuwa wachaguliwe na hao ma-councillor wengine. Achaguliwe huko na wananchi. madiwani wawe na kiwango cha elimu ya kidato cha nne na kuendelea. Wakati wowote, mayor ama mwenyekiti au diwani yeyote akiwa na makosa afukuzwe apelekwe nyumbani, watu wachague mwingine.

Madiwani wateule waweko lakini wote wawe ni wanawake wa kuangalia maslahi na maendeleo ya akina mama, watoto na walemavu. Muundo wa utaratibu wa uchaguzi. Twataka utaratibu wa uchaguzi upangwe kwa namna ambayo itaruhusu kushiriki zaidi kwa wanawake katika Bunge au serikali za mitaa. Twataka viti zigawanywe nusu kwa nusu. Kuwe na viti vitakavyotengwa kwa makundi maalum kama akina mama, walemavu, watoto na vijana.

Uchaguzi wa uRais- madiwani na waBunge uwe tofauti tofauti. Hasa tulisema wakati wa kuwa watu wanachagua waBunge wawe na siku yao. Ma-councillor wawe na siku yao halafu na Rais vile vile awe na siku yake kwa sababu twahofia watu wetu hawakusoma sasa wakati wa uchaguzi wakifika pale, wanachagua tu. Mara jogoo! Jogoo mama anachagua lakini hajui amechagua wapi. Kwa hivyo kuwe na special day hawa ma-councillor siku yao waBunge na Rais vile vile.

Haki za makundi- tungependa jamii ya mahali pale na mtu binafsi kutoka mahali pale awe mtu wa kumiliki ardhi. Halafu wanaume na wanawake wawe na haki ya kurithi kisawa.

Mazingara na mali ya asili- inapasa kuwe na uwezo wa kuhakikisha utekelezaji sheria za uhifadhi wa mazingira na uwe chini ya serikali za mitaa. Serikali ya mitaa inaweza kumiliki mali ya asili.

Haki za binadamu- serikali ina wajibu wa kuelimisha watoto wa kenya bila kujali rangi, kabila ama maumbile, katika shule ya malezi mpaka chuo kikuu. Serikali iangalie maslahi ya wale watu wasio na kazi ili wasiwe wezi kwa hivyo wapatiwe allowance mtu ambaye hana kazi. Kila mtoto anayezaliwa apatiwe allowance ya kumwezesha kukua. Kila mkenya awe na haki ya kupata matibabu ya bure. Kila mkenya ana haki ya kuchangia maendeleo ya uchumi wa kenya. Asanteni sana.

**Com. Swazuri:** Asante sana mama. Munyole Tabu na atafuatiwa na Omari Saidi.

**Mr. Munyole:** Makamishina, mabibi na mabwana salaam aleikum. Mimi yangu ni mambo mawili tu. Kwanza ni mfumo wa maongozi. Mfumo wenyewe tunataka Majimbo. Pili, ni lugha ambayo tunataka ifundishwe katika kila jimbo. Tunapenda lugha ambayo tunataka ifundishwe katika nini kila jimbo. Tunapenda lugha ya mama ifundishwe kwa maskuli, kwa sababu nchi zile zimeendelea wanazungumza lugha zao na wanafundisha lugha zao mashule. Ndio sababu, from the word go mtoto anajua, anakuwa mwerevu kwa sababu anafundishwa lugha ya mama. Kwa mfano, hapa sasa hivi kuna wazee wengi ambao hawawezi kuzungumza Kiswahili ama kizungu wakifahamu hawawezi kuelezea vile ambavyo wanataka Katiba iundwe. Kwa hivyo sasa utakuta watu wengine wamekaa na hawawezi kuzungumza kwa sababu ni lugha zile zinafundishwa shule ni geni. Kwa mfano, kizungu.

**Com. Baraza:** I want to interrupt you. Kama hujui kizungu au Kiswahili uko na haki ya kusema mambo ya Katiba kwa lugha yako. Usikae hapo umeogopa kwa sababu hujui kizungu ama Kiswahili hiyo itakuwa ni makosa. Nilisahau kuwaeleza, ongea kwa kidigo, ongea kwa kichonyi, tutaelewa tu.

**Mr. Munyole:** Sasa mimi nataka kuongea kidigo. That one is very important because wengine hawakusoma kabisa. Sasa tunataka hii Katiba mpya itakayotungwa ya Majimbo wawe shule wanafundishwa kidigo. Hesabu mwanafunzi awe anaelezewa kidigo na masomo mengine. Hata sayansi iwe ni kidigo ndio mwanafunzi ataweza kukutana maprofesa wengi kuliko sasa. Kwa hayo machache asanteni.

**Mr. Omari Said:** Kamishina na wasikilizaji salaam aleikum. Mimi naitwa Omari Said Rua kutoka Gombeni location. Mwanzo nitazungumzia serikali na sitazungumza mambo marefu kwa sababu mengi yamepitiwa na wenzetu. Kitu cha kwanza, serikali tunayohitaji sasa ni serikali ya Majimbo na ziko sababu mbili ama tatu kwa nini tunahitaji serikali ya aina ya Majimbo. Sababu ya kwanza, serikali ya mfumo tulio nao imewaacha watu wa Pwaninyuma.

Imetuacha nyuma kimaendeleo, kiutajiri na kadhalika. Kwa upande wa ugawanyaji power, au ugawanyaji uwezo tunaona kwamba vitu vingi vimelemea juu. Kule kwa wenzetu tunaona ya kwamba upande wa maintenance wa vitu vya kimaendeleo kama barabara, utakuta hata chooni lami imefika huku lakini sisi barabara ambayo inaenda kwa DC kutoka wakati wa uhuru ilitiwa juzi. Kama hii yetu hapa. Kwa hivyo tunahitaji Majimbo ili ugawanyaji uwezo upatikane nasi tuweze kula matunda ya

uhuru.

**Com. Baraza:** Na kama ni serikali kuu ambayo inaangalia watu wa Pwanina maslahi yao. Wajua, serikali mbaya ndiyo inapeleka utajiri mahali pamoja na usifikirie kule mwingine iko kitu na hiyo serikali ni nzuri? Hiyo inapeleka mahali pamoja inasahau kwingine. Ikiwa ni serikali nzuri hata hiyo hamtaki au/

**Mr. Omari:** Kama ipi/

**Com. Baraza:** Kama ile barabara zetu inatengeneza, mahitaji yetu yanaangaliwa.

**Mr. Omari:** Lakini sio hii tuliyo nayo. Hii tuliyo nayo inayoendelea Katiba hii haifanyi hivyo.

**Com. Baraza:** Lakini sio Katiba ni serikali. Na serikali ikiwa mbaya ni mbaya.

**Mr. Omari:** Kwa hivyo hii ni mbaya. Haitufai. Hii haitufai, kwa hivyo tunahitaji ile ya Majimbo. Imagine mimi hata baiskeli sina na nimekaa karibu miaka ishirini. Pili, mimi nitazungumza kwa kifupi, upande wa ardhi, ardi zetu nyingi zimechukuliwa. Kwa hivyo Katiba hii mpya ijaribu iwezavyo irudishe ardhi hizo ambazo zimechukuliwa kinyume cha sheria kwa wananchi wa hapa pwani. Hapo nimemaliza.

Upande wa elimu- elimu inayoendelea pia inaendelea kimakosa. Serikali haienezi elimu kama inavyotakikana. Serikali hii ikijenga secondary school hapa, kule kwa wenzetu inajenga university. Serikali ikijenga hospitali hapa kule inajenga hospitali ya hali ya juu. Hapa imejenga dispensary sorry. Ikijenga dispensary hapa, kule inajenga hospitali. Huko kwa wenzetu. Tunapendelea equality yaani ugawanyaji uwezo.

**Com. Baraza:** Na kule ninatoka, natoka Western (magharibi), ushasikia mahospitali huko?

**Mr. Omari:** Mimi naona tumemaliza.

**Com. Baraza:** Hapana, bado. Wacha nikuambie, nikuelewana. Huko western hakuna shule, hakuna university, hakuna hospitali.

**Mr. Omari:** Western Province hiyo ni pamoja na magharibi, kakamega. Unaniambia hakuna dispensary mama? Ama hospitali? Kakamega? Wananchi hiyo ni kweli hiyo? Na ningependelea kamishina upande wa elimu ya 8-4-4, hiyo haifai kabisa kwa sababu ninavyoelewa skuli watoto wanaenda siku tano. Na kwa mfumo huu wa sasa, hizo siku tano hazitoshi mtoto ni lazima aende kwa tuition na bado hajui kusoma. Kwa hivyo tunapendelea mfumo ule wa zamani urejeshwe ili mtoto akifika seven, awe

anaweza kuzungumza kiingereza fluently.

**Bishop Kariuki:** Umesema ya kwamba yarudie wenyewe. Yaani yale yalinyakuliwa kutoka kwa wenyewe yaregeshwe. At least ningetaka useme yakirudi kwa wenyewe yasichukuliwe na governor yapewe wenyewe. Kwa sababu inaweza kurudi kwa governor, governor apatie watu wake.

**Mr. Omari:** Pia kwa kuongezea mfumo unaoendelea shamba iko gombeni lakini inagawanywa hapa kwa meza. Kwa hivyo ni watu wale wako gombeni wakae wajue hii shamba ni ya ukoo gani na itagawanywa ipewe nani? Wazee wa gombeni, ukoo mmoja unatoa maDC kumi na hapa DC mmoja hatoki, hiyo itakuwa sasa. Asante sana.

**Mr. Ngati:** Kwa majina naitwa Jackson Ngati, ni civic provider. Maoni yangu ni kuhusu, ninaonelea Katiba ipunguze uwezo na mamlaka ya Rais na pili kuwe na serikali ya Majimbo. Na kila jimbo liweze kutawalwa na mtu mweusi. Tatu Bunge liwe na uwezo wa kipimo. Nne, umri wa kugombea viti vya uRais na uBunge iwe miaka arobaini na tano mpaka hamsini.

Umri wa kugombea viti vya uRais na uBunge ni miaka arobaini na tano mpaka sitini na tano. Umri wa kupiga kura ni miaka kumi na minane na kuendelea. Sita, waBunge wafanye kazi kulingana na utaratibu wa wananchi wala sio wao.

Saba, marupurupu yatolewe kabisa ibaki mshahara pekee. / ya waBunge na madiwani maalum itolewe. Haki za binadamu – Katiba ilinde haki ya binadamu kwa kuwapatia maji safi, matibabu ya bure, shule ziwe hali ya juu na tuwe na barabara safi. Rasilimali- bandari, msitu, viwanda na mbuga za wanyama vitunufaishe sisi watu wa Pwanina hiyo inaweza kupata asilimia themanini.

Viwanda vyetu viweze kufufuliwa, hiyo ni ramisi, kilifi, kenya bidza na msambweni coconut development na tuwe na vifaa vya kisasa vya kulima na vya kunyunyizia mashamba yetu maji.

Ardhi- zisiuzwe bila kamati kukaa. Shamba za ukoo zisiuzwe. Kuwe na adhabu kwa wenye kuharibu mazingira. Lugha za kigeni zifundishwe kutoka primary school mpaka secondary school. Hiyo ni kizungu, kijerumani pia tuwe na computer ifundishwe pia. Ingine machifu wachaguliwe kwa muda wa miaka mitano. Hiyo ndio maoni yangu.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Mzee Kanda.

**Mr. Jasper:** Commissioners, ladies and gentlemen, distinguished guests, how are you? This is mzee Jasper, Kenya Society of the Physically Handicapped community based rehabilitation coordinator coast branch. I am here representing my views for disabled people.

I say, the constitution of kenya currently has marginalized the groups of disabled persons. Physically handicapped, visually impaired, hearing impaired, mentally at the age of 65% I now ask the coming constitution to consider these people and these are what I would to be put into. Education, starting from nursery schools, primary, secondary up to the up to the capable level should have special funds for these disabled children. These are in two groups. We have persons with disabilities and a child of a person with disability who is also to be considered by the constitution.

Also, should have equal opportunities for training. They are capable to go for training and then equal opportunities to job opportunities to every sector then we come to political basis. We need to have special seats separated in the political basis. Civic, parliamentary and presidential. According to these groups of mine should be five. Parliament five groups, five seats. I am still adding some. In percentage, we need at least 25% to be considered.

Also, these children because they are near to the mother's concept. A mother who brings up a disabled person should also be considered because he is the host of the disabled person.

Then, we have to have funds for bursaries which will cater the education of the disabled children. Then, we have these other access like transport. In via cause, when a disabled person is in this hear cause, there is a person which is capable but because he is called a big man you can see a disabled person with crashes. They ask to give a chair to a person who is capable of holding but him being taken out of the seat whereby he cannot stand the momentum of the movement of the object because he has no respect just because of his discrimination. So we are talking about discrimination is stability should be the first thing to be considered.

This discrimination should be considered from any type, race, colour, movement, liberty, freedom of talk and should cover all these. The rights which are here, the / and political rights, economic, social and cultural rights, people solidarate rights. These are things which should be considered to the disabled person and for this cause I say thank you.

**Com. Swazuri:** Thank you verry much and the next one is Peter Mtambo. Said Bakari.

**Mr. Bakari:** Bwana kamishina, bi. Kamishina, mabibi na mabwana. Nitazungumza machache sana kwa sababu naona mengi yameshazungumzwa. Kwa jina kamili naitwa Said Bakari Vombo, natoka Mwaluvanga location. Maoni yangu kulingana na Katiba tunayoiunda kwa muda huu nahitaji iwe ya Majimbo. Nahitaji iwe ya Majimbo. Majimbo wenzetu wakisikia habari za Majimbo huwa wana wasiwasi mkubwa tujuavyo nchi nyingi sina muundo wa Majimbo, na watu kabila zote zinaishi sehemu hizo. Kwa hivyo ndugu zetu ambao wanasikia wasiwasi, wasiwe na wasiwasi wakisikia kwamba tunahitaji Majimbo.

Majimbo malengo yetu ni kwamba, tuwe na serikali ya Majimbo tuwe na waziri mkuu, tuwe na Rais ili tuweze kupunguza ule uwezo mkubwa ulioko kwa wakati huu kwa sababu hivi sasa Rais yuko juu ya sheria. Kwa hivyo tunataka sheria iwe juu

badala ya Rais kuwa juu au waziri mkuu kuwa juu. Tunataka wote wawe chini, sheria iwe juu.

Jimbo, wakati wa kugawa mapato yake, jimbo libakishiwe 75% na 25% zipatiwe serikali kuu. Mishahara na marupurupu ya waBunge- naomba ombi langu ni kwamba wasikae wenyewe wakakata shauri kuwe na Tumendogo ambayo itaweza kukaa kuweza kukata shauri kuwapatia mishahara au marupurupu yao.

Uajiri wa machifu- uajiri wa machifu usiwe kama vile sasa. Uajiri wa machifu, wananchi waweze kuwachagua machifu na hatutaki machifu watoto kama vile wanavyoajiriwa sasa. Kutoka miaka miaka thelathini na tano mpaka arobaini. Hivi nimesema mengi yameshazungumzwa bwana kamishina na nilikuwa sina haja ya mambo mengi. Kama kuna swali ninaweza nikaulizwa kabla sijaondoka. Asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Kibwana na atafuatiwa na Omari.

**Mr. Kibwana:** Waheshimiwa Commissioners, mabwana waheshimiwa mliohudhuria, viongozi, mabwana na mabibi, salaam aleikum. Hapa yaliyozungumzwa Majimbo majority lakini neno moja nitawaambia, mimi nilikuwa diwani hapa miaka kumi na saba, tukapitisha by-laws lakini zilisumbua watu halafu tukazibadilisha. Hata nyinyi mtabadilisha maanake hayo mliyozungumza hayamfaulu, hayampati mwananchi.

Hii ni barua ya chairman / mwenyekiti Katiba ya kenya. Serikali ya kenya na Katiba yake iliuliza wananchi wa kenya ikiwa Katiba ya kenya ni mbaya mnataka vipi? Ama sivyo. Jibu kutoka kwangu na wengine tunasema tunataka watu wa Pwanikujitawala wenyewe kutoka Vanga, Lamu mpaka Taita Taveta. Sisi sio waasi serikali wala kujitenga kwa kikabila kwa sababu kuna sababu tatu nazo ni hizi. Kwanza umaskini, pili hofu, tatu uchaguzi. Kwa maelezo machache, umaskini tunateseka na njaa kwa sababu ya kukosa ardhi ya kutosha, ya kulima mashamba, kunyang'anywa mashamba yetu, kupewa idara za serikali, kupewa watu binafsi na watu watarudishwa mashamba yao na hakuna jina la masquatter tena walionunua ardhi sawasawa yaani self- seller and self-buyer watabaki na ardhi zao na serikali itawalinda.

Tunakufa kwa mahoma kwa sababu kukosa pesa za kwenda hospitali na kupata dawa za gharama ya juu. Watoto wetu wanafukuzwa shuleni mara kwa mara kwa kukosa pesa za kulipa karo. Kukija mtihani watoto wanapita, hawapiti mtihani vizuri wanaanguka.

Pili, hofu ni ndugu zetu wa bara baba kuua mtoto, mtoto kuua baba, mama kuua mtoto, mtoto kuua mama, bwana kuua bibi, bibi kuua bwana na ndugu kuuana. Na mtandio wa mapanga na bunduki kuuana. Kuibiana ng'ombe na umwagikaji wa damu wa daima. Dawa ni pwani, tunataka kuzuia mambo haya maovu yasije yakaenea kwa ajili ya umaskini kwa sababu Katiba ya kenya haina kifungu kimoja cha sheria cha kuondoa umaskini kwa umma.

Sisi vina, sauti ya umma tunacho kifungu cha sheria ya kuondoa umaskini kwa wananchi. sababu nyingine ni uchaguzi wa madiwani wa Bunge, uRais, kutoa pesa nyingi kwa wananchi ili wapigiwe kura.

Moja, kati ya wao na aliyeshinda anasema hakufanya race. Mwisho matokeo ni vita vya kikatili kuuana wao kwa wao. Sisi tukikubaliwa na serikali ya sauti ya umma hakuna utoaji wa makundi ya pesa kwa wananchi ambaye atachaguliwa kama diwani, Bunge ama Rais ila atachaguliwa atajichagua mwenyewe, yaani self- elections baada ya kupitishwa wazi na baraza ya umma katika location yake.

Usifanye shaka serikali ya sauti ya umma italinda kila mwananchi haki zake, mali zake na maisha yake. Hiyo ni fupi tu. Mimi nina Katiba hapa nataka kukupa lakini neno moja tu nauliza baada niondoke. Sasa hii Katiba sisi hatujafanya mabaraza kutosha na wananchi. Tunatoa hizi Katiba kwa ma-group ama vipande vipande na hiyo haifai. Tunataka tujue sauti za wananchi wanataka nini ama sivyo. Sisi hapa nauliza wale ambao wanataka kutawaliwa mpaka maisha ya kiama wainyoshe mikono juu. Na wale ambao wanataka tujitawale sisi wenyewe nasi tuwe wa bwana mkono juu.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Said.

**Mr. Said:** Waheshimiwa Commissioners, waheshimiwa ndugu zangu, salaam aleikum. Ni furaha kubwa sana kutafakari makosa yetu kama wakenya, kupitia kwa Katiba na kukubaliana kwamba kupitia kwa Katiba tunaweza kurekebisha. Mimi naitwa Omar Changoma, senior chief Mwaluvanga location.
Oni langu la kwanza ni kuhusu ardhi na nasema ya kwamba maswala yote ya ardhi, ikiwa ardhi ni chombo muhimu sana. Yatatuliwe na yaishie kwa ngazi ya kata. Cheo cha Commissioner of lands hakina maana, is irrelevant to land issue. Kwa hivyo kama tunataka kujirekebisha kweli maswala yote ya ardhi yaishie kwa ngazi ya kata that is a location. Labda kwa documentation inaweza kufanyiwa kwa wilaya. Kuhusu mambo ya serikali, mfumo nawaunga mkono wenzangu wanaosema mfumo wa Majimbo na ikiwa ni hivyo basi tunasema kila jimbo liwe na governor ambaye hatakuwa na chama chochote cha kisiasa.

Pwani ikiwa kutakuwa na vyama tutakosa governors wazuri wale ambao labda niwachia hawana pesa, wazungumzaji hawana mali. Kwa hivyo awe ni mtu ambaye hafungamani na chama chochote, hata naibu wake kama iko iwe namna hiyo. Huyo apiganie u-governor katika kila jimbo.

Kwa central government, president na vice wake pia wawe wenye watu ambao hawana vyama. Napendekeza pia waziri mkuu awe hana chama chochote anachowakilisha. Maoni yangu tu. Nikienda mbele kwa upande wa akina mama, najua wazee sana ndio wamebarikiwa sana kuwa na mali nyingi kushinda akina mama. Kwa hivyo nasema habari ya nomination iendelee lakini iendelee tu kwa akina mama. Kuwe na nominated councilors wa akina mama na kuwe na nominated MPs wa akina mama.

Tukifanya hivyo, tutapata akina mama wazuri wanaojua kuzungumza werevu lakini hawana mali za kununua watu kuwapigia kura. Nikiendelea mbele vyeo hivi ama viti hivi viwe kwa idadi. Kwa mfano, kwa upande wa u-councillor hapa kwa mfano hapa Kwale, kuwe na viti vitano, akina mama wawe nominated councilors.

Kwa upande wa MPs, jimbo lipewe viti vitano nominated MPs akina mama. Sikusahau vijana wale ambao ni werevu sana, wanaoweza kuzungumza, wanaoweza kutetea haki zao, pia nao wapewe nomination kwa serikali. Kama MPs na kama councilors. Nisije nikasahau pia upande wa mayor, sitazungumza mayors nao lazima wawe ni watu ambao hawa chama chochote. Wasiwe ni watu wenye vyama. Maoni yangu tu hayo. Nafikiri hiyo ni upande wa serikali.

Nikirudi upande wa rasilimali, nataka kusema hivi, sasa tunafahamu makosa yetu Katiba ile ya zamani tunayo na sasa twachangia Katiba mpya. Ikiwa tutakubali makosa yetu basi, ni kuangalia central government, sehemu zile ambazo labda ilipendelea na kuendeleza kama hiyo iko, basi sehemu hizo zilizopendelewa na kuendelezwa ikome hapo hapo. Na iangaliwe zile sehemu ambazo labda zilipuuzwa na hazukuendelezwa. Kwa hivyo nasema zile sehemu ambazo labda ziliachwa nyuma kwa sababu juu ya kwamba labda zilikosa minister wa sehemu hiyo na zina haki ya kuendeleza kama sehemu nyingine Central Governmentitumie rasilimali nyingi kuendeleza sehemu hizo ambazo zimesahauliwa.

Kwa upande wa rasilimali hivyo hivyo nasema hasa kwa upande wa bunga za wanyama wa pori, zile mbuga zinazopakana na ma-location, wananchi ambao ndio macho ya mbuga hizo, wawe watanufaika directly na mbuga hizo. Na kwa upande wa wanyama hawa wanaotisha maisha ya wananchi hasa ndovu, ikiwa ndovu amemwathiri mwanadamu au mimea yake basi Katiba hii mpya irudishe mara moja ridhaa kwa yule anayeathiriwa. Katiba hii mpya irudishe mara moja ridhaa kwa yule anayeathiriwa. Kama mtu ameuawa, mimi napendekeza watu wake walipwe milioni moja. Kwa mahindi basi itaangaliwa vizuri na wale wataalamu wa mimea.

Naam, nikiendelea kidogo tu nataka kusema kwamba habari ya ufisadi unaletwa sana na hizi kazi ambazo zinawaajiri tofauti. Napendekeza Katiba tunayoichangia sasa ipendekeze kwamba kila jimbo liwe na mwajiri mmoja. Wataalamu hawatashindwa kupatia jina ya mwajiri huyu badala ya kuwa ile ni parastatals, ile sijui ni nini, ile sijui ni nini, mimi nikiwa nafanya kazi sawa na huyo parastatals mshahara wangu ni yeye anapata pesa zaidi ya mara ishirini ya mshahara wangu na hiyo ndiyo ina-encourage corruption. Lakini tukiwa na mwajiri mmoja, yeye ndiye ataangalia mambo ya harmonization ya kila kitu wafanyi kazi katika hilo jimbo ama serikali kuu.

Hata waBunge wawe chini ya mwajiri huyo kwa sababu mBunge anachaguliwa na mwananchi na sioni kwa nini mBunge awe anafunga sheria tena awe yeye ndiye mtekelezaji, kwa sababu akisema anataka 200% salary tayari kesho anazipata. Inakuwa sasa yeye ndiye anatunga sheria, na yeye ndiye anaitekeleza. Yawezekana vipi? Kwa hivyo kuwe na mwajiri mmoja ambaye hata mBunge atamheshimu. Habari ya ma-parastatal ndiyo ina-encourage corruption. Kwa hayo machache, asante sana.

**Com. Swazuri:** Asante sana, nenda uandike pale. Na sasa ni Ngome Amani.

**Mrs. Ngome Amadi:** Wageni mliohudhuria salaam aleikum. Kwa jina naitwa Mwamtenda Ngome Amadi kutoka Gombeni. Maoni yangu kwanza, tungependekeza kuwa ofisi za maKadhi ziwe mpaka ngazi za kata, yaani kwenye ma-location. Hii ni kupunguza zile kesi za ndoa na talaka kusikizwa katika ofisi za ma-chief.

**Com. Baraza:** Rudia mama.

**Mrs. Amadi:** Ningependekeza kuwa ofisi za maKadhi ziwe mpaka ngazi za kata, yaani kwenyee ma-location ili zile kesi za ndoa na talaka zisisikizwe na ofisi za machifu. Pili, magawanyo ya makazi. Twapendekeza kuwa Rais akiwa mume mdogo awe mke, mayor akiwa mume, mdogo awe mke, chairman akiwa mume, mdogo awe mke, wazee wa mitaa wawe wake kwa waume, sio wanaume peke yao.

WaBunge maalum wawe wanawake na madiwani maalum wawe wanawake na madiwani maalum wawe wanawake. Pia twapendekeza kuwa katika milolongo ya serikali kama kwenye vitambulisho ama hospitali, wanawake wenye mimba kama mimi na wanawake wenyewe watoto wapewe nafasi ya kwanza.

Pia twapendekeza kuwa serikali iondoe ile hospital funds. Twapendekeza pia serikali iondoe ile hospital fund kwa wafanyaji kazi wote wa serikali kwa sababu utaona sisi tutatozwa pesa zile za hospitali na hatuna hospitali yoyote ambayo tunakwenda.

Pia, twapendekeza kuwa kuna haya mambo ya rape. Msichana aki-rapiwa na baba yake twapendekeza kuwa baba huyo afungwe milele. Na msichana wa shule au mvulana wa shule wakiwekana mimba hawa watoto wawili twapendekeza kwamba hawa watoto wapewe kifungo cha nje ili iwe funzo kwa wale watoto wengine. Watoto wawili wa shule yaani msichana na mvulana wakiwekana mimba twapendekeza sisi wazazi kuwa watoto wale wapewe kifungo cha nje ili iwe funzo kwa wale watoto wengine na pia ipunguze zinaa.

Kwa upande wa serikali za wilaya, tungependekeza kuwa wale wafanyi kazi wa serikali za wilaya, wapewe mishahara kulingana na standard of education, kwa sasa huwa wanapewa mshahara kulingana mwaka walioingia kazini na pia mshahara uongezwe kulingana na mwaka ambao aliingia kazini. Lakini sisi tungependekeza kama wale wafanyi kazi wengine wa serikali hata kwenye mabaraza ya wilaya, mishahara iwe inafuatilia standard of education. Ikiwa ni wa darasa la saba aangaliwe style yake ifuate ile ya form four au form six and above.

Upande wa madiwani na waBunge twapendekeza kuwa hawa watu hawana ofisi. Hatuwajui baada ya kuwachagua tuwafuate wapi. Twapendekeza kuwa kila mBunge kila diwani, mahali ambapo ana-represent ajenge ofisi yake.

Tukija upande wa wapigaji kura, tungependa hawa wapigaji kura wote wapige kura mahali walipozaliwa. Hii hupunguza ununuaji wa kura. Kuna wengine wana pesa kununua kura, wengine hawana na ni viongozi bora. Kwa hivyo kila mpigaji kura twapendelea Katiba hii, mpigaji kura apige kura katika mahali alipozaliwa.

Tukija kwa upande wa stakabadhi, tungependa kuwe na uwazi baina ya mwanamke na mume na watoto wake. Hii nikifafanua kuwa upande wa title deed mwanamume akinunua shamba majina matatus yaweko. La bwana, la bibi na la mtoto kama mtoto yuko kama hayuko, liwe la bwana na la bibi. Bibi akinunua shamba liwe la bwana na bibi.

Upande wa stakabadhi za kazi kuna mambo ya next of kin. Hii ijulikane kuwa bibi anajua yeye ni next of kin of bwanake. Na bwana naye ajue next of kin wa bibi yake. halafu kwenye malipo ya uzeeni, bibi lazima ajue kuwa incase bwanangu akufe mapema mimi ndio mrithi wa malipo ya uzeeni. Na bwana naye hali kadhalika ajue kuwa bibi yake pia ni next of kin. Kuna mabwana wengine huwa na bibi pale nyumbani na watoto lakini bibi hajui next of kin ni nani. Incase atakufa mapema kumbe next of kin wake ni mama yake. hatutaki Katiba ya sasa.

Upande wa urithi, twapendelea kuwa, mtoto anayezaliwa nje ya ndoa arithi mali ya mama yake lakini asirithi mali ya baba. Na mwanamke wa nje ya ndoa pia asirithi mali ya mume yule. Kwa hivyo ikiwa mmeamua hamtaoana mtakaa hivi hivi wewe mke baada ya mume akifa usirithi ile mali. Na ikiwa kutatokea mtoto ambaye alitokana na zinaa, asirithi mali ya yule baba, arithi mali ya mamake peke yake.

Nitamalizia upande wa utawala. Tungependelea la mwisho kuwa machifu tuwachague kwa mlolongo na pia wazee wa mitaa. Kwa hayo machache nasema asante.

**Com. Swazuri:** Tunamtaka mama Mwanarusi akifuatiwa na Zolo Muma awe tayari.

**Mrs. Mwanarusi:** (Arabic) Bismilahi Rahman Rahim. Salaam aleikum warakba tulai ta Allah wabarakatu. Mimi kwa jina naitwa Mwanarusi Rashid Indago kutoka Gombeni sublocation Gombeni location. Maoni yangu nasema muhimu nataka Majimbo na singetaka Majimbo ni kumiliki ardhi yangu kama mwananchi wa hapa Pwani ama mzaliwa. Nataka Majimbo kwa sababu ya ardhi nimiliki kutoka hapa niliposimama mpaka chini.

Nataka Majimbo nami nijisikie kwamba hapa pamezaliwa nani na nani mpaka ikafikia mimi. Ikiwa leo hii nimesimama hapa tu niko hapa hapa juu juu lakini chini ya ardhi kukipitika ni kitu sicho changu. Hiyo ndio sababu nikataka Majimbo nimiliki vilivyo Pwanikama mwananchi wa pwani.

Nikirudia hapo, nasema hivi, sisi twasema hatuna elimu. Twataka Majimbo lakini hatuna elimu. Hatuna elimu vipi.nikisema hapa pwani, diploma zimelala kwa mifuko, ma-pilot tunao. Wakati huo tulipata uhuru tulikuwa sisi hatuna elimu lakini sasa tunayo

elimu ya kutosha. Kwa hivyo ni lazima tupewe Majimbo yetu. Majimbo iliambiwa baada ya miaka mitano watu wawe na Majimbo au miaka kumi. Miaka kumi ilipokwisha mambo yakaharibika. Kwa hivyo sasa ni muhimu tupewe jimbo letu, wakataka wengi, wasitake wengi lakini sisi watu wa Pwanitunataka jimbo letu.

Hatukatai wageni kutoka nje ya sisi lakini kwa heshima, tusiogopane tuheshimiane, tupendane. Hizo nguzo nne nasema huko ziambiwe na zijulikane hizo nguzo nne. Kuna nguzo nne ya kwanza kupendana. Pili, ni kukutana hizo mziandike zieleweke ni sheria ya kenya itakayotungwa leo hapa.

Ya tatu, ni kukutana, ya nne, ni kuzungumza kama hivi kushauriana. Kama tulikuwa hatupendani hatungekutana, na kama hatukutani hatungekuwa hatushauriani, na kama hatushauriani, hatufanyi. Kufafanua hizo nguzo nne za Majimbo. Leo sisi tuko hapa twataka Majimbo tumiliki mali zetu bahari, mahoteli, kila kitu kilicho juu ya ardhi na ndani ya ardhi.

Narudi hapo kwenye machifu. Machifu wachaguliwe na wananchi wenyewe. Tena chief huyo awe aliposoma alipitia kama mwalimu, alitumia hiyo kazi ya jumuia. Asichukuliwe chifu amesoma tu analetwa hapo ndani. Wawe wametoka kwenye waalimu, sasa nataka huo uchifu lakini si awe alicheza mpira ama alikuwa mtu wa sarakasi kwa sababu alisoma kwa sababu alisoma aje ahudumu wananchi.

Chifu awe na umri wa miaka thelathini na tano mpaka hamsini atakuwa amechoka huyo chifu. Kwa sababu chifu naye pia achaguliwe na wananchi. ikiwa hatachaguliwa apewe transfer kama vile DO anavyopewa transfer akapate elimu kwa nchi nyingine, aje aongoze wananchi. mBunge naye huyo mBunge akichaguliwa awe na wenzake awajue wananchi ni akina nani walionichagua awajue wananchi walionichagua kwa sababu hao ndio matajiri zake na wafanye mikutano kujua wananchi wanataka nini. Asije akawa anangojea wakati wa kura ndio aone wananchi. Pia kwa upande wa akina mama. Akina mama wasinyanyaswe na mabwana. Wawe hiyo inaitwa hiyo kikundi. Lakini kikundi kiwe ni cha bwana na bibi kwanza, maendeleo yatoke mle ndani ya nyumba.

Urithi kwa bwana upatikane kwa bibi na watoto wake. Kwa mama hiari na kwa baba ni hiari. Bado, kuna kitu sijasema. Asichapwe makofi, achapwe kwa maneno tu, kwa maelewano. Kama nilikosa kuchapwa huko, akinichapa nitasikia lini.

Muhimu ni Majimbo, tupate Majimbo yetu, tusinyanyaswe, tusipigwe, tusikae mtu anasema naweka spare, hakuna spare nasema serikali hii isiwe na spare bwana nje. Ukimtongoza mume akitongoza bibi awe ana hakika atamuoa. Hii ndio inaletwa ukimwi, hii spare. Asante.

**Com. Swazuri:** Solomon Kuba. Atafuatiwa na Mohammed.

**Mr. Solomon:** Makamishina, wananchi wenzangu hamjambo. Maoni yangu niliyokuja kutoa hapa katika kuchangia Katiba

yetu mpya tungeomba mamlaka ya Rais yapunguzwe vilivyo kwa sababu hayo yamechangia umaskini mkubwa katika nchi nyingi. MaRais wapunguziwe uwezo na uwezo urejeshewe Bunge kwa sababu waBunge ni wateule wa wananchi na kwa hivyo maoni mengi na kazi nyingi za wananchi zinapitishwa kwa waBunge. WaBunge wapewe mamlaka ya kujitawala huru na uongozi wa Rais kwa sababu kama sasa Bunge letu linafanya kazi kidogo sana kwa sababu Rais mara kwa mara anaingilia kazi zao. Anapokuwa na harambee anawabeba waBunge, hawafanyi kazi ya wananchi. kwa hivyo Bunge lipewe uhuru kamili mbali na uongozi ule wa serikali zilizoko mamlakani.

Mahakama- kuna mahakama za wazee ambazo ambazo zinatumika zikiumia kutuchukua mzigo mkuu wa kuweka amani katika miji na mitaa lakini hazitambuliki kiserikali. Zinatambulika tu kijina. Tungeomba Katiba mpya ikumbuke hizi mahakama za wazee zilizoko manyumbani ziwalipe mshahara na kuwatambua kama mahakama zingine kubwa zilizoko mamlakani sasa.

**Com. Baraza:** Zinafanya kazi gani?

**Mr. Solomon:** Zinatatua matatizo ya ugonjwa wa jamii kama sasa unakuta ugomvi wa mipaka ya mashamba, ugomvi wa vita vya nyumbani vya mabibi na mabwana, visa kama vya utunganaji wa mimba wa watoto. Kesi nyingi kama hizi hutatuliwa na hao wazee lakini hawatambuliki. Na utakuta hata saa nyingine wanashtakiwa kwa mapolisi kwa mapolisi, wanatatizwa na wamepitishwa hukumu za kisawa na wananchi wanaishi kwa upendo. Kwa hivyo serikali hii inayokuja sasa tungependa iwatambue na itambue hizi mahakama.

Serikali za mitaa- tungependa mayor achaguliwe na wananchi na naibu wake kwa kipindi cha miaka minne. Awe alikuwa mzuri kupita kiasi, awe alitenda maovu lakini miaka minne ikiisha apishe mwenzake naye akiye ujuzi wake katika kuendeleza sehemu hiyo. Elimu- elimu ya wananchi tungependa elimu ya msingi hadi ya upili iwe ya bure. Ichangiwe na kuangaliwa na serikali katika hali zake zote. Kuanzia mavazi na mahitaji yote ya wanafunzi hadi viwango hivyo vya shule ya upili.

Kura ya maoni- tungependa wananchi wapewe mauwezo, mkuu wa kuchagua Rais kama hawajaridhika na maongozi yake hata kama amechaguliwa kwa kura nyingi lakini uongozi wake umeonekana haufai, wananchi wawe na uwezo wa kutoa kura ya imani, kuchagua ama kuamua uendelezaji wa kazi ya Rais huyo, mBunge na hata diwani.

Haki za ardhi- tungependa wakuu wa wilaya watolewe kama wenyekiti wa Tumehizi za ardhi kwa sababu mara nyingi wengi wamechangia kupoteza ardhi. Wao ndio wenye viti lakini utakuta mara nyingi ardhi nyingi zinatolewa kimagendo, nyingine zinatoa miradi ambayo haifanikiwi na ardhi zinapotea na wananchi wanateseka na kuitwa masquatter hali kuna ardhi zilizokuwako zikatumiwa kimakosa.

Mali ya asili- kama mfano madini na sehemu zingine kama bahari, mara nyingi zimekuwa zinatesa wananchi kwa sababu ya kuwa zimeingiliwa na serikali, zinafunguliwa miradi halafu mwananchi yule mzaliwa wa hapo sehemu hiyo anatengwa na serikali

na anakosa kunufaika na ile ardhi ambayo Mungu mwenyewe amemjalia kuzaliwa pale ili anufaike na mazingira yale aliyo nayo.

Kwa mfano kama madini utakuta viongozi wa kiserikali hata wakisiasa, utakuta mbinu nyingi za kuvuruga wananchi, kuondoa kisababu za hila kama sehemu wamegundua zina madini na kukosa kunufaika wale wananchi wazaliwa wa pale ambao Mungu mwenyewe amewajalia yale madini wanufaike. Kwa hivyo tungependa jamii zinazotoka sehemu zile ambazo zimegunduliwa madini na mali zingine za asili zifaidi wale wale watu.

Serikali ichukue kodi kama inataka lakini isiwakoseshe wale haki zao ambazo Mungu amewabarikia. Kwa hivyo kama dakika imebakia hapo nashukuru na hayo machache, asanteni sana.

**Com. Swazuri:** Asanteni sana. Mohammed sheikh. Atafuatiwa na Fatuma Mwamakeba.

**Mr. Mohammed:** Commissioners na wananchi wapendwa salaam aleikum. Nashukuru kupata hali kama hii ya kuelezea katika mchango wa katiba. Wenzangu ambao wamepitia wameelezea mengi na nimeyaunga mkono yote yale ambayo kwamba yamepita. Nami pia nina machache yangu ambayo ninaweza kuchangia ndani yake na kisha baadaye mengi sana nitayatoa kule kwa ajili ya maelezo ya ziada.

Katika upande wangu naingia kwanza katika upande wa ma-chief Kadhi. Mamlaka yao yazidishwe. Badala ya kuhukumu tu ndoa na talaka, waweke katika mamlaka yao yawe na uwezo zaidi. Ikiwa kuna mtu masalani ni mwislamu na ameua mwenzake kwa kusudia, jambo hilo ndani ya dini linapatikana hukumu zake. Ikiwa ameua kwa kusudia katika kiserikali lazima ipitishwe hukumu na hukumu hiyo inaafikiana na Kadhi katika mamlaka ya kidini, basi arejeshwe mwenyewe Kadhi ili mambo haya yawe yanaweza waislamu nao kujihumudu. Kuwe na mahakama hizo ziada ambazo zitakuwa mahakama hizi zitahukumu sisi ambao kwamba tuna imani kama za dini. Malasani katika ukubwa kabisa kuhusu habari ya mambo mengi yameelezewa kama urithi na mengineo. Ndani ya dini yameelezwa kwa wingi sana lakini mpaka dakika hii nastaajabu ikiwa akina mama wanasema ya kuwa urithi uwe sawasawa ndani ya (a) ama ndani ya vitabu vya Mwenyezi Mungu vimeeleza urithi wa akina mama. Sasa jambo kama hili ndilo ambalo kwamba linalotuletea katika hali ambayo sio.

Pili ninaingia katika upande wa elimu. Elimu, sababu yote ya kuona mambo haya ya kuwa kwmaba sisi tunahitajia mambo ya urathi, yaani tuwe sawasawa katika waume na wake, haya yote ni kwa sababu ya elimu ya taaluma ya dini haijawa katika sehemu zetu na sababu hiyo serikali iliachana na kuna mambo ya elimu ya kidini na ambayo mambo haya yangelikuwa lau kama kungelikuwa na ajira ya kuwalipa katika masomo ya dini na ndivyo inavyohitajia katika Katiba hii iwakilishwe, Katiba hii ipitishwe ya kuwa masomo ya dini katika ukristo, katika uislamu, katika dini hizo na ikiwa kuna nyinginezo ambazo zitakubalikana katika kisheria, serikali pia nayo isimamie katika ajira hizo, elimu hizo zifundishwe, ili watu wajue sheria za dini yao katika hukumu aina mbali mbali kwa sababu ninaona katika kuangalia kwangu kumekuwa na upungufu wa hali ni kama hiyo na hayo mambo yote yameelezwa ndani ya Korani hata katika biblia.

Na katika mahakama ya Katiba napendelea katika Katiba hii kuwa na mahakama ya Katiba kwa sababu councillor hatumtaki sisi au mBunge hatumtaki tutaenda wapi. Pale ambapo kwamba tutaende kumshtaki ni wapi ili tumrejeshe nyumbani maana Katiba inatueleza hivi. Kwa hivyo mahakama ya Katiba iwekwe ambayo itaongoza nchi taasisi iongoze jimbo na katika afisi zije mpaka katika ma-location. Ikiwa watu wa location ile councillor wao hawamtaki, moja kwa moja waenda ku-file kesi katika ofisi yao ya mahakama. Hiyo ndio itakayokuwa jinsi ya councillor kumrudisha nyumbani lakini ikiwa tutaimba tu lakini mahakama hayo hakuna tutakuwa hatutafanya lolote. Kwa hivyo ninaunga mkono katika kuiunda Katiba hii mchango wangu kuwe na mahakama ya Katiba ili tufafanushie wale ambao kwamba hatuwapendi na tuwarejeshe katika uongozi wao haufai basi tuwe tunawarejesha nyumbani kwa usalama na urahisi.

Kisha naingilia katika ukosefu wa masoko katika pwani, hasa katika jumla hii nachangia wale wenzangu ambao wamesema Majimbo. Hivi mabwana makamishina, tukishuka hapa chini mabarabarani ikiwa twaelekea Mombasa, hapo barabara kuwe na mlima. Pana majengo ambayo yalikuwa yajengwe sijui mitambo ya korosho, kuna majengo sehemu zingine ambayo ilikuwa ni miwa, kuna majengo mengi ambayo ni yamepatikaniwa katika wakati wa ukoloni huko. Mengine ni wakati huu wa serikali ambayo tunayo lakini mpaka dakika hii hakuna lolote.

Tukiangalia kuna maua tu, pareto. Nayo pia yana masoko na hali nyingi kubwa kabisa huko. Ndio maana wenzangu wamechangia Majimbo na mimi ninachangia Majimbo kwa sababu Pwani imerushwa mno. Sehemu ambazo kwamba tulikuwa tusomeshewe sisi, umri huu nilio nao either kama lau kama sukari ingekuwapo, bigza ingekuwapo na viwanda vinginevyo. Nisingelishilia kwenda darasa la nane au darasa la form four, ningelikuwa ninapiga hatua zaidi lakini sababu ya kuwa umaskini umepatikana pwani. Serikali iliyopo ilituacha kabisa kabisa mpaka zile rasilimali za kuleta pato la kuweza kutusomesha sisi pia wakabwaga kabisa ili Pwani awe ni mtu wa kuongozwa milele kama alivyosema mwenzangu aliyepita.

Naingia katika elimu ya dunia. Ndio sababu iliyopatikana sisi mpaka dakika niliyoingia hapa makamishina anawaambia ya kwamba tuwe sisi tunapawa Majimbo yetu kwa sababu rasilimali kubwa ya kenya hii inatoka katika sehemu ya Pwanilakini mpaka dakika hii tunaangalia university hatuna national school hatuna, training colleges kwa aina mbali mbali tumeachiwa tu kiji-training college cha ualimu kile kitatufanya nini.

Yaani watu wa Pwaniwaende hapo wakasomee huo u-teacher tu lakini udaktari hatuna, utalii hatuna, kila jambo hatuna ila uwe unaenda huko huko juu na huko juu nako mpaka ukafanye kuangaliwa huyo ni nani, ni Joseph Maitha, ni Joseph nani lakini ikiwa ni Bakari Hamisi, mtu huyo anawekwa kando. Tumekuja hapa kuitunga katiba, ama katika maelezo yake. Naendelea kuwaelezea, usaidizi wa wazee wetu wazee ambao kwamba either wawe wahuduma wa kuhudumu katika serikali. Wana miaka sitini sabini hawana sehemu za chumo. Serikali iangalie. Wapewe chumo hao.

Na vile vile, wazee wa vijiji, machairman village, hawa watu wana kazi kubwa. Chairman village anamshinda Rais, chairman

village anamshinda mBunge, chairman village anamshinda chifu, lau kama Rais anataka kila siku ajue mgonjwa aliye, mtu ambaye ameamka na ugonjwa siku ya leo hapa kwale anampata na anaona village chairman. Kwa hivyo village chairman alipwe mshahara wale waBunge walipitisha ya kwamba asilipwe lakini naona kidogo hao wametupoteza.

Kwa hivyo, nilikuwa na mengi kidogo machache machache lakini kwa kulingana na wakati na ni muhimu sana kwa hivyo inshallah tutakutana wakati mwingeneo. Na kumalizia ni kwamba hii Tumeimetupoteza sana maana yote yamezungumzwa lakini hii Katiba haikupitishwa kule. Haikuletwa watu wakatufundisha mpaka sisi wengine labda ni siku tano tu ndio tunapata mambo ya katiba.

**Com. Swazuri:** Hiyo makosa ni ya providers ambao tulikuwa nao na hawa hawakufanya kazi yao. Fatuma aje hapa.

**Mrs. Fatuma:** Bi kamishina na bwana kamishina mabibi na mabwana, salaam aleikum. Hii ni Katiba ya / kutoka Tiwi location. Jina langu naitwa Fatuma Rashid Mwamachache. Mwanzo twataka Majimbo, tuwe na jimbo letu ili uwezo wa Rais upunguzwe, asiwe na uwezo wa kuchagua viongozi peke yake. Rais apewe miaka miwili, term mbili za kuongoza iwapo atakuwa haendeshi vizuri kabla ya miaka yake kuisha, kupigiwa kura ya maoni ili aondolewe mamlakani.

Twataka wanawake asilimia ishirini wawe nominated councilors. Halafu asilimia arobaini ya wanawake waende Bunge. Ardhi zipewe wananchi wa hapa hapa mjini. Asilimia themanini na tano ya wafanyi kazi wawe wa sehemu hiyo. Kodi zibakie na county council. Shule za upili tuachiwe fee peke yake na watoto wasifukuzwe manyumbani.

Huduma za hospitali ziwe za bure kwa sababu hali zetu ni dhaifu kwa hiyo wananchi wengi wanajifia kiholela. Watu walemavu wapewe haki sawa na watu wengine. Mfano kwa usafiri au kwa makazi sawa na wale watu wa kawaida.

Passport zipatikane kwa bei nafuu na kwa njia rahisi. Msichana akiolewa na mgeni yeyote watoto wake wawe raia wa kenya. Wazee wa kijiji walipwe mshahara na iwapo wanaume wetu wakinajisi wasichana wetu wa shule wahukumiwe kifungo cha kifo na tungependa hukumu kama hizi zipewe majaji wanawake.

Maternity leave kwa wanawake tungependa ianze ile siku atakapojifungua mtoto wala si kujaza form kabla hajajua atajifungua lini. Nafikiri mengi yamesemwa kwa hivyo itakuwa ni kazi ya kurudiarudia na kupoteza wakati. Kwa hayo machache nasema asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante mama Fatuma. Rehema na atafuatiwa na Juma.

**Mrs. Rehema:** Salaam aleikum. Kwa jina naitwa Rehema Matemo ni chairlady wa kikundi cha women group. Kwa chango, sisi wananchi wa hapa mambo mengi yameshazungumzwa tukasikizana nayo yote lakini tuna matatizo kidogo. Kwa sababu

hapa tunapenda wageni ambao wameingia hapa kwetu Pwanilakini wakiingia hapa kwetu pwani, sisi wazaliwa wa hapa Pwanihuwa hatupati mamlaka ya kuzungumza.

Kama kiongozi yule ambaye utampatia kura unasema huyu nikimpatia huyu sitapata mamlaka lakini huwa hawapati ruhusa katika ofisi yeyote kuzungumza mambo ya wananchi nyumbani. Kwa hivyo sisi sikitiko kubwa sana zaidi, ni mwananchi wa hapa tupate Majimbo angalau furaha nasi tupate kidogo kwa sababu hapa kuna misitu, hapa pana mahoteli, tuko nayo hapa. Hatujui ile pesa yaenda wapi kwanza. Tuko hapa tu. Kuna chairman wa location, huyo chairman mambo yote anapelekea serikali lakini anasemekana eti chairman hawezi kupata mshahara. Mimi napendekeza pia, apate mshahara wake kwa sababu yule ndiye anayejua shida zote za mwananchi wa hapa location. Kwa hivyo hayo machache Mungu ambariki.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Juma:** Bi kamishina, akina baba, ndugu zangu, akina mama na nyote mliohudhuria.Yasumbua watu, wakati wote ashikwe mguu kupandishwa kwenye ngazi. Kwa hivyo tunaomba hiyo isiweko. Iwe mlemavu ikiwa ame-qualify mahali popote aweze kuwekwa mahali pale.

Upande wa afya- mlemavu kwanza ni mtu wa kwanza ambaye yeye upande wa kazi si rahisi, kwa sababu yeye kwanza alinyimwa elimu na mzazi wake akiambiwa hatembei. Sasa alipoambiwa hatembei akaambiwa huyu kwa vile hatembei wacha akae hata asisome, kazi utakuta tayari yeye hana. Kwa hivyo katika upande wa afya, mlemavu yeye hana pesa. Pawe na njia maalum ya wale wafanyi kazi wa serikali katika ofisi zote za elimu ya afya wahakikishe mlemavu anapata matibabu bila matatizo yoyote. Bila kuulizwa pesa kwa sababu yeye atakuwa hana uwezo. Yeye mwenyewe kama hana uwezo pia mtoto wake aweze kutibiwa.

Ikiwa yeye hana uwezo iwe mpaka mtoto wake anaweza kusaidika pia kielimu kwa sababu tunasema kuna bursaries zinatolewa lakini kusema kweli hivi sasa bursary hizo zinaenda kwa ma-chief, maDO, mapolisi na wakuu wa idara, lakini yule ambaye anahitaji usaidizi kama huo hapati. Kwa hivyo sheria kama hiyo iwekwe kuwe na pesa maalum za watu kama hao waweze kupewa elimu.

Upande wa uongozi- kuna kamati ndogo ndogo ambazo zinaundwa katika kila wilaya. Utakuta kwamba kuna DC wako na yao ya development katika district, katika division, utakuta kunawekwa representative ya mlemavu ambapo mlemavu mwenyewe yuko, hausishwi. Kwa hivyo tunaomba katika sehemu hizo, walemavu wenyewe wahusishwe. Hakuna habari ya representative kwa sababu ikiwa wewe shida unayo. Ukienda pale utakwenda represent kitu gani ikiwa mimi mwenyewe ndiye najua shida zangu. Awe yule yule mlemavu iwe ni kipofu, awe ni bubu na awe mtu mwenye physically disabled. Lakini awe pale badili ya kuwa akawe representative.

Katika hizi uongozi iwe vile vile. Tunaomba nafasi ya Bunge, walemavu watengewe nafasi zao asilimia kumi na tano. Iwe ni special ya walemavu. Katika council, asilimia kumi iwe ya walemavu kwa sababu tukisema kuwa eti pengine tungojee nomination, kulingana na iendavyo, huenda ikaja mpaka hii nominated ikawa imekatwa. Utakuta mlemavu amewekwa nje. Na kama amewekwa nje itakuwa yeye hakuna lolote analofanya kwenye serikali. Katika mikutano yote ambayo inapangwa ya kiserikali, mlemavu ahusishwe pale kwa sababu utakuta mikutano mingi lakini ikiwa sheria iko, kila division, kila chief atahusisha walemavu walio kwenye location zake ama division yake.

Pia ningeomba katika mijadala mingi ambayo inaendelea, upande wa akina mama ijapokuwa hutajwa akina mama tukaambiwa pia sisi walemavu tuTumehuku upande wa akina mama. Lakini ujue pia walemavu wako pia akina baba. Tungeomba hao nao pia waweze kutengewa fursa zao kwa upande wa kipato kwa sababu kama hana kazi na hana shillingi yeye atategemea nini? Kupangwe angalau allowances fulani za walemavu waweze kujitegemea badala ya kutegemea omba omba.

Ningeomba pia humu majumbani. Narudi chini upande wa elimu kuwe na sheria sasa ambayo itawafanya wazazi walazimishwe kupeleka watoto wao walemavu shule kwa sababu hiyo iko kwa watoto wote lakini haikusisitizwa kwa walemavu kwa sababu kama hivi sasa mtu akipeleka mtoto wake wa kawaida kama hakumpeleka shule utakuta yuashughulikiwa alazimishwa ampeleke lakini mtoto mlemavu hashughulikiwi kabisa. Kwa hivyo naomba hiyo fursa ipatikane ya mtoto mlemavu kutoka kwa ma-chief wenyewe wazee wa vijiji wawe watachukua hiyo nafasi mtoto wa mlemavu apate kwenda shule. Asanteni.

**Com. Baraza:** Asante bwana Juma. Nimeelewa maneno yako na tutayapeleka kule. Taithi Mwachimonje.

**Mr. Mwachimonje:** Mimi nimefika hapa kwa maneno kidogo tu lakini ambayo ni mengi. Jambo la kwanza ninasema kuwa tunataka ile serikali inayoitwa Majimbo. Kwa hivyo kwa kuwa watu wengi wameeleza, mimi ni kutaja tu hilo jina na mengine yameendelezwa mbele. Kitu ambacho kimenileta hapa nimeomba hii Commission iweke sheria ambayo itatunga Commission wakati ujao, PC awe anachaguliwa na Commission badala ya kuandikwa ni Rais. DC awe anaajiriwa na Commission na DO awe anaajiriwa na mission.

Jambo lingine nimekuja hapa kusema hivi, wakati ujao, hii Commission iweke sheria hivi, msitu ya forest. Forest tangu zamani ilikuwa misitu yetu na ikachukuliwa na serikali eti italindwa lakini kufikia sasa, misitu hiyo forest sasa zime-jam inachezewa na ndovu. Sasa kile kitu tunataka Katiba ijayo itunge Katiba kuchukua hii misitu ya forest irudishwe kwa wenyewe wa kawaida misitu yao. Kwa sababu ikiendelea kukaa hivyo kutakuja kuwa na uwezo wa serikali kugawa misitu ile kwa watu wengine. Kwa hivyo tunataka hiyo msitu turudishiwe wenyewe.

Namba nyingine inasema hivi, hawa ndovu ni wanyama wa serikali. Ndovu hawa wametutia umaskini mwingi sana na wasiwasi mwingi hata kama wengine tuko hapa, tuna woga wa kwenda nyumbani jioni sana, unaweza kukutana naye. Kitu ambacho nimekuja kuomba Commission hii, ipitishe sheria katika ndovu hawa watengwe sehemu zile zenye na watu wapelekwa katika

national park zao mbali na wananchi. Kwa hivi sasa ndovu hawa wamerudi tunaishi nao. Mimi niko hapa, pale analisha nyasi nikimwona tu na jioni niko kwangu.

**Com. baraza:** Hakuna seng'eng'e?

**Mr. Mwachimonje:** Hata seng'eng'e sasa wale watu wa ndovu wameleta ujanja ambao usioeleweka, wanaweka seng'eng'e ndovu akija akigusa seng'eng'e unaanguka ndovu anapita juu. Kwa hivyo ni kuonyesha mchungaji akiona mahindi anasema ni mazuri sana kwa ng'ombe zake na hao watu wa wanyama wakiona msitu wanataka wavunje waje kule kwetu. Jambo jingine ni la Rais. Rais asiwe na uwezo zaidi ya watu wengine kwa sababu Mwenyezi Mungu tu ndiye ambaye ni mkubwa kuliko watu wengine wala si binadamu. Jambo jingine tena ni yameshazungumzwa lakini nitatilia nguvu, jambo jingine ni chief achaguliwe na wananchi na awe na umri wa miaka arobaini wala asiandike application eti amepita mitihani na sisi hatumjui vile alivyo. Sisi wenyewe kwa majumbani, ndio tujue ni nani anafaa kuwa chief. Kwa hivyo bi. Kamishina sina zaidi ya hayo, nimemaliza yangu.

**Com. Baraza:** Nenda u-sign hapo na kama umeandika maelezo yako unaweza kutuachia. Mwanakombo Mkoma.

**Mrs. Mwanakombo:** Bi. Kamishina, mabibi na mabwana, salaam aleikum. Mimi sina mambo mengi sana kwa sababu mengi yamezungumzwa lakini ni kutia mkazo na kusisitiza hasa kuhusu jambo la elimu. Elimu yenyewe ama kusomesha baada ya kusomesha hadi mtoto kufikia darasa la nane hasa hapa pwani. Huwa kupatikana mtoto ambaye amefuzu zaidi huwa ni shida sana na sio kuwa ya kwamba watu hawasomi ama hakuna waalimu wa kusoma lakini nafikiri ama tukizingatia sana ni kwa sababu marking ya mtihani kule huwa ni kwa sababu labda ile equality hakuna ya kuwa baadhi ya wale walio-mark zile examination huwa wako busy sana huko juu.

Kwa hivyo ningeomba ama kusisitiza ya kwamba kila district iwe itawakilishwa na na watu kama wanane kwenda kwa marking kwa mitihani yote kama ni KCPE, kama ni KCSE, wawe wote wanawakilisha district zao. Watu wanane, ningeomba hivyo. Halafu tupate college mbili hapa na university moja, utalii college kwa sababu mambo ya utalii sana yako hapa pwani. Utalii college iwe inajengwa hapa na course iwe inafanywa hapa, na idadi kubwa ya wafanyaji kazi ambao watakuwa ni hao wanaofanya huko mahotelini iwe inatokana hapa, at least 75%.

Halafu tukija kwa university, utakuta hasa watu wa hapa Pwani ama watoto wa hapa Pwaniwanapopita kuchukuliwa kwa university wataenda lakini wanapofika kule mtu ame-pass sciences lakini utakuta kitu kule uchaguzi unaofanyika ameenda kupita sciences lakini anapatiwa arts ambayo kwa ile mambo ya arts hakuna hata hasa kuajiriwa sana. yeye ameenda kwa sababu amepita sciences lakini ikifika kule utakuta kuna ule uchaguzi ya kuwa kuna watu asilimia wanaotakikana kwa pale hasa atachaguliwa yale yanayohitajikana lakini mtu anayetoka Pwani anaambiwa wewe utakwenda kwa arts ambapo hilo..

**Com. Baraza:** Akitoka hapa hajui anaenda kwa bachelor gani?

**Mrs. Mwanakombo:** Hata kama anajua lakini kule si kutakuwa kuna selection na katika selection ni nani ako pale ambaye atakuwa anawakilisha kwa upande wa huku jimbo la pwani? Hakuna. Kwa hivyo hapo tayari pana hitilafu.

Halafu katika hizi ma-college, training zote kama za ma-institute za nurses, utakuta pia kuna huo uchache wa watu wa Pwani ambao wako trained hapo. Utakuta hiyo training idadi kidogo tu ya kama 45% ambao wako hapo ni watu wa Pwanilakini idadi nyingi ni ya watu ambao wanatoka juu. Kwa hivyo pia katika hiyo serikali nayo itilie maanani igawanye, itoe equality. Kama kila district ni 10%, 10% ya kila district katika kenya iwe inawakilishwa hivyo. Sio wengine wanakuja wengi, wengine wanakuwa wachache. Kwa hayo machache bi. Kamishina asante sana.

**Com. Baraza:** Rashid Hamisi Mwakungu.

**Mr. Mwakungu:** Bi. Kamishina, mimi kwa jina naitwa Rashid Hamisi Mwakungu. Mimi ni chairman wa vijana wa location. Mimi niko na maombi matatu kwa Katiba hii. Swala langu la kwanza linasema katika ugawanyaji wa mashamba uliogawanywa mwaka tisini na tatu, haukugawanywa vizuri kwa sababu wakati wa nyuma ugawanyaji wa mashamba ulikuwa unagawanywa kwa machifu lakini hii ndio unaona katika Waa location sisi tumekuwa na taabu ya mashamba. Mashamba yetu yamegawanywa katika kwenye meza, hakuna chief, hakuna chairman, hakuna village chairman. Kwa hivyo tungeiomba Katiba hii katika ugawanyaji wa mashamba, kuhusishwe chifu kama vile zamani.

Kwa sababu serikali inayokuja ni serikali ya Majimbo. Serikali ile iliyofanya vile tuko na harakati ya kuitoa. Kwa hivyo kama tuko na harakati ya kuitoa iwe ni serikali ya Majimbo tunataka katika ugawanyaji wa mashamba iregeshwe vile vile, sio councillor kuwe kuna chief, kama ni hapo kwa DC kuwe kuna chairman, kuwe kuna village chairman. Kwa sababu wakati wa nyuma, unakuta shamba inagawanywa, kuna councillor pale. Hakuna chifu, councillor atafanya anavyotaka kwa sababu yeye ni mtu aliyechaguliwa na watu, hata kama ni watoto wake sita wote atawaandika. Hii ndio unaona sisi tuko na shida mpaka dakika hii. Matuga scheme ilivyogawanywa iligawanywa makosa mpaka sisi vijana tunalia hatujui mtu ako na watoto sita, utalima wapi, utaanzia wapi wala uende wapi.

Kwa sasa hivi tuko na shamba yetu ya minazi inasemekana itatoka. Mimi kama kijana ama kama maanake si kijana hivyo niko na miaka thelathini na sita, nimechaguliwa na wenzangu ni chairman, tunasema hakuna mdigo wa Kwale district ambaye ako na shamba bara lakini watu wa bara wako na mashamba hapa. katika ugawanyaji wa mashamba utakaokuja na serikali ya Majimbo hatutaki mtu wa kutoka nje ya Pwani au nje ya Kwale apate ardhi hapa. ikiwa mimi nina watoto sita, shamba yangu imepatiwa mtu kutoka juu na sijaona mdigo ambaye ako na shamba Nyahururu wala kirinyaga.

Kwa hivyo kama Katiba hii ya sasa ama serikali hiyo inayokuja itakuwa ni ya Majimbo, tunaiomba iweze kufuata mambo ya watu wenyewe wanavyotaka. Na kama ni mashamba, yasigawanywe pale kwa DC kwa sababu DC ametumwa na serikali aje

atumikie wananchi. DC hajakuwa na uwezo achukue ndugu yake kutoka nje amgawanyie shamba hapa. makosa yale ya kuwa councillor anakuwa pale na mjumbe ndio sababu anawacha haki ya mtu wa Kwale inakwenda bara kwa sababu yeye anajipendekeza kisiasa. Kwa hivyo Katiba hii tunaichangia kwamba hatutaki councillor wala mjumbe ahusishwe kwenye meza ya DC pale ugawanyaji wa mashamba hiyo hatutaki. Tunataka chief ndio anajua uchungu wa location na village chairman, na chairman.

Halafu sisi ni waislamu, sisi watu wa Kwale ama sisi watu wa Waa. Ni makosa makubwa sana katika mwezi wa Ramadhani wetu wa kujivunia tunakwenda kwa swala ama tumetoka kwa swala ama tuko na kawaida yetu. Wakati wa saa kumi ukifika umeenda kwenye mkahawa umepumzika unacheza karata mapolisi wanakuja kutunyanyasa ambapo hiyo mkristo anafanya matanga yake pale atakunywa tembo, atapiga madansi, hasumbuliwi. Kwa hivyo kama Katiba hii ni kweli leo twairekebisha ama serikali itakayokuja ni ya Majimbo sisi kama waislamu tuko na kawaida zetu. Mwezi wa ramadhani ukifika hatutaki polisi watunyanyase. Na wakati wa nyuma polisi walikuwa wanafanya kazi vizuri kwa sababu ulikuwa unafanya kazi kutoka kwa ofisi ya chief. Saa hii polisi hawawezi kufanya kazi kulingana na ofisi ya chief. Polisi watakuja tu na gari yao, mama yule ametengeneza mahamri yake amekuja yauza lakini pia mama yule hatauza mahamri yake vizuri. Kwa sababu watu wamefukuzwa, samaki watamwagika, mahamri yatamwagika. Kwa nini hawa polisi kama wanajua,

kwa nini wasifike ofisi ya chief wakamwambia chief sisi tumekuja tuna-report tunataka mtoto fulani, wanaleta ma-landrover, ule sasa ni mtego wa panya. Ule ni mtego wa panya. Kila ambaye hahusiki anashikwa, kutoka kule ni vigumu. Utatoka na elfu kumi. Ziko wapi? Kama mimi ni kijana wa umri wa miaka thelathini na sita sijakuwa na kibarua. Ndugu yangu ameshikwa, hizo elfu thelathini ama kumi nitatoa wapi nikamchukue kule. Tunataka tuachwe free mwezi wa ramadhani. Kama kweli watu wanarekebisha Katiba serikali ile nyingine yaondoka, ijayo ni ya Majimbo. Kwanza nataka Majimbo, pili tuachwe huru mwezi wa ramadhani tufanye mambo yetu tunayoyataka. Tatu, mashamba yasigawanywe na mjumbe wala councillor. Chief, chairman, village chairman. Yangu ni hayo.

**Com. Baraza:** Nina swali.

**Mr. Mwakungu:** Niulize mama.

**Com. Baraza:** Siku zingine zisizo za ramadhani mnasumbuliwa na polisi?

**Mr. Mwakungu:** Hata siku zingine pia tunasumbuliwa lakini uchungu ni ramadhani. Hata hivi si ajabu nikitoka hapa, wako huko, nimefanya kuficha tu.

**Com. Baraza:** Sawa, na mambo ya mashamba sikuelewa. Umesema na iwe watu wengine isipokuwa law courts na wewe unaweza kuuzia mtu. Nikitoka bara kama mimi nitake kununua kutoka kwa wewe unaweza kuniuzia?

**Mr. Mwakungu:** Hatuwezi kuuza kwa sababu mimi nikiwa mdogo kama mwaka sabini na sita kama sina makosa ama sabini na saba nilisikia Ngala ameenda Ukunda kulikuwa kuna shamba ina matatizo huko. Ngala akaenda akaitoa hiyo shamba na alisema hakuna mtu ambaye ataiuza, na mpaka dakika hii sehemu hiyo ya Ukunda ya shamu hakuna mkikuyu wala nani, ni wao wenyewe wanamiliki ardhi yao. Kwa hivyo kama kutakuwa tuna haki yetu kuna faida gani mimi nina shamba acre kumi nikatafute mkikuyu nije nimuuzie. Ndio mambo tusiyoyataka hayo mama. Hatuuzi.

**Com. Swazuri:** Bakari Kazi Mwakazi.

**Mr. Bakari:** Asante sana kamati ya kurekebisha Katiba kwa kuja hapa Pwanikwa kutaka maoni ya wananchi. hivi sasa ninavyozungumza, mimi jina langu naitwa Bakari Kazi Mwakazi kutoka hapa Goleni. Mimi ni mkulima. Mimi nashukuru kwa kupata hii nafasi, kwa kuzungumza machache ijapokuwa mengi yameshazungumzwa na kile ililozungumzwa kwa kusema kweli imenifaa. Na kama ingekuwa watu wanachukua memorandum mpaka dakika hii ningesema hii maneno imekwisha kwa sababu kila mmoja atakayekuja anasema habari ya Majimbo. Mbona matatizo haya yote uliyoyasikia katika katika mambo ya wananchi vile wanavyolalamika. Ni kwa sababu ya usawa wa serikali haifanyi usawa katika wananchi wake hasa katika Kwale. Sasa basi, katika urekebishaji huu wa Katiba hii ya sasa ambayo tunatarajia pengine tutaambiwa vile tumezungumza kwa sababu siku za nyumba tulikuwa na Tumekama hii ya Njonjo na akaje mpaka hapa. tukapiga kelele, tukapiga kelele baadaye hiyo ikatokomea kabisa ikaenda.

**Com. Swazuri:** Tumeya Njonjo haiandamani na Tumeya kurekebisha katiba.

**Mr. Bakari:** Sawa, sasa wasiwasi wangu ni kwamba kwa vile hatujapata majibu naona labda imetokomea, lakini asante. Sasa, kelele zote hizi bwana mimi nataka jambo la kwanza, Majimbo. Utawala wa Majimbo katika kenya. Na kama katika kenya wengine hawataki sisi watu wa Pwanitunataka Majimbo. Pili, neno squatter kwa vile sisi tumepata uhuru liondoke. Tatu, scheme iondoke hasa katika Kwale kwa sababu haina usawa kulingana na kugawanya. Mahali scheme ni mahali ambapo hakuna mimea ya watu. Ni mahali msitu hiyo inaitwa scheme kila mmoja yule ambaye hana shamba aende. Lakini scheme ikiwa hapa Pwanihasa Kwale district ndio watu wagonjwa sana katika kenya nzima. Ijapokuwa watu wanasema kenya ni moja.

Yes, ni moja, mtu anaweza kukaa mahali popote lakini aliyesema kenya ni mbili ni nani. Si ni moja lakini kila mmoja anastahili akae pale mahali pake ambapo Mwenyezi Mungu alimwambia akae hapo. Kwa mfano kuna wakamba, kwao ni ukambani, wadigo kwao ni coast, wakikuyu kwao kikuyuni, wajaluo kwao ni ujaluoni. Sasa ikiwa Mwenyezi Mungu alipanga hivyo kwa nini sisi tukaidi? Tufuate hivyo hivyo. Kwa hivyo kelele zote bwana hizi ni Majimbo. Na hii ya kusema 80% kila kitu tutatengeneza tukiwa tumepata Majimbo lakini ugonjwa mkubwa tunataka Majimbo.

Na wenzangu umewapa dakika tano lakini mimi sitaki hizo ni nyingi sana. hizo zangu ni mbili tu tatu lakini yote yamezungumzwa

na watu ambao wameketi hapa na wakazungumza na yote yaliyozungumza ni yangu mimi. Kwa hivyo mimi ninatia mkazo. Majimbo bwana. Asante. Kwani kati ya nyinyi hapo, hamtaki Majimbo? Mimi najua mzee pale pengine alikuwa na wasiwasi kabila mbili bwana ndizo ambazo hazitaki Majimbo katika kenya na mkiniambia nitaje nitataja. Kikuyu na mkamba. Jaluo hana neno.

**Com. Swazuri:** Atafuatiwa na Ali.

**Mr. Ali:** Bwana kamishina, wakwale wenzangu mabibi na mabwana salaam aleikum. Kamishina wetu nafikiri kitu cha kwanza ambacho tunahitaji kirekebishwe katika hii Katiba mpya ni uwezo wa Rais upunguzwe halafu serikali iwe ya Majimbo kwa sababu hii ndio dawa pekee ya Wapwani. Hii ndio itatibu ugonjwa wa elimu, ugonjwa wa ardhi, ugonjwa wa kazi, ugonjwa wa makao na ugonjwa wa maendeleo na ni hali hii hii ya utawala wa Majimbo ama serikali ya Majimbo ikiwa itakubaliwa ndio itafanya DDC iwe na maana kwa sababu DDC ilikuwa introduced kutupumbaza sisi watu wa Pwanikwa sababu ile composition ya members wa DDC 95% ya departmental heads ambapo hutapata watu wa pwani, utapata ni watu wa bara na interest zao haziko hapa pwani. Kwa hiyo wakati ukipeleka mapendekezo yenu kama wakaaji wa Kwale ama watu wa Pwanikwa sababu majority ya wale members wa DDC ni watu wa kutoka nje hawayatilii maanani na hata ikifikia wakati wakupatia ile miradi priority utakuta wenyeji ambao ni indigenous ambao ni members wa DDC watashindwa kwa sababu ni simple minority sio simple majority.

Kwa hivyo kila atakayesimama hata hawa waliokuja hapa hata wale walioko nyumbani ukiwauliza rai yao kuhusu mwongozo ama serikali wanayoitaka watakuambia ni Majimbo kwa sababu wanakuta hiyo peke yake ndio itakuwa ni dawa kutokana na matatizo walio nayo hapa Pwanitangu ukoloni mpaka tumepata uhuru lakini hakuna mafanikio yoyote. Nafikiri mpaka sasa hivi utapata zile universities zote ziko kwa location moja na hasa mtoto wako akichaguliwa kwenda university atapatiwa zile faculty kama animal husbandry na akitoka huko atabaki nyumbani sawa na yule hakuenda shule. Tukiwa na mikutano tunaeleza kwamba watu wa Pwanitumeachwa tuna watoto ni graduates lakini hawapatiwi kazi. Hii ni kwa sababu kwamba faculty ambazo wanapatiwa hazimfaidishi maana zile nzuri nzuri zinapatiwa wale.

Unakuta pia kama shirika ya kutoka nje tuna mengine ambayo pia yako hapa kwale lakini ukienda wale wafanyi kazi wa hilo shirika utapata hakuna hata mtu mmoja wa hapa kale lakini wale wafadhili wanajua tu kwamba watu wa Kwale wanafaidika tunawasaidia kimiradi lakini wasimamizi pia sio sisi. Kwa hivyo tuna imani ya kwamba serikali kwamba serikali inayokuwa ya Majimbo governor, DC, DO, Chifu hawa wote watakuwa ni indigenous wa hizo sehemu. Kwa hivyo wakati wanakaa kwa mipango ya maendeleo. Ni wao wenyewe watapeana priority kwa miradi yao na wenyewe watatekeleza. Na kwa sababu kwa upande wa uchumi tutakuwa hizo resources zote za Pwaniziko mikononi mwetu basi hatutakuwa tunategemea central government. Kule tulikoachwa tuta-adjust wenyewe na kuona nasi tunakuwa kama wenzetu.

Kwa hivyo tutasema elfu moja lakini kitu muhimu ama dawa pekee itatuokoa ni serikali ya Majimbo. Utapata mpaka sasa hivi

issue kama ya national identity card hapa imekuwa na matatizo amewekwa mtu kutoka nje ambaye ni registar of persons na hata akiletewa barua ya chief ambayo chief ndio indigenous na anajua ya kwamba huyu ni mtoto wa fulani bado atahangaishwa, mara anaambiwa afanyiwe vetting mara afanyiwe nini. Wakati kule kwingine sehemu nyingine za kenya ambaye anahusika na kuandikisha ama utoaji wa vitambulisho ni mwenyeji wa ile sehemu hakuna hizo conditions. Kwa hivyo ningeomba katika Katiba hii uwezo wa kuandikisha vitambulisho urudi ofisi ya ma-chief, kwa sababu chief kupitia kwa village chairman wake ndio wanajua wazi kwamba huyu ni mtoto wa nani na anastahili kupata nini.

Habari ya matatizo ya mashamba kama ilivyoelezwa ya kwamba ni ajabu, mtoto wako umemzaa wewe halafu jina lake likatolewe Nairobi. Ardhi iko kwale imepimwa hapa lakini uwezo wa kibali unatoka Nairobi kwa Commissioner of lands ndio pekee ana uwezo wa kukupatia wewe document. Kwa nini kama composition ya kamati ya ploti ya location ni indigenous wenyewe. Local office kama district isiwe na uwezo wa kutoa hizo document. Ni makosa makubwa kila baada ya miaka kumi na mitano tunachagua waBunge only kuenda tu kupitisha ya kwamba mwanadamu akiuawa na ndovu ridhaa yake iwe shillingi elfu thelathini ambazo hata yule kin of interest atakufa na hajalipwa.

Kwa hiyo tunataka wanyama wa mwitu katika wale watu wanaoishi sehemu za hifadhi za wanyama wa pori wawe beneficiaries direct na kwa sababu tunataka federal government ni kwamba hizo resources zote zitakuwa kwetu mikononi na ni hiyo 25% ambayo tunajaribu kupendekeza itaenda kwa Central Governmentotherwise mapato yote ya Pwani yabaki kwa mPwanimaana aliachwa na mpaka sasa hivi anatumiwa kama stepping stone. Asante.

**Com. Swazuri:** Halima na Idriss awe tayari.

**Mrs. Halima:** Makamishina, kina baba, kina mama salaam Aleikum. Mimi kwa ufupi bwana kamishina maoni yangu nilikuwa kwanza kabisa naomba katika hii Katiba itakayoandikishwa sasa kuwe na utangulizi na utangulizi huu utaje juu ya Majimbo. Halafu kuhusu mfumo wa serikali nilikuwa naomba serikali ya Majimbo na Majimbo haya tunataka kuwe na Rais mmoja lakini Rais yule asiwe na mamlaka katika jimbo. Kila watu wawe watajisimamia wenyewe katika jimbo lao. Katika chochote kile kitakachopatikana kwenye jimbo, asilimia sabini na tano ibaki kwenye jimbo, asilimia ishirini na tano iende kwa central government. Kuhusu mambo ya kuuza mashamba. Mimi kwa maoni yangu sipendelei kuuza mashamba bali mashamba, mtu kwa mfano amependezwa na shamba awe akikodisha badala ya kuuza.

Kuhusu kina mama- kina mama wawe na uridhi kwa mabwana zao kusudi tupunguze mambo ya talaka na pia vile vile waridhi makwao kabla hawajaolewa wawe wameridhishwa na kuhusu watoto pia wasinyanyaswe na wasibaguliwe kimakazi. Kama ni kufanya kazi wafanye kazi sawa na mtoto wa kiume afanye kazi sawa na mtoto wa kike. Kuhusu walemavu, wasibaguliwe, wapatiwe makazi sawa na wale wengine. Kama magari yaletwe ya kutosha, machine hizi za kushonea waletewe za kutosha, naona hayo kwa leo bwana kamishina nasema asante sana.

**Com. Swazuri:** Mwingine ni Bi. Omari.

**Mrs. Omari:** Bwana kamishina mabibi na mabwana. Salaam Aleikum. Mimi kwa ufupi mambo yangu yamesemwa na watu wengi lakini jambo la kwanza mimi nataka Majimbo kwa sababu Majimbo kukiwa kuna Majimbo jimbo la Pwanikujitawala itakuwa ni urahisi watoto wetu kupata kazi yatakuwa ni rahisi serikali kutusikiza, wakati huu ambapo serikali ni hiyo kubwa huko watoto wetu hawapati makazi, kwanza hatuna university ambayo ni kitu cha muhimu. Tumepiga kelele kwenye mikutano kila siku tunaomba university hapa lakini hata inaonekana serikali haitujali. Kwa hivyo kwa ufupi tukipata Majimbo tutakuwa tunaweza kujitawala ama kujifanyia sisi wenyewe. Jambo la pili ni kuhusu mashamba. Tumenyanyaswa kwa muda mrefu. Mtu umeishi miaka karibu hamsini sitini mahali. Unaambiwa kwamba ni squatter. U-squatter huu hatujui tumetoka Tanzania ama tumetoka wapi. Mambo ya squatter hatuyataki. Sisi ni wananchi wa Kenya, na mtu kama umeishi zaidi ya miaka ishirini haina haja ya kwamba mtu mwingine aje na karatasi kutoka Nairobi huko au kutoka headquaters huko anasema kwamba amepata karatasi unaambiwa uondoke hapo na una miaka ishirini au thelathini hapo. Mambo ya mashamba ningeomba serikali mpya inayokuja iwe yataachiwa wenyeji. Watu kutoka zamani wanaishi bila title deed na watu walikuwa wakiishi bila kusukumana, bila kupigana. Jambo jingine ni kuhusu akina mama, kina mama kidogo tumebaguliwa, mna-apply kazi, mtu umepita mtihani wa hiyo kazi lakini kunakuwa kuna mambo mengine hapo ambayo hayaeleweki.

Kwa hivyo akina mama pia tunataka uwezo wa kikazi, tuwe tunapatiwa makazi ya kisasa. Bado kidogo bwana kamishina. Jambo jingine ni kuhusu hao maKadhi pia kama tuliyosema kwamba serikali iwe ya Majimbo, mambo yote tufanye wenyewe hapa. na ikiwa pengine haitakuwa hivyo basi sisi watu wa Pwanitupewe jimbo letu tujitawale maanake tumesumbuliwa watoto hawapati makazi kwa ufupi kwa vile ameitwa mwenzangu, mimi nasema asante bwana kamishina lakini msisitize hayo mambo ya Majimbo.

**Com. Swazuri:** Nasikia kuna machifu ambao wanaogopa kusema. Tunawaambia kwamba tumewasomea hapa sheria, hakuna mtu anayeruhusiwa kuadhibu mwingine au kumzuia kutoa maoni yake. hiyo nilisema hapa mbele. Chief, DC, DO hata nilimwambia hata yeye aseme maoni yake kwa sababu chief na DO na wewe ni mwananchi wa kenya. Hutakuwa chief ama DO permanent, kwa sababu utakuwa raia wa kawaida. Kama maoni yangu ukiyatoa. Kwa hivyo ma-chief mlioko hapa, hakuna kuogopa. Sheria iko ambayo inawaruhusu mseme. Wale ma-chief tuliokuwa nao Kinango walisema kila kitu mbona nyinyi mnaogopa? Mama endelea.

**Mrs. Kauchi :** Asante sana bwana kamishina na wazee, na viongozi wa ngazi mbali mbali pia. Mimi jina langu naitwa Kauchi Chivumba.

**Com. Swazuri:** Wacha tumpishe mama kwanza akimaliza utapata nafasi.

**Mrs. Kauchi:** Mimi kwa jina naitwa Kauchi Chivumba, nawakilisha chama cha national council of women of Kenya, na pia

kwa vile mimi ni mama, watoto pia lazima niwawakilishe kwa vile ambavyo dakika ni tano tu peke yake na niko na memorandum, kwa upande wa akina mama tumeizungumzia bill of rights, women's participation of the legislature and local authority na pia tumeizungumzia mambo ya governance na decision making, tumeizungumzia pia mambo ya state. Tumezungumzia family protection and children's rights, property and land's rights, elections, local governance, substation, citizenship na public finances, huo ni upande wa akina mama.

Kwa upande wa children's rights tuko na principles maalum ambazo ni constitutional principles ambazo tumezungumzia kuhusu defination of a child yaani mtoto awe ni mtu aina gani ambapo tunasema kuwa ni kutoka pale umri anazaliwa mpaka akiwa miaka kumi na minane huyo tunamhesabu ni mtoto. Na pia nationality and citizenship ama citizen rights za mtoto, rights and life and basic rights, rights to education, protection from abuse and exploitive measures, based interest principles, special constitutional offices for protection of children, access to justice by children and governance lakini mimi mwenyewe ndio nina maneno kidogo ambayo ningependa kuyaongea. Hizo zote niko na memorandum zake. Kwa upande wa elimu nasema watoto wote wapate elimu sawa mpaka chuo kikuu. Elimu ya lazima na ya bure bila kubagua msichana mvulana na mlemavu. Msichana aendelee na masomo yake hata kwa bahati mbaya iwapo amepata mtoto msichana aendelee na kusoma.

Mtoto ana haki ya kusafiri na mama yake hasa wale wanaozaliwa nje ya nchi na mama mkenya wawe na haki ya kuingia kenya bila masharti. Mume anayempatia mume mtoto msichana na akatae kumhudumia mtoto huyo alazimishwe kumhudumia mtoto huyo au aadhibiwe. Hapa tunasema ni ile affiliation Act iwe itarudishwa. Wazazi wanaowaoza watoto wao wa kike na pia wa kiume walio na umri chini ya miaka kumi na minane waadhibiwe vikali, serikali iangalie.

Watoto wote wana haki ya kurithi, mtoto wa kike, wa kiume na hata wale waliozaliwa nje ya ndoa pia wana haki kuridhi kwa hivyo wasiwachwe. Na kwenye mitihani ya kitaifa, kuwe na index number peke yake kwa sasa kuna index number na jina. Hapo utakuta kila ukiangalia majina ambayo ni ya upande wa pwani, siku zote ni kama bei iko nyuma wanaonekana kwamba si werevu. Hawa watu wa Pwanikusema kweli ni werevu lakini hayo mambo ya index number halafu hapo hapo pana Salim ama Fatuma, kusema kweli tunanyanyaswa kwa upande wa ku-mark mitihani.

Kwa hivyo ikiwezekana iwe ni index peke yake kama pale mwanzo. Kupunguza umaskini serikali iwe na mpango wa kuwapa kiwango maalum cha pesa yaani allowance kwa wasio kazi ili wasikose chakula haya ndio ambayo yanaleta matatizo ya machokora ama watoto wa barabarani ama na ujambazi pia maanake kuna ukosefu wa kazi sana. kila mtoto anayezaliwa awe na allowance ya kumwezesha kuishi na kukua vyema. Yaani ni serikali hiyo ifanye hivyo. Uajiri wa kazi wafikiriwe wale waliomo katika wilaya, mkoa wa kwanza kama KPA, mahoteli na makampuni nyinginezo, kuanzia kazi zisizokuwa na ujuzi na pia za ujuzi.

Kuwe na haki sawa ya uajiri wa ngazi za juu katika wizara zote na hata Bungeni kwenye kamati za mawaziri na hata serikali za wilaya. Tabia za kuumiza- kuna watu wengi ambao wana tabia ya kunajisi watoto, wazee au walemavu. Hawa watu, serikali

itilie mkazo hata katika hii Katiba yetu. Wapewe adhabu kali. Wazazi wanaoingilia watoto wao kimwili wapewe adhabu kama hiyo ya kunajisi, adhabu kali. Katiba mpya ikomeshe tabia ya kufanya mapenzi waume kwa waume yaani homosexuality, au mke kwa mke that is lesbianism au ndoa hizi za aibu. Watu hawa wakipatikana wafungwe maisha maana hawana maana humu. Kuna wanawake wengine wanaolipa mahari ili kuoa wasichana wadogo na wale wasichana wadogo kwa kuwa yeye ni mwanamke amemuoa msichana mdogo, anawawacha watembee na yeyote ili wawazalie watoto. Haya huwa hasa inafanywa na wanawake ambayo hawakubahatika kupata mtoto badala ya kuenda kufanya adoption anachukua msichana mdogo halafu anamwachilia huru ili awazalie watoto.

Hii ni tabia ya kinyama na adhabu kali sana ifanywe kwao. Mume yeyote asimpige na kumnyanyasa mkewe nyumbani na kumjeruhi mwili. Huyu mume amlipe gharama mkewe na pia achapwe viboko ikiwezekana ili ayasikie maumivu hata yeye yale ambayo mwanamke anayasikia kwa kupigwa. Yaani hii Katiba yetu iangalie sana, kuna wazazi ambao wanawatendea kinyama waoto wao ama pengine mtoto wa kambo. Mtoto amechelewa lakini yeye anamwadhibu vibaya ama pengine kumpeleka shule hampeleki ama hampatii zile basic needs za sawa.

Umilikaji wa ardhi- hatutaki raia wa kenya awe squatter wa mtu mweupe au mtu yeyote ambaye hatoki ama haishi sehemu inayoishi wanaoitwa masquatter. Hakuna squatter anayeishi kwenye shamba iliyoishi babu ama wazazi wake pia. Ugawaji wa ardhi, wahusishwe wenyewe wa pahali hapo panapogawanywa hiyo shamba na ikiwezekana wenyewe wapate ardhi ile sehemu yao. Hatutaki kunyanyaswa na ardhi yetu na watu kutoka wilaya nyingine na mikoa mingine. Na vyeti vyote vya kumiliki mashamba yaani title deeds zitolewe wilayani sio Nairobi. Utakuta kuwa kuna mashamba mengine yale ya kawaida ambayo yalitumwa kawaida, title deed zinaletwa hapa. halafu kuna yale mashamba ambayo yanapimwa kwenye meza title deed zake zinapatwa Nairobi. Yaonyesha kuwa hapo kuna unyanyasaji ama kuna uporaji mali ya wenyewe.

Magonjwa ya kuambukiza yasio tiba kama ukimwi. Sheria iwekwe na kuzingatiwa katika Katiba mpya kwamba yeyote anayepatikana na hatia ya kumwambukiza mwenzake ugonjwa kwa kudhamiria iwe kwa kumnajisi ama kwa kukusudia ahukumiwe na apate adhabu kali sana ama hata ahukumiwe kifungu cha maisha hata kifo. Ukahaba au umalaya, upigwe marufuku katika Katiba hii mpya ya kenya. Utakuta hivi sasa tunawapatia majina yaani tunatoa majina kama Malaya, tunawaita commercial sex workers ili watu waendelee ku-practice umalaya, hiyo hatutaki. Katika Katiba hii yetu mpya hiyo ikomeshwe kabisa na anayepatikana akiuza mwili wake ama kufanya biashara ya kuajiri wasichana wadogo wampatie pesa kwa kufanya umalaya ahukumiwe kifo.

Tunataka iwe ni sheria, wakenya kuvaa mavazi ya heshima. Vazi linaloonyesha matusi na kuleta hamu ya ubakathi lipigwe marufuku katika Katiba yetu na tunasema kuwa kiswahili iwe ni lugha ya taifa na kiingereza iwe ni lugha ya ofisi. Tunapenda Katiba mpya iandikwe kwa lugha ya kiingereza na kiswahili. Pia lugha hizi mbili ziwe rahisi na kueleweka. Hapo nyuma Katiba ilikuwa ni kama ambaye inasambazwa kiuchoyo ndio maana hivi sasa civic providers wamepata shida kabisa kuelimisha mambo ya katiba.

Tunataka katika Katiba hii mpya, Katiba isambazwe kote nchini na ifundishwe hata shuleni ili tuijue Katiba yetu kuanzia mashinani. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Amin Ali.

**Mr. Ali:** Bwana kamishina, mabibi na mabwana salaam aleikum. Katika Katiba ya kenya tumewahi kuwa na Katiba ya kenya moja kutoka sitini na tatu mpaka wakati huu. Katiba hii ilikuwa ni ya unitary ambayo tumeweza kuona vituko vingi vya unyanyasaji wa ardhi, wizi, abuse of office na kunyang'anywa mashamba yetu. Katika wakati huu tunataka tujaribu utawala wa kimajimbo. Mimi nimejiandaa kuwa na memorandum lakini nitaigusia sehemu kidogo kidogo kwa sababu sehemu nyingi zimeguswa. Katika katika Katiba ya leo tunajaribu kuona kuwa asilimia sitini na tano ya Katiba ikiwa kuna uwezekano wa kubadilishwa iwe imepata vote yaani wananchi waulizwe asilimia sitini na tano wananchi wakubali Katiba kubadilishwa ama la. asili mia sitini na tano ikikubalika, inaweza kuingizwa Bunge na asilimia mbili ama tatu ya Bunge ikikubali kubadilishwa Katiba hii iwe imepita. Hayo mabadiliko yawe katika hiyo kiwango fulani cha katiba.

Citizenship- katika kenya tuko na kama makabila arobaini na mbili. Ningeliomba makabila haya yote bila ya kuulizwa ulizaliwa na nani ama nani iwe ni automatic citizenship. Na wale wenye kuja kutoka kwa nchi fulani waombe citizenship kupitia kwa immigration office na wawe hawana mamlaka ya either kumiliki ardhi moja kwa moja ama kuingia kwenye siasa moja kwa moja.

Nitazungumza kuhusu defence and security- twazungumza kuhusu defence and security katika serikali ya Majimbo Central Governmentitakuwa ikimiliki army, navy na air force na regional government itakuwa ina huduma za polisi wao wenyewe kwa hivyo kila jimbo litakuwa na polisi wake baadaye polisi bora katika kila jimbo watachaguliwa equal numbers wa kila jimbo watengeneze central police court ambayo itakuwa ni ya Central Governmentili kuweza kufanya kazi pamoja na nchi za nje.

Hawa navy, central police code pamoja na army watakuwa chini ya Central Governmentambayo itakuwa under the prime minister. Political parties – ni ubora katika kenya kwa vile iko na makabila mengi si ubora kuwa kabila iwe na chama chake cha kisiasa. Kwa hivyo ni ubora kuwa vyama vya kisiasa visizidi kumi na viwili. Kwa hivyo Katiba iruhusu vyama visizidi kumi na viwili katika siasa.

Mawaziri – Prime Minister ndiye atakayechukua jukumu la serikali, itakuwa ni kazi yake kutoa majina au kukisia majina ambayo yatakuwa ni ministers ambapo majina yale kabla hajakuwa appointed ama kwa mfano yawe vetted na regional provinces. Kwa hivyo kila jina la waziri lirudishwe kwa regional ili lipate vetting asije akajipandishia minister ambaye he is so corrupt kiasi cha kuwa either ni kabila lake, ni jirani yake ama pana undugu ndani. Kwa hivyo kila mtu ambaye anachukua uaziri awe vetted na province zote nane ama kumi.

Ma-mayor – ma-mayor wote wawe wanachaguliwa na raia baada ya kuwa wameshakuwa ma-councillor. Ardhi- kwa sababu kutoka mwaka wa uhuru mpaka sasa utakuta watu wa Pwaniwote ni masquatter. Ni kitu cha kuhuzunisha kuwa ardhi yote iko chini ya mtu mmoja kutokana hii system ya central government. kwa hivyo mtu huyu ana uwezo wa kuamua kunipa mimi mjukuu wake part of land iliyo Lunga lunga ama Lukore ama Lodwar ama Nyanza kwa sababu yeye ardhi ni yake na anapompa letter of appointment baada ya muda fulani anapewa title deed moja kwa moja huko huko. Hali hii ardhi yote iwe chini ya regional government ndio mwenye ardhi mkuu, kisha mtu wa kawaida asiwe na ardhi zaidi ya acre mia moja na ardhi hii iwe yake wakati amei-develop. Sio ardhi tu ambayo ni mbunga hapa anavuga kwa sababu ni yake ana title deed. Iwe ni kiasi cha kile ambacho ameweza kui-develop peke yake. ile sehemu ambayo imebaki mbunga iweze kugawanywa wale ambao hawana mashamba na mtu mgeni yeyote ambaye anatoka either province ya pili ama nchi yoyote ya pili na anataka kuishi katika jimbo lile, anaweza kupata ardhi isiozidi acre mia moja. Na uuzaji wa ardhi uwe umepigwa marufuku kabisa isipokuwa uuzaji wa property. Kile kilicho katika ardhi ile ndicho unakiuza, sio ardhi ambayo sio yako. Kile kilicho juu, either ni nyumba ni mashamba, ni mmea ndio unaiuza lakini sio kuuza part of land ambayo it is undeveloped. Kwa hivyo uuzaji wa ardhi wote upigwe marufuku. Hii ni kwa sababu utakuta ardhi ambayo mtu amechukulia hapa na Kinango kwa sababu hana kazi nayo anaweza akaiuzia watu zaidi ya kumi ajipatie mapesa ale tu na kuna masquatter ndani.

Kwa hivyo huu mtindo upigwe marufuku. Pili, wakati wa kuuza ardhi, DC ambaye mpaka sasa ndiye chairman of land committee awe amepigwa marufuku. Tunataka mtu wa kijiji kile ama location ile awe amechaguliwa kusimamia uuzaji wa ardhi na committee members wa ile kamati lazima wakathibitishe ardhi yenyewe inapouzwa. Na mwisho nikimalizia ni kuwa ardhi zote zile ambazo zinaitwa trustee na state land zote zirudishiwe wenyewe ili kusiwe na masquatter kabisa kabisa. Katika hali hii itamfanya kila raia wa kenya asiitwe squatter. Huwezi kuishi katika ardhi na miaka ishirini na bado unaitwa squatter. Kwa hivyo neno squatter lipigwe marufuku kabisa.

Economic- Pwani ama jimbo lolote liwe lina uwezo wa kujitafutia donors nje direct. Isiwe ni kupitia kwa mtu mmoja Nairobi ndipo akiona pande muhimu ya donor huyo kuletwa mombasa aletwe Mombasa. Liwe jimbo linaweza kujitafutia donors effectors direct nje.

Minerals- kitu kama madini ningelipenda district ile ambayo iko na madini iweze kupata asilimia arobaini ili iweze kunufaisha wananchi katika district ile. Central Governmentipewe portion ya 20% of the total profit kutokana na mauzo ya madini yale na utalii wote fedha za kitalii zote ziweze kusaidia direct kwa mwananchi ili aweze kuondoa mahitaji yake. Pili iweze kufuata vitu kama universities, industries na kila kitu. Tatu na mwisho ni kuwa kila crop iweze kutengenezewa factory yake I-benefit mkulima katika crop ile. Utakuta sasa Pwanituna aina nne ya crops lakini zote hazina factory na hii imesababisha watu wa Pwanikuwa maskini, kiasi cha kuwa hawezi hata kumsomesha mtoto wake.

Kwa hivyo hizi crops nne kuanzia korosho, bigza, maembe, na zile citrus fruits na nazi, hizi zote kama tungekuwa watu wa Pwaniwote sio maskini. Lakini kwa sababu ya uhaba ya kufinywa hao / wote wameweza kuwekwa bara na sisi tumebaki bila

industry yoyote. Kwa hivyo all food products zipatikane cash crops zote ziwe na factory hapa hapa pwani. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Toa memorandum pale na uandike majina. Chief Mamba.

**Chief Mamba:** Asanteni sana makamishina wote mlio hapa pamoja na ndugu wote mlio hapa, akina baba na akina mama salaam aleikum. Kwa jumla taratibu zote zimezungumzwa lakini yangu natoa tu kupatana na zile memorandum ambayo natarajia zikiwa ndani zitakuwa zimesaidia zitakuwa zimesaidia wananchi wengi. Kwanza wazee wa vijiji kwa kila location wapatiwe mishahara ya kikawaida ili zile kazi ziwe rahisi kwa location na itakuwa kwa division mpaka kwa district. Ulipaji wa mishahara ya wafanyi kazi wote wawe wa serikali, wawe wa makampuni iwe mishahara ya hali ya juu ili iweze kusababisha wafanyaji kazi wale waweze kutekeleza mahitaji yao kwa watoto wao yaani mambo ya family zao na mambo ya masomo.

Passport number tatu, passport irahisishwe sawa na kitambulisho pamoja na birth certificate viteremshwe viwe hali ya urahisi ili mtu ile passport asipate kwa ugumu, ule ambao hata sasa unaendelea kuwa ni lazima wathamini sijui watatu, tena kule mpaka itapitia sijui ni njia ngapi, hiyo passport hata inachukua muda hata ukipata umepata taabu sana. kwa hivyo ifanywe kibali sawa na kile cha ID card kwa sababu ukitaka kwenda nchi ya nje tayari kinakuruhusu.

Upande wa ID cards hizi ID cards zote zirudishwe kwa ma-location mahali ma-chief wako, wazee wale wa vijiji wako hapo kwa hivyo kila ofisi ya chifu itumiwe wafanyi kazi wa vitambulisho na vetting itakuwa moja kwa moja pale ofisini kwa chief. Birth certificate. Masharti ambayo yalipangwa kule yapunguzwe maana ni jambo la ajabu kuwa mimi pengine sijachukua birth certificate lakini inasemekana mpaka niwe na card ya clinic. Sasa mama alikufa na hata akiwa ni mzima, si rahisi mtu kama mimi kuwa na ile clinic card. Kwa hivyo irahisishwe kikamilifu masharti hayo sijui clinic card, sijui nini, yote yatolewe ili ipatikane kwa sababu ni kibali ambacho ni muhimu.

Haya narudi kwa mambo ya vyuo vikuu. Vyuo vikuu kila mkoa mfano sasa kama hapa Pwanipawekwe chuo kikuu kama vile Mombasa polytechnic ama kama kule shanzu teachers college viwe hata ikiwa ni viwili vitatu hata Matuga DDI iwe na chuo kikuu ili watu wawe karibu na hivyo. Hivi nikisema vyuo vikuu vitamaanisha kati ya hivyo viwe vitatu ama vinne viwe vya udaktari, viwe vya utalii na aina nyingine na itakuwa imerahisha wale wasomi kuwa karibu.

Nikishamalizia, hawa ma-NGOs mashirika ambayo huwa yakiwasili kwa mfano kwa district headquaters. Mawasiliano yapitie through chief’s office ili wale wafadhili, wale machifu wote wa kila ma-location ndio wanajua zile shida za pale. Hiyo itakuwa ni jambo bora na hizi shida kama ni za maji, kama ni za madaraja, kama ni wapi na wapi mambo yote yatakuwa rahisi kwa sababu wale ma-chief wanajua taratibu za shida hizo.

Nikimaliza, huduma za mahospitali. Huduma za mahospitali kwa kusema kweli mpaka ziwe na wale waangalizi yale ambayo wanafuatilia. Kwanza kwa njia rahisi pesa zimekuwa juu. Kuwe kwa jumla pesa hakuna. Na madawa yawe ya kutosha kisha

hospitali hizi kila location yaani kila district itakuwa ni ubora tupate hospitali ambayo operation inafanyiwa hapo. Kwa mfano Kwale ni Kwale hospital lakini shida ya operation mpaka Msambweni au Kinango mama anazaa njiani na anaweza akafia hapo hapo kabla ya kufika pale mahali ya uzalishaji. Kwa hivyo hilo lipitishwe na liwe watu watakuwa taratibu za mambo haya. Nafikiri mengi yameongewa na mimi ilikuwa ni kuongeza nikifikia hapo nasema salaam aleikum asanteni.

Sasa, asante sana bi. Kamishina, nikisema hospitali ziwe hali ya juu tayari najua kukamilika kwanza nipewe na gari ambayo ni ambulance. Pawe na madaktari ambao ni wale operation wanaifanya. Halafu nilikuwa nimesahau mahali kidogo mnisamehe, hii taratibu ya uchukuaji wa mambo ya MTC yaani habari za vyuo vikuu na ma-university. Hilo jambo kwa kusema kweli ni pangilio ipangwe ya kiusawa. Watoto wanapita na points za kutosha lakini uchukuaji ikienda kule anapangiwa faculty ya chini na pengine yeye kila subject alipita A ama B. kwa hivyo huu uchukuaji wa faculties huko kwa ma-university utazamwe upelekwe kwa njia ya kihaki kabisa bila ya kuacha wengine. Kwa hivyo nikimalizia hapo ni mengi lakini machache kwa leo asanteni.

**Com. Swazuri:** Na wale ma-chief walikuwa wakiogopa kuja, amesema nini mbaya huyo. Councillor mkiwa na mzee Ali muwe tayari.

**Councillor Mabavu:** Ndugu bwana kamishina na bi. Kamishina kwa jina ni Said Mabavu wa Mabavu. Mimi kwanza napendekeza Katiba ama serikali inayokuja iwe ni serikali ya Majimbo na katika haya Majimbo, pendekezo langu ikiwa wanakenya wote watakubaliana basi kila jimbo liweze kuwa na governor. Pia wanakenya tukikubaliana, kila jimbo liweze kuwa na Katiba yake ya kuongoza hilo jimbo. Pia katika marekebisho haya kuna section ya waislamu. Chief Kadhi wa kenya awe anachaguliwa kulingana na taratibu za dini ya Kiislamu. Asichaguliwe na Rais wa jamhuri ama wa jimbo.

Vile vile katika marekebisho haya tunayoyarekebisha yasihitilafiane na taratibu za uongozi na sheria ya Kiislamu kwa maana hayo basi waislamu waweze kuongozwa na sheria ambayo imekamilika kuwahukumu na kuwaongoza. Katiba hiyo katika hali ya marekebisho pia natoa maoni kwamba ni dhambi kwa serikali inayokuja ikiwa ya Majimbo ofisi ya ardhi kubaki Nairobi vile ilivyo.

Pia katika marekebisho haya tunayoyarekebisha, napenda pia iwe waziwazi kwamba ingawaje tumeletewa ile Commission ya kuchunguza maswala ya ardhi lakini inaonekana pia haina matokeo. Basi kulingana na mkataba ule ambao wazee wetu walikuwa wamekubaliana kabla ya hii sehemu ya / kuunganishwa na Jamhuri nzima kulikuwa na mkataba wa maswala ya ardhi kwa hivyo katika Katiba hii ambayo tunairekebisha kuwe na review pia ya kuonyesha je, wakati kenyatta alipokuwa akiomba kwa sultan na akakubaliwa kupewa sehemu hii lakini akapewa na masharti. Je, masharti yale tunavyoelewa sisi vijana licha ya wazee.

Wazee wanaelewa lakini sisi tunaelewa kwamba hakukuwa na marekebisho, hakukuwa na ukamilikishaji wa ule mkataba. Kwa hivyo wengi vijana wa Pwanitunasimamia ule mkataba kwamba pia uweze kurekebishwa kwa sababu hizo land zote wakati ule

ambazo zilikuwa bado ni trust, walizipa majina ya trust land wakazipa whatever zote zimerudi kwa hao watu wakubwa wakubwa wote. Kwa hivyo swala hilo nilikuwa napenda sana liangaliwe.

Pia naungana mkono kwamba swala hili la uongozi wa sehemu za hawa ma-governor kama nilivyotangulia kwamba isiwe ni uongozi wa maPC uondoke na pia uongozi jimbo liwe na full mandate ya kutengeneza serikali yake, kutoka makao makuu mpaka chini. Naamini wakifanya hivyo hawatafanya vile ambavyo watu wananchi hawapendi. Labda nibakishe mengine yale ambayo nitazungumza kule Lunga lunga. Lakini tunasema basi makamishina ikiwa Katiba hii kati ya vile tunatoa maoni yetu tuna wasi wasi kama haitaongoza katika serikali baada ya uchaguzi basi tuna wasiwasi watakaochukua huenda marekebisho haya kama hayataenda mfululizo mpaka kutengeneza serikali inayokuja. Tuna wasiwasi kwamba basi watakaochukua pengine huenda ikapigwa marufuku, ikatupiliwa mbali. Kwa hivyo pia natoa maoni kwamba ni serikali inayokuja iongozwe na haya maoni ya watu wa kenya. Isiwekwe kando watu wakasema wafanye kitu kidogo kwanza kwa sababu we believe watu wengine wakija wakichukua wale ambao kwa sababu we believe wengine wakija wakichukua wale ambao kwa sababu saa hii tunaondoa mamlaka kwa mfano.

Maoni yangu pia naungana na wenzangu kwamba mamlaka ya Rais yamekuwa makubwa na ni kutoka tupate uhuru. Kwa hivyo yapunguzwe na uwezo wapewe parliament. Pia napendekeza Rais wa Jamhuri ya kenya baada ya kuwa Majimbo yanajitawala awe hatoki kwa chama chochote. Napendekeza tuwe katika serikali ya kenya katika Majimbo yanayokuja tuweze kuwa na waziri mkuu.

Pia napeana maoni yangu kama wanakenya watakataa namba kubwa ya neno la Majimbo basi tunawauliza makamishina watafute kipengele chochote cha kuwezesha wale ambao ni kilio chao wapewe sehemu yao ya jimbo lao kwa sababu hiyo imefanyika sehemu za Canada. Kwa hivyo kwa vile tunasikiza ma-civic providers wengi wa kutoka nje na wa kutoka ndani. Kwa hivyo ikiwa ni lazima kwa sababu wengine wanayaogopa, ikiwa ni lazima basi jimbo hili la Pwanimukae mje na decision sawasawa ya kuachiwa hili jimbo letu kwa amani. Mengine nimebakisha, tutakutana inshallah.

**Com. Swazuri:** Asante sana councillor Mabavu.

**Mr. Mwajuma:** Bi. Kamishina na bwana kamishina na mabibi na mabwana salaam aleikum. Mimi maneno yangu ni machache sana kwa sababu mimi nimechaguliwa huko Golini ni chairman na tumeandika ripoti yetu hapa, amekuja secretary wangu akaandika lakini akaambiwa tosha hapo na amepeleka kule. Kuna ripoti kamili ya hayo tumeandika lakini sasa mengine bila shaka tumeandika kama tumesema niseme. Ni hivi naweza kuangalia hawa makamishina. Bwana kamishina, sisi Pwanikutoka kizingitini mpaka Vanga na kwa nini juzi niulize swali lile lile na leo naliuliza vile vile. Mbona ulichaguliwa wewe mwafrika peke yako kutoka kizingitini mpaka vanga. Kwa nini?

Sasa serikali hii ya Katiba haikufanya kazi. Mimi nalia choyo kabisa kwa sababu ukaniambia kwamba kuna wawili

walichaguliwa lakini wale wawili kwa kusema kweli hatutaki kutaja kabila lakini wale wanafuata ukabila. Hata siku moja wewe umesimama hapa mara kadha wa kadha. Hata siku moja mwenzako wa huko uliochaguliwa nao hajaja akazungumza nasi. Hajaja akazungumza nasi hapa. sasa hatufai huyo, tunataka bwana ama bibi atakayesema aseme nasi na sisi tumjibu ili makusudi afahamu tunasema nini na yeye aseme yale yale.

Lakini mpaka sasa nasikitika bwana, wewe peke yako huwezi Pwanihii. Mimi nataka nyinyi muwe watano. Nataka nyinyi muwe watano, kutoka kizingitini mpaka vanga, kutoka mombasa mpaka taita, hii ni nchi kubwa sana, mtu mmoja hawawezi. Na wale wenzako wamechaguliwa lakini ni kimbelembele. Ni watu wa kimbelembele, najua nimeketi nao mimi. Najua watu kimbelembele, sitaki kuwataja.

**Com. baraza:** Hata sisi ni makamishina, kwani hatuwezi kuelewa mambo ya coast?

**Mr. Mwajuma:** Ndio sasa namweleza yeye sasa ataelewa na wewe utaelewa vile vile madam. Kwa sababu kwa nini mlimchagua mtu mmoja tu, mwafrika mmoja tu kutoka kizingitini mpaka vanga. Kutoka Mombasa mpaka taita mwafrika mmoja. Ni nani mwafrika mwingine mnayemtaja?

**Com. Baraza:** Mimi na yeye tu waafrika.

**Mr. Mwajuma:** Ni mwafrika lakini sasa kwa kusema kweli sisi tunazungumza Majimbo, mimi nikizungumza nazungumza Majimbo. Sasa wewe hauko katika jimbo. Sasa kwa sababu hii, tafadhali nataka wewe uongezwe wenzako maana wewe utakufa bwana. Unasema mpaka kichwa kinaumia, uende Vanga, uende Lunga Lunga, uende Diani, uje Kwale na kila kitu kwa nini? Kwa nini iwe namna hiyo? Mimi nasema hivyo kwa sababu ya mimi sina maneno mengi, na maneno yote nitayaona kwenye Katiba ile lakini nasema tafadhali, mama amesema lakini mama yeye ni wa upande wa bara. Sasa bwana, bibi wewe uko upande wa bara bibi wewe. Wewe uko upande wa bara wewe.

**Com. Baraza:** Ee mimi natuka bara lakini huyu jamaa wa coast anaweza kuenda asikize maneno yao.

**Mr. Mwajuma:** Ngoja. Lakini je, mtu wa coast mmoja aangalie ma-district saba, ma-DC manane mtu mmoja peke yake atafanyaje. Watembea naye lakini wewe hujui hii lugha tunazungumza. Sasa mimi nikisema kilugha yeye atasikia lakini wewe hausiki.

**Com. Swazuri:** Haya mzee tumesikia.

**Mr. Mwajuma:** Basi mimi sina mambo mengi lakini naomba Mungu kwamba kazi yenu iwe nzuri na sisi tuendelee vizuri tupate hakika tupate Majimbo. Tukipata Majimbo kelele zitakwisha. Tupate governor wetu tupate na nyinyi na kadhalika na kadhalika

mambo yote yawe sawa.

**Com. Swazuri:** Salim Chapu. Endelea.

**Mr. Chapu:** Makamishina, mabibi na mabwana salaam aleikum. Kwa majina yangu naitwa Salim Salim Chapu. Maoni yangu nataka era ya Majimbo na bila kuficha Majimbo ndio kila kitu. Hakuna haja ya kutangatanga mnakuja mnasema mambo mengi bure. Tukishapata Majimbo, ardhi zote zitarudi kwetu, kazi zote zitarudi kwetu kwa sababu Majimbo maana yake, ni wenyewe tujitawale, wenyewe tumiliki kila kitu. Kwa hivyo kazi kwanza zote zetu. Mapato yote ya jimbo letu tunapata asilimia sabini na tano zote ni zetu automatic ya umajimbo. Ishirini na tano, serikali kuu hakuna shida.

Sehemu yangu si bado iko. Na kukiwa Majimbo na ndio tuyatakayo na yawe hospitali zote za serikali ziwe bure, chakula chote madukani kisimamiwe na serikali za mikoa, ama serikali za Majimbo, maji ya mfereji kila jimbo lisambaze kwa kila mwananchi bure, stima zisambazwe kwa kila mwananchi bure na mila yote ya mijikenda kwa mfano kama vile kupelekana viaponi, hiyo kwa jimbo la Pwanisiwezi sema Majimbo mengine lakini jimbo letu la Pwanimila kama hiyo iwekwe ni sheria.

Elimu ya msingi kutoka nursery mpaka darasa la nane iwe bure na tukirudi kwa ardhi kusisitiza yakiwa Majimbo kuanzia mwaka tuliopata uhuru hadi leo. Ardhi zote ambazo zilipatiwa wageni ama wabara bila mapenzi ya wenyeji wa pwani, zote warudishiwe wenyewe wenyeji bila vikwazo vyovyote. Mfano kama vile Zimbabwe wazungu wanaondolewa na Zimbabwe wenyewe na wame-develop hayo mashamba bila malipo yoyote kwa hivyo vile vile wabara wamenufaika huko Pwanina ardhi zetu Majimbo yakishaingia ardhi zote zirudi kwa Wapwanibila vikwazo vyovyote. Kwa hayo machache Asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Sasa ni bwana Baguani Juma.

**Mr. Baguani:** Asante sana. makamishina, mabibi na mabwana salaam aleikum. Kwa majina naitwa Baguani Juma. Kazi yangu ninayofanya ninasafiri na meli. Maoni yangu mimi Baguani ningependa katika nchi ya kenya Rais mamlaka yake yapunguzwe. Rais asiwaajiri wakuu wa mapolisi, Rais asiwaajiri majaji wakuu. Na wengine walio na vyeo vya juu. Kwa sababu hiyo ndiyo ambayo imechangia ufisadi ukazidi katika hii nchi. Kwa mfumo ambao naona ungeleta amani katika nchi ya kenya ni Majimbo. Na kiupande wangu nasema Majimbo si yale ya kuwafukuza watu bali ni Majimbo ambayo mambo mengi katika mkoa, wenyeji watamiliki.

Sikusema eti mtu kutoka bara atafukuzwa. Ikiwa kwa mfano niliuza shamba yangu nimemuuzia mtu, nikimpokonya nitakuwa nimemdhulumu. Shamba yangu lima, ni yako sasa lakini hii ni Majimbo mamlaka ya wilaya iongezwe. Elimu kutoka class cha nursery mpaka class cha nane ikiwezekana iwe bure kwa sababu wengi wasio na uwezo wanakosa elimu.

Upande mwingine, serikali ambayo itakuja itatawala hapa kenya. Ichukue dhamani ya mwanadamu iwe juu kuliko ya mnyama.

Kwa sababu nikisema hivyo, hapa hapa tulipo, tunaishi na tunaishi na wanyama kama ndovu, na vile tunavyojua hapa kwetu akiua mwanadamu watakuja watu wa wizara ya wanyama watatu wanne na landrover yao moja. Lakini ndovu wakifa, hata DC hakai hapa. mtu akiuawa na ndovu alipwe pesa za kutosha, sio shillingi elfu thelathini kama ambaye ni mtu amekatwa kidole.

**Com. Swazuri:** Alipwe pesa ngapi?

**Mr. Baguani:** Milioni tatu. Na ikiwa ndovu hao hao wameharibu mashamba ya watu moja kwa moja ripoti hii ikipelekwa, utaratibu uchukuliwe na mwenye aliyeharibiwa mimea yake alipwe kwa sababu watu huwa wanapata taabu, ametegemea shamba na limechafuliwa na ndovu, hana chakula, hajui atapata wapi uniform ya watoto wala si ya watoto, sasa yeye ni mtu anakuwa anadhulumika. Ingine, Majimbo yakija na ikiwa mamlaka ni ya kimajimbo urongo, mambo mengine yatafanyika kirahisi maanake hapa kwetu Pwanimkoa ni mkubwa kutoka kizingitini mpaka lamu, kutoa mombasa mpaka taita. Ni njia chache sana ambazo zinapitika. Barabara hakuna na ukweli ni kwamba hata sasa kuna hospitali nyingine mtu akipata faradhi amekufa, inabidi mtu yule achukuliwe na baiskeli apelekwe mahali atakapokwenda zikwa.

Ni jambo la kusikitisha sana kuona tangu uhuru mpaka sasa kuna sehemu nyingi hazifikiki. Ingine tena katika mkoa kwa mfano mkoa wetu wa Pwanitunashangazwa na kitu kimoja sisi, maji mengi yanayotoka sehemu za mlima, maji mengi yanayotoka hapa hapa kwale yanapitishwa chini kwa chini mpaka Mombasa na katikati hii kuna wadigo na waduruma pamoja na ndugu zao wa kikamba ambao ni wa hapa hapa Pwaniwanakosa maji. Ni jambo la kusikitisha, lakini ikiwa umekuwa ni utawala wa kimajimbo urongo sehemu nyingine zitatengenezeka, hata ijapo inchi yetu imekuwa dhaifu, imekuwa na ufisadi mwingi lakini sidhani kama mtu anaweza kukoka moto na akajichoma mwenyewe. Mengine nitasema wakati mwingine asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Sasa tuna Hassan Haji Masa.

**Mr. Hassan:** Asante sana makamishina wote wawili na wageni waliofika. Mimi sina maneno mengi sana mengi yamezungumzwa. Jina langu naitwa Hassan Haji Masa. Kwa sababu mengi yamezungumzwa, mimi nitazungumza kama matatu hivi. Na ni kuongezea tu lakini yameshazungumzwa. Kwanza ni upande wa utawala. Mfumo wa serikali. Serikali ninayohitaji mimi katika mawazo yangu ni Majimbo. Majimbo maana ndicho kitu ambacho kitakuwa kitamfanya kila mwananchi ili aweze kufaidi katika haya matunda ya uhuru.

Kwa upande wa Majimbo, tumezungumza kwamba ma-governor wawe kama vile walivyotajwa kwamba kila jimbo liwe na governor, ikiwa Majimbo ni yale manane basi governors wawe wanane basi governors wawe wanane lakini kwa upande wa Rais ambaye atakuwa katika central government, mimi katika maoni yangu kwa sababu sisi sote ni wananchi wa kenya, Majimbo yote manane ni ya watu wa kenya ili kusiwe na wasiwasi na ikiwa tunapendana kwa kweli kabisa tuwe katika kile cheo cha uRais, kiwe kinaweza kuzunguka kwa Majimbo yote.

Ikiwa wa hamu moja ni kama miaka mitano hivi, Rais akiwa kwa miaka mitano anatoka mimi ningeomba yale Majimbo yakitokea ipitishe sheria ya kwamba mtu akae kwenye kiti kwa miaka mitano halafu akiondoka ipelekwe jimbo jingine. Jimbo lile litolewe candidates kama wanne watano wapiganie uRais. Wazunguke hivyo mpaka Majimbo manane yote itakuwa miaka kama arobaini lakini itakuwa kila mmoja amesha-taste amejaribu na ameona utamu wa uRais. Lakini ikiwa kwa mfano itawekwa huko central, na watu wengine ama kabila jingine ni ndogo sana na kwa kawaida katika ukura watu wanaweza kutoa ile majority na kabila zingine huwa ni ndogo sana. kwa hivyo itakuwa kila mwaka au miaka yote itakuwa uRais unatoka sehemu moja. Maana wengine ni wengi zaidi kuliko wengine. Lakini kama ingepitishwa kwenye Katiba hii ambayo tunaipanga sasa kwamba kila miaka mitano au miaka kumi Rais anakaa pale halafu anaondolewa anapelekwa jimbo jingine, hiyo ni kama wanakwenda round sasa.

Pili ni upande wa elimu. Sote tunafahamu kwamba elimu ndio nguzo ya serikali na watu wengi wanategemea elimu. Sisi tumekuja hapa kwa sababu ya elimu pia lakini wakati ule wa kabla ya uhuru tulikuwa hatuhusishwi sisi. Watu walikuwa hawahusishwi kwa sababu walikuwa hawana elimu. Kwa hivyo ilikuwa ni wachache tu wanaokwenda kwenye Bunge ama wanapelekwa huko uingereza wanazungumza juu ya watu wote katika kenya. Kwa sababu elimu ndio chombo ambacho kinategemewa katika nchi lakini naiona katika upande wa waslimu hasa waalimu wanapuuzwa kwa mambo mengi sana. hasa kwa upande wa mshahara.

Mishahara ya waalimu haiwezi kuangaliwa na serikali yenyewe kwamba wacha tuwape waalimu kiwango fulani ili wasiwe na wasiwasi wasiwe na taabu sababu wao ndio wafunzaji wa watoto wetu, ndio wanatupa elimu, ndio ambao wanatufanyia vitu mpaka tumeanza kuona mbali. Kwa hivyo ningeomba serikali iwapatie mishahara waalimu kiwango ambacho kingewarithisha ambacho hawezi kuwa mpaka wagome ndio waanze kupandishwa. Serikali yenyewe ikate shauri kwamba tukiwapa walimu wetu wa hapa ama tukiwafanyia hivi bas! Na tutakuwa hatutaweza kusema zaidi kama kwa mfano serikali imetuangalia kisawa sawa.

Kama vile vile elimu na afya tumesema iwe bure. Iwe bure kama vile wenzangu walivyozungumza. Wengine nimesikia wazungumzaji wengine wakisema kwamba zitatoka wapi hizo pesa za kuhudumia elimu bure na afya bure. Mtu binafsi mwenyewe anaandika Kadhi kwa sababu ya kuhudumia maneno matatu manne hivi. Yaani anaangalia kwa upande wa elimu, anaangalia kwa upande wa magonjwa na anaangalia kwa upande wa umaskini wake, mtu binafsi.

Serikali kwa hivyo katika zile resource zile rasilimali zake zote, huwa ngapi? Lazima wazifanye ili ziwe zinahudumia mambo kama haya ya elimu na afya. Maana hivi ndivyo vitu ambavyo ni muhimu kwa mtu ambaye ameelimika na mtu ambaye hakuelimika pia kwa sababu katika kenya kuna watu aina kama mbili hivi walio wasomi na ambao hawakusoma.

**Com. Swazuri:** Asante sana na uandike pale kwa sababu tutakwenda kusoma memorandum kwa hivyo hakuna haja ya kueleza.

**Mr. Hassan:** Okey, basi nimesema hivi kwamba elimu iwe bure, na afya bure na waBunge wawe wanachaguliwa na watu wote katika hapa kenya. Na kura zikipigwa ziwe zinapigwa na msomi na hata ambaye hakusoma lakini ikifika wakati wa ikiwa ameshapata huwa serikali inachagua ambao waliosoma peke yao, waliokosa kusoma hawatambuliwi kidogo. Kwa hivyo naomba Majimbo, ile serikali ya Majimbo ikiwako, iwe watu hawa wote wanatambuliwa kisawasawa kwa sababu hawa wote ni watu wa kenya. Asante.

**Com. Swazuri:** Eddie Mwakaba. Dakika tano tafadhali na uwe focused.

**Mr. Mwakaba:** Nashukuru kwa Commissioners na wasikilizaji wenzangu ambao mmekuwa pamoja nami. Point yangu ya kwanza na maoni yangu naonelea kwamba upande wa elimu ningeonelea elimu iliyokuwa ya zamani ile ya 7-4-2 halafu miaka nne hiyo ndiyo iliyokuwa elimu yenye heshima. Oni lingine la pili naonelea ya kwamba yeyote mfanyi kazi ambaye ni wa serikali katika nchi yetu ama katika sheria tunazoziunda, mtu yeyote atakayepatikana ame-mess up with the government funds, yule mtu achukuliwe sheria sawa sawa kama inavyotakikana. Si kama vile ilivyo wakati huu tunakuwa tunaimba corruption halafu mtu ana-collect milioni moja anapelekwa mahali pengine pia anaenda na kuendelea na kumaliza zaidi ile alikuwa amebakishia.

Kwa hivyo afungwe sawasawa kabisa na ikiwezekana hiyo pesa inyakuliwe ile yenye alikuwa amenyang'anya watu. Point no. 3 majimbo kwa upande ya serikali ni sawa nakubali hayo kwa upande wangu ili pesa yote ifike kila mahali katika sehemu za nchi igawanywe sawa sawa ili iweze kufikia kila mmoja mahali alipo katika nchi hii yetu tuliyonayo.

Upande wa utawala maombi yangu ni kwamba upande wa chief and sub-chief tulio nayo, ningeonelea kwamba ni vizuri wangeliweza kuwa within the division ile ambayo ma-subchief huwa wangelikuwa waki-rotate ama kufanya transfer. There can have transfer within the division ile ambao wako wanatawala. Pia kwa upande wa sub-chief, ni ombi langu ya kwamba ningeonelea ni vizuri kuwa wangeweza kuwa wameajiriwa kupitia wako elected na watu wenyewe. Wamechaguliwa na watu wenyewe ili wakitumia ofisi vibaya pia wananchi wana mamlaka ya kusimamisha na kusema tunataka mwingine lakini sasa tukiandikiwa tunangoja retire ama kifo na hapo tunaumia sana maana hafi haraka na anatuumiza. Hatuiti mikutano na tunaendelea. Kwa hivyo hapo tunaumia sana.

Lile lingine ni kana kwamba katika ulimwengu wa leo, mtu anatoka shule leo anaandikwa miaka mitatu, tayari millionaire. Hiyo ndio tunasema, tunauliza ya kwamba serikali ijayo kuwe na accountability vile mtu angeweza kuthihirisha mapato yake vile amepata hiyo pesa tayari anunue ndege baada ya mwaka moja. Kwa hivyo awe akichunguzwa, tuseme uchunguzi wa vile anapata mali yake yule mtu. Hiyo ndiyo ambayo ile tunaita kuchunguza mali yake. nafikiri hizo mmezipata hizo ni points, naenda sasa kwa kiwango cha points zile nimeandika na wameniambia ile nyingine ni ombi langu la kwamba waBunge tunaowachagua, ule mshahara hujawahi kupatikana ulimwengu huu ni mkubwa zaidi.

Makamishina hili jambo liwekwe kwa uzito ya kwamba mshahara huu ni mwingi upunguzwe ili tuweze kupata kazi wale ambao tumetoka mashule na tumekosa kazi. Hii mshahara inaweza kuandikwa nayo karibu watu mia mbili kwa mtu mmoja na tunakula. Maana oxygen ni mmoja dunia hii na tuna-breath, sote tuko sawa pamoja.

Point yangu ya mwisho ni kwamba ningeonelea serikali ya kenya ijapokuwa matatizo yako na shida ziko wafungwa wako wanaopatikana lakini wanapofungwa hapa jela unakuta ya kwamba yule mtu hakuwa anakula na anakaa lakini ni ombi langu ya kwamba wafungwa pia badala kule kufanya kazi kidogo unakuta kwamba ni kama hata mtu akitolewa tena anaweza kufanya makosa tena ili arudishwe ndani. Wawe wanafanyia kazi serikali ni kazi mzito hata kama kujenga hii madaraja kujenga mabarabara hii ndio kazi ile ambayo ina faida ambayo inaweza kusaidia nchi na halafu zile pesa zingine ambazo zingeandika watu zifanye kazi zingine. Kwa ma-prisoners wale ambao wamefungwa wawe wanafanya kazi na inaweza leta biashara kubwa katika nchi yetu. Asante sana makamishina.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Sasa ni bwana Juma.

**Mr. Juma:** Commissioners na wengine ambao mmehudhuria, salaam aleikum. Mimi yangu ni machache kwa sababu mengi yamesemwa tena vile vile tumeongea mengi huko Golini wakati tulipokuwa tunachaguachagua hii mambo ya Katiba hii yetu. Kwa hivyo mimi ni kama kuongeza kitu kidogo au viwili.

Kwanza ningesema kwamba hii Katiba ambayo tunaitarajia kuiandika sasa ni ya Majimbo. Halafu katika Majimbo, utamaduni iangalie tamaduni za wadigo na maadili yao. Kwa mfano wadigo hapo mbeleni walikuwa na kitu kinaitwa ngambi. Kwa hivyo ngambi ihifadhiwe sana kwa sababu ngambi ndio karibu kipengele ambacho kinaangalia sana sheria za wadigo.

Kwa mfano kama unataka kuweka kitu fulani, quarantine ya nazi au quarantine ya maembe walikuwa wanaketi halafu wale kamati ya ngambi inapitisha unaona kwamba hakuna mtoto au mtu mwingine kuangusha nazi au kuangusha vitu vingine bila ruhusa yao. Kwa hivyo kitu kama hiki ni kitu ambacho kinachunga nchi sasa kwa hivyo tunataka Katiba ambayo inaiandika hapa itilie maanani hiyo kitu inaitwa ngambi. Kadhalika tukija kwenye ngambi vile vile tuangalie kitu kinaitwa makaya. Wadigo kuna vitu tunaita makaya.

Kwa hivyo hizi kaya zihifadhiwe vile vile kwa sababu ndio vitu na mambo ambayo yanaficha siri sana ya wadigo. Kwa hivyo hivi vitu ni vitu muhimu na vile vile sheria zake zihifadhiwe kwa sababu katika kaya hakuna mtu yeyote anaweza ruhusiwa kuingia kaya lakini sasa tunaona kwamba kaya zimeharibiwa nyingi sana, watalii wameingizwa huko na wameanza kuharibu mambo mengine mengi ya utamaduni.

Kwa hivyo tunataka hizi kaya zihifadhiwe na zilindwe ili kama ni mtalii ataenda huko asiruhusiwe kwa sababu hiyo ni siri ya wadigo. Nyingine, ni kitu kinaitwa mnazi. Katika kenya tuna coffee authority, tuna tea authority lakini hapa Pwani ambapo kuna

mnazi ambao ni uchumi wa nchi katika hapa Pwanilakini hii kitu haikufanyika katika sheria ya kenya.

Kwa hivyo katika Katiba hii ambayo tunaitarajia kuiandika mnazi uingizwe kwenye sheria na iwe na authority yake ili wakati tumetengeneza mambo yetu tunapata masoko, tunatafuta wahifadhi ambao wanaweza kuiongeza ili ipandwe namna gani nazi ili iwe nyingi zaidi. Kwa hivyo hii ni kitu muhimu sana.

Na kitu kingine ni akina mama. Majina ya akina mama yamebadilishwa yakuwe ya mabwana zao. Sasa hiyo inaleta matatizo kwa sababu mara ingine hujui mtoto ni yupi, bibi ni yupi. Kwa hivyo tunataka tutofautishe kwamba yule mtoto awe ni mtoto nimemzaa mimi mwenyewe. Jina lake sawa sawa achukue jina langu lakini yule bibi yangu achukue jina la babake huko alikozaliwa, asichukue jina langu mimi. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Swazuri:** Haya, bwana Omari.

**Mr. Omari:** Commissioners, mabibi na mabwana salaam aleikum. Mimi jina langu naitwa Omari Jarumata. Kwa kusema kweli makamishina mnasema tunarudia maneno maneno lakini mimi nitarudia kwa sababu kila yakirudiwa ndio mtajua kumbe hawa wote wanataka yale yale na mimi hapa naanza, nataka mjue mimi naunga mkono wale wenzangu waliotangulia kwa mambo ya Majimbo. Pendekezo la pili, hata iwe ni hayo Majimbo lakini wale watakaosimamia wahakikishe wananchi wanapata elimu ya bure, matibabu ya bure, maji ya bure, umeme usambazwe kila mahali na nitaingilia ufisadi.

Nafikiri ni wale wako katika mamlaka ndio wanasababisha huo ufisadi. Kwa mfano kama hao hawatazingatia kuwalipa mishahara watu wale wamewaajiri nitoe mfano natoa mfano kama machiefs na wale watumishi wa serikali itakuwaje mtu kama chief umpatie basic salary ya shillingi elfu tatu? Hiyo ina maana kuwa atanyanyasa wananchi kwa kuombaomba kwa sababu yeye mwenyewe hazimtoshi. Kwa hivyo serikali ipeane mishahara ya kisawa sawa. Pili nazungumzia habari ya security ama usalama wa wananchi. Mapolisi wahakikishe kuwa wanapeana heshima kwa wananchi wanapokuwa pengine wamekosea. Kwa mfano mtu achukuliwe pale kwa heshima. Sio tu kuchuliwa pale kama ambaye anaenda kuuawa.

Tatu ningependa kueleza makamishina mchukulie maanani kwamba watu wengine wanasema eti politicians mpaka awe na elimu ya na kiwango ambacho kinazidi hivi na vile lakini mimi kwa maoni yangu nasema hivi. Ule mtihani wa kiingereza na kiswahili bora tu mtu aweze kupita mitihani hiyo miwili basi aweze kuorodheshwa na aweze kuwa mgombea moja kwa moja kwa sababu mBunge linahitaji mtu achangie mswada wa kimaana wala sio elimu.

**Com. Swazuri: (Inaudible)**

**Mr. Omari:** Kuwe na mtu ambaye kwamba ana hekima ya kujua huyu ni msomi na huyu si msomi. Tatu, ninasema kuwa hawa wanaogombea viti kwa mfano kama mayors, waBunge na Rais, uchaguzi wao mimi nataka uwe siku moja kwa maana, yaani

wakati mmoja kwa sababu itakuwa ni gharama kubwa sana kwa kuita wachaguzi kila mara. Kwa hivyo unapofanya siku moja, unapunguza gharama.

Ardhi, nasema kuwa mtu aachwe amiliki ile ardhi yake bora tu hapo mahali ni pake, sio kama vile ilivyo Katiba ya sasa kuwa futi mbili huko chini zikishazidi basi ni mali ya serikali. Ikiwa itatokea lolote lile la maana hana haki mtu kama yule kuweza kumiliki. Kwa hiyo ikiwa anaweza kumiliki huko juu hata katika mbinguni kwa nini asimiliki huko chini mpaka uwezo wake vile anaweza. Ningependelea ingawaje wamama wengi watanichukia lakini swala hili la gender liachiwe waislamu katika huu mkoa wa pwani.

Swala la urithi, waachiwe waislamu wenyewe kwa sababu kitabu cha waislamu kimekamilika ambacho, kina sheria hizo zote na kinaweza kuhukumu mambo hayo yote. Hapa Pwani nafikiri waislamu ndio majority.

**Com. Baraza:** na wale ambao ni minority?

**Mr. Omari:** Nafikiri hao wataangaliwa na serikali kuu kwa sababu tutakuwa na central government. na katika wale ambao wanasimamia viti pengine kama Rais, Bunge ama councillor wawe wanaangaliwa tabia zao. Awe mtu pengine si mhuni, anaye bibi, si mkora, si mvutaji bhangi, si mlaji unga, ana tabia nzuri anapendeza mtaani na anapendwa na watu ndio mtu kama huyo anaweza kuchaguliwa wala si mtu tu ambaye wamehongana mapesa na nini na nini, na vile vile awe mtu yule ambaye anachagua yule mBunge ama councillor ikiwezekana awe ni mtu wa pale pale kwa sababu ikiwa atatokeza watu wa kutoka nje pengine ameenda kununua kura nje na pale nyumbani hapendwi, hawezi kuwa kiongozi mwadilifu na akawa anaweza kufanya maslahi ya wananchi katika pale mahali alipochaguliwa.

La mwisho kabisa nasema itiliwe maanani walemavu. Walemavu ni wa kila aina wale wasiojiweza kutembea, wale mabubu, chongo, vipofu, viziwi wale hawatambuliwi na serikali, na serikali ihakikishe kuwa inapojenga mijengo pia in such a way kuwa hawa walemavu nao wawe wanaweza kuingia hapo bila ya vizuizi vyovyote vile. Kwa hayo mengi au machache, nataka nikomee hapo ili nisiwape kazi ya kuandika maana mmeandika muda mrefu. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Andika jina lako pale.

**Mrs. Riziki Mwachai:** Makamishina wote, wageni wetu hapo, mabibi na mabwana salaam aleikum. Yangu ni machache tu. Naitwa Riziki Mwachai natoka kwa women’s development group Kwale. Jambo la kwanza, kuna mambo haya ya mashamba. Katika mambo ya kumiliki shamba, nafikiri kuna wasemaji wengine hapo waliozungumza habari ya mtu kumiliki shamba kama amekaa kwenye shamba lile kwa muda wa kama wa miaka kumi na mbili aweze kupatiwa lile shamba liwe ni lake asiitwe squatter tu akawa ni squatter wa milele na pale pahali yeye ameishi zaidi ya miaka kumi na mbili, amelima vitu vyake na amekuwa na makao yale kwa muda mrefu. Kwa hivyo twaomba katika Katiba mtu kama aweza kuishi hapa pahali kwa miaka

kumi na mbili au zaidi asiitwe squatter tena serikali impatie pale pahali pawe kwake.

Kitu cha pili, ni kuhusu waBunge na macouncillor. Sisi wananchi twapatiwa hawa waBunge na ma-councillor, lakini twaomba wananchi waelimishwe kazi za macouncillor zijulikane. Ajulikane huyu councillor kazi yake muhimu ni ipi kwa mwananchi. Sio councillor tu kuchaguliwa tu halafu wananchi hawaoni huduma za councillor kisawasawa. Asiwe ni councillor kuwa mwananchi ajua mimi nikipatiwa pesa basi huyu ni councillor. Ala! Ajulikane concillor akichaguliwa umuhimu wake ni nini?

Jambo la tatu, ni katika magawanyo ya kazi. Serikali hugawanya kazi katika provinces. Sisi kama watu wa Pwanitwalalamika hizi kazi zikitoka. Tutaona mfano askari wamechaguliwa hapa Kwale lakini tutaona nafasi kubwa itapatiwa watu kutoka juu watoto wetu hapa watarudi nyumbani aweza kuchukuliwa mtu mmoja tu. Na huyo mtu mmoja na aliyechukuliwa hizo taabu atakazozipata kabla hajachukuliwa hata hiyo kazi atakuwa hana raha nayo. Kwa hivyo twaomba serikali ikiwa itafikiria mambo haya magawanyo ya kikazi, watoto wetu wafikiriwe na waweze kupatiwa nafasi ya kutosha. Ikiwa ni asilimia watoto wanaotakikana ni hamsini, basi asilimia watoto thelathini watoke hapa pwani, wale ambao wamekuja kufanyiwa yale mazoezi waweze kuchaguliwa. Isiwe sisi twalia watoto wamebaki hapa na tukifika huko watoto waliochukuliwa ni wa kutoka juu na sisi twajua watu wa juu wamegawanyiwa nafasi zao na watu wa Pwaninao wamegawanyiwa nafasi zao.

Kitu kingine kuna wakati kulikuwa na district focus. Hii district focus ilipokuja tuliona ilitusaidia sana wakati huo. Watu walipata makazi, waalimu walichukulia wale wale waliotoka hapa na kazi nyingine. Tungeomba hii district focus irejeshwe kwa nini ililetwa kwa muda mfupi na ikaondolewa na tuliiona faida yake.

Kitu cha nne, nazungumzia upande wa wanawake. Wanawake wapatiwe maternity leave baada ya kuwa amezaa mtoto wake tu aambiwe hii ndio maternity yako leave na apatiwe miezi mitatu aweze kupumzika vya kutosha.

**Com. Swazuri:** Na je, bwana?

**Mrs. Mwachai:** Hata ikiwezekana bwana apatiwe maternity leave amsaidie bibi yake kwa miezi mitatu. Jambo lingine, kuna katika uislamu wetu kuna wanawake hufiliwa akiwa makazini na kuna neno eda wanawake hukaa. Hii eda tunavyojua mwanamke anatakikana akikaa hiyo eda asiweze kukaribiana na mwanamume wala asishikaneshikane na mwanamume kwa miezi minne na siku kumi. Sisi twaambiwa sasa mtu akifiliwa aende kazini. Kule kazini anakaa karibu na wanaume anawasalimia yaani hakuna tofauti yoyote ya kuwa huyu ana eda na huyu ana eda.

Tungeomba wale akina mama wa eda ikiwa itawezekana wapatiwe ruhusa ya kukaa ile miezi minne na siku kumi na walipwe. Wasiambiwe wamekaa halafu wafutwe kazi. Walipwe pesa zao za miezi minne na siku kumi zikiisha warudi kazini.

Kitu kingine, kuna hii siku ya Ijumaa. Wenzetu wakristo walibahatika wana jumapili ambayo ni siku ya mapumziko kwa kila

mtu. Lakini waislamu yetu ni Ijumaa. Kwa hivyo twaomba katika hiyo Katiba hii Ijumaa kama itawezekana mwislamu apatiwe ruhusa. Kama si ya siku nzima lakini asiende akiswali Ijumaa akimaliza. Aweze kumpumzika kwa ule muda mfupi uliobakia. Asiwe siku ya Ijumaa pia yuafanya kazi ni siku ya maombi. Twaomba katika katiba, sisi waislamu tuwekewe hiyo siku. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Nenda pale uandike jina lako. Kulingana na majina ya watu niliyoyapata nimeyamaliza. Kwa hivyo tumeshukuru sana au kama kuna mtu ambaye tumemwandika na hatukumtaja hapa anyooshe mkono. Kwale hapa naona list yangu watu wote waliojiandikisha kasoro Amina Ali ambaye hakuweko na Mwanakombo Mkono hao wengine wote nimewaita na wamefika. Kwa hivyo nafikiri tumeshukuru mmefika nyote, wewe bwana ulikuwa hapa wewe. Tukisema hivyo tutaanza tena upya kwa sababu kila mmoja ataona nafasi yakuandika. Lakini tunakwambia leo sio mwisho wa kukusanya maoni hapa. ikiwa una maneno mengine zaidi unataka kutupa kuna ofisi yetu. Pale commercial bank ya zamani.

Una ruhusa kupeleka memorandum pale au kukutumia direct mpaka Nairobi au wakati ule tukirudi maanake tutarudi na hii ripoti yenu. Tutakwenda kuandika halafu tutarudi hapa. tutarudi tena tukae kwa kama siku sitini hivi. Na tutampatia kila mtu tena kama hivi hivi nafasi tena. Kwa hivyo pia hapo kuna nafasi. Siku ya mwisho ya kukusanya maoni ni ile siku ya kikao cha kitaifa kwa hivyo tuko na muda. Wale ambao wanataka tunawaomba mzidi kutoa maoni yenu kupitia kwa ofisi yetu kupitia kwa district coordinator. Kwa hayo machache tunawashukuru sana hasa wale ambao mmekuwa nasi kutoka asubuhi. Kwa hivyo tutampatia mzee mmoja atufungie kwa dua. Ni nani hapa mzee Ali. Tafadhali.

**Mzee Ali:** (Prayers) Ee Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Tunakushukuru umetuleta hapa kutoka asubuhi mpaka saa hizi lakini hatukuketi bure tumeketi kwa mambo ambayo yanahusu waja wako. Na hayo tuliyozungumza yote tumezungumza kwa nguvu zako Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu. Uyabariki, hayo tuliyozungumza yawe kamishina wetu uliomchagua wewe Mwenyezi Mungu mwenyewe ukiwapa nguvu ukiyachukua na kuyatengeneza kama yawe sasa kama tunavyotaka, ee Mwenyezi Mungu ututegee heri sisi tuliokuja hapa turudi nyumbani kwa njia nzuri, ee Mwenyezi Mungu ututegee heri sisi tuliokuwa unatufikiri zaidi ili makusudi tukiitengeneza hii nchi iwe nzuri. (Arabic)

**Com. Swazuri:** Asanteni sana na muende salama.

Meeting ended at 5.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&**